

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA TATU

Kikao cha Tisa – Tarehe 14 Aprili, 2021

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Akson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, sasa aulize swali lake.

Na. 69

**Ujenzi wa Vituo vya Afya kwa Nguvu za Wananchi - Lushoto**

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Jimbo la Lushoto lina Kituo kimoja cha Afya na sasa wananchi wameanza kujenga Vituo vya Afya viwili vya Gare na Ngwelo.

Je, Serikali ipo tayari sasa kutoa fedha kwa ajili ya kumalizia vituo hivyo na ni lini itafanya hivyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa za Serikali za Mitaa, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Jimbo la Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha huduma za afya katika Wilaya ya Lushoto kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 - 2019/2020, Serikali imetoa shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wodi ya wazazi katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto pamoja na ukarabati na upanuzi wa Vituo vya Afya vya Mlola, Kangagai na Mnazi ili kuvizezesha kutoa huduma za dharura za upasuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Machi 2021, Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto shilingi milioni 150 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma matatu ya zahanati. Serikali inatambua na kuthamini juhudhi za wananchi wa Jimbo la Lushoto katika ujenzi wa Vituo vya Afya. Serikali itaendelea kujenga na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya nchini, vikiwemo vituo vya afya vilivyoanza kujengwa kwa nguvu za wananchi Jimboni Lushoto kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swalii la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kituo cha Afya cha Mlola ndiyo kituo pekee kinachohudumia zaidi ya kata nane lakini kiuo kwa muda mrefu hakina gari la wagonjwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka kuwapatia Kituo cha Afya Mlola gari la wagonjwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, vituo hivi vyatia Gare na Ngwelo ni vituo vilivyojengwa na nguvu za wananchi kwa muda mrefu sana. Vituo hivi nilianza kuviongelea tangu 2017, 2018, 2019, 2020 mpaka sasa hivi 2021 lakini hakuna majibu ya kuridhisha, majibu ni haya ya nadharia bila vitendo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari sasa kuongozana nami ili akaone kazi iliyofanywa na wananchi wale? Nadhani hapo ndipo atatupa fedha za kujenga vituo vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Festo John Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shabani O. Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Mlola kinahudumia wananchi wengi, kata nane katika Jimbo lile la Lushoto na ni kituo muhimu sana kuhakikisha kwamba kinapata gari la wagonjwa ili kiweze kufanikisha rufaa lakini pia na huduma dharura kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Lushoto. Naomba nimhakikishe Mheshimiwa Shekilindi kwamba Serikali inatambua kwamba kituo hicho kinahitaji kuwa na gari la wagonjwa na taratibu za kupata magari ya wagonjwa katika kituo hicho lakini pia katika Vituo vingine vyatia Afya zinaendelea kufanyika na tutaeendelea kupelekeea magari hayo kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo, naomba nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hilo tumelichukua na tunalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusiana na Vituo vyatia Afya vyatia Gare na Ngwelo kuanza kujengwa kwa nguvu

za wananchi kwa muda mrefu, kwanza, Serikali inawapongeza sana wananchi wa Lushoto kwa kujitolea kuchangia kuanza ujenzi wa Vituo hivi nya Afya. Serikali inatambua sana mchango wa wananchi na itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuunga mkono nguvu za wananchi katika kukamilisha vituo hivi nya afya. Naomba nimhakikishie, pamoja na kwamba vituo hivi kwa muda mrefu vimekuwa vikiahidiwa kupatiwa fedha, jitihada zinaendelea kuendelea kutafuta fedha na mara zitakapopatikana Vituo hivi nya Afya vitapewa kipaumbele.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Changamoto zilizopo Jimbo la Lushoto zinapanana kabisa na zilizopo Jimbo la Meatu kwa kuwa ni Kituo cha Mwanhuji pekee kilichoongezewa miundombinu ambacho pia kinatumika kama Hospitali ya Wilaya.

Je, Serikali haioni haja ya kuongeza miundombinu katika Kituo cha Afya Bukundi ili kukabiliana na wagonjwa ambao pia wanachangizwa na wagonjwa kutoka Wilaya ya Mkalama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Leah Komanya, Mbunge wa Meatu, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Bukundi katika Jimbo la Meatu ni muhimu sana na kwa bahati njema nakifahamu vizuri nikiwa nimefanya kazi huko kama Mganga Mkuu wa Mkoa wa Simiyu. Nafahamu kwamba tunahitaji kukiboresha na kukitanua kituo kile ili kiweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi kwa sababu

kipo pembezoni sana na eneo lile kuna umbali mkubwa sana kufika kwenye vituo vingine vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge Leah Komanya kwamba Serikali inatambua umuhimu huo na mipango inaendelea kufanywa kutafuta fedha. Mara fedha zikishapatikana tutahakikisha kituo hicho ni miongoni mwa vituo ambavyo majengo yake yatakwenda kupanuliwa ili kiweze kutoa huduma bora zaidi za afya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala hili linafanana kabisa na Vituo vyangu vya Kisesa na Nyanguge, ni vituo vya siku nyingi ambavyo havitoi huduma inayostahili kwa wananchi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha hasa kufanya ukarabati na kuvipatia vifaa vya kutolea tiba katika Vituo vya Nyanguge na Kisesa? (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, Mbunge wa Magu, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kusema kwamba sisi sote Waheshimiwa Wabunge tunafahamu kazi kubwa sana ambayo imefanywa na ambayo inaendelea kufanywa na Serikali yetu katika kuhakikisha kwanza tunajenga vituo vya afya lakini tunakarabati vituo vya afya. Sisi sote ni mashahidi

kwa kipindi hiki cha miaka mitano jumla vituo vya afya vипатаво 487 vimeendelea kujengwa na kukarabatiwa na vimeanza kutoa huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba hatua moja inatupelekea kuendelea na hatua nyingine. Naomba nimhakikishe Mheshimiwa Kiswaga, kwanza kuhusiana na Kituo cha Afya cha Kisesa na Nyanguge kwamba vinahitaji ukarabati, ni kweli na suala ambalotunakwenda kulifanya ni kuanza kuweka taratibu za ukarabati na upanuzi wa vituo hivi kadri ya upatikanaji wa fedha. Tuna kata nyingi, tutakwenda kwa awamu, si rahisi kumaliza vituo vyote kwa pamoja lakini vituo hivi vyote ni kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na vifaatiba, naomba niwakumbushe watendaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, maelekezo yalkiwishatolewa Serikali imekuwa ikigharamia ujenzi wa vituo hivyo, kuanzia hospitali za halmashauri, vituo vya afya na zahanati.

Katika hospitali za Halmshauri tumetenga bajeti kwa ajili ya vifaa tiba lakini katika vituo vya afya, tumewaelekeza Wakurugenzi katika mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga fedha ili tuweze kununua vifaatiba.

Kwa hiyo, ni muhimu sana Mamlaka ya Halmashauri ya Magu wahakikishe wanatenga fedha katika mapato ya ndani na fedha zipatikanazo na malipo ya *cost sharing* ili kununua vifaatiba. Kwa ujumla, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuboresha miundombinu hii kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mrisho Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, sasa aulize swalı lake.

Na. 70

**Hitaji la Stendi ya Kisasa - Jiji la Arusha**

**MHE. MRISHO M. GAMBO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga stendi ya kisasa Jijini Arusha ili kukidhi mahitaji ya Wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Jiji la Arusha imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 30 katika eneo la *Bondeni City* kwa ajili ya ujenzi wa stendi mpya ya kisasa. Stendi mpya itakayojengwa itazingatia pia mahitaji ya wafanyabiashara wadogo kama Machinga, stendi ya teksi, pipipi, bajaji, Ofisi za Polisi wa Usalama Barabarani na maeneo ya huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi inayoendelea sasa ni taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu wa mradi huo. Mradi huu wa ujenzi wa Stendi ya Kisasa Jiji la Arusha utajumuishwa kwenye Mradi wa Uboreshaji Miundombinu yaani *Tanzania Cities Transforming Infrastructures and Competitiveness - TACTIC* utakaoteklezwa kwenye Halmashauri 45 za Majiji, Manispaa na Miji nchini ambapo Serikali inaendelea na majadiliano na Benki ya Dunia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mrisho Gambo, swali la nyongeza.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, napenda nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo, lakini ujenzi wa stendi hii ultakiwa uanze toka mwaka 2010/2011 ambapo Serikali iliweza kuzuia maeneo ya wananchi wa Kata za Moshono na Kata za Olasiti na maeneo hayo yaliwekwa mpaka kwenye *master plan* ya

Jiji la Arusha. Sasa hivi Serikali imefanya maamuzi ya kwenda kujenga stendi kwenye eneo lingine la *Bondeni City*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali yangu ya nyongeza, napenda kufahamu kwanza, je, sasa Serikali ina mpango gani na yale maeneo ya Olasiti na Moshono ambayo yalitengwa maalum kwa ajili ya kujenga stendi na yameishingia kwenye *master plan*? Je, Serikali sasa hivi inawaruhusu wananchi wale waende wakayaendeleze maeneo yao? Je, wako tayari kupabilisha *master plan* au Serikali inao mpango wa kulipa fidia?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wa siku wananchi wale walitarajia kwamba Serikali ingeweka shughuli yoyote ya kiuchumi pale, hata kama sio stendi, pengine soko au shughuli yoyote, ingesaidia shughuli za kiuchumi za watu wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la nyongeza ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mrisho Gambo ushauiliza maswali matatu tayari katika swalii lako la kwanza la nyongeza na maswali yanayoruhusiwa ni mawili. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunielewa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Jimbo la Arusha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali kwa dhamira ile ya kuhakikisha inaboresha miundombinu ya vitega uchumi kwa maana ya miradi ya kimkakati katika Jiji la Arusha, ilitenga maeneo haya na mradi huu ultarajiwaa kuanza mwaka 2010/2011. Yale maeneo ambayo yalitengwa awali, ni yale ambayo wananchi walihidiwa kwamba

watafidiwa lakini pia ili kitega uchumi kiweze kujengwa eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sababu kadhaa ambazo zilifanya Halmashauri ya Jiji la Arusha lakini na Serikali kuona ni vema sasa eneo la *Bondeni City* ambalo ni kubwa na linaweza likasaidia zaidi kwa maana ya *geographical location* yake kuwa na stendi ya kisasa ambayo itasaidia zaidi kuboresa mapato lakini pia huduma kwa wananchi wa Arusha. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mrisho Gambo kwamba nalichukua jambo hili twende tukalifanyie tathmini zaidi, tuweze kuona sababu ambazo zimetupelekea kuhamisha kwenda sehemu nyingine lakini tuweze kuona nini kitafanyika sasa katika lile eneo ambalo mara ya kwanza lilikuwa limedhamiriwa kujenga stendi ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sehemu ya pili naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mrisho Gambo, kama nilivyotangulia kusema Serikali inadhamiria kujenga miradi hii ya kimkakati yakiwemo haya masoko kisasa. Kwanza kuboresha huduma kwa wananchi, lakini pili kuwezesha halmshauri kupata mapato katika vyanzo vyake vya ndani. Baada ya tathmini hiyo na baada ya kumpata Mkandarasi Mshauri tutahakikisha kwamba tunakwenda kuanza ujenzi wa soko hilo la kisasa katika Jiji la Arusha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya swali Arusha yanahuksika kabisa na Mkoa mpya wa Songwe, yanafanana vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika Mkoa wa Songwe, kuna eneo ambalo lilikuwa limetengwa la Mbimba *TaCRI* kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya Mkoa. Kwa kuwa michoro tayari ilishakamilika kwa muda mrefu karibu zaidi ya miaka sasa mitatu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba stendi kubwa ya Mkoa wa Songwe inaanza kujengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Japhet Hasunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wa Songwe tunahitaji kujenga Stendi ya Kisasa ya Mabasi. Katika majibu yangu ya msingi, nimeeleza kwamba tunatarajia kujenga stendi katika maeneo haya yote ambayo tayari yamekwishatambuliwa na sasa tunaendelea kufanya mazungumzo na Benki ya Dunia ili kupata fedha kwa ajili ya kuwezesha sasa ujenzi wa maeneo haya ya miradi ya kimkakati kuanza. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Hasunga kwamba katika miradl hilo inayokuja, mara mazungumzo yatakapokamilika na fedha hizo kupatikana basi tutaweka kipambele pia katika kuwezesha Kituo cha Mabasi cha Mkoa wa Songwe kuanza kujengwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Atupele Mwakibete, swali la nyongeza.

**MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa changamoto za stendi katika Jimbo la Arusha Mjini, zinafana sana na changamoto za kukosekana stendi katika Jimbo la Busokelo. Je, ni lini Serikali itajenga stendi za Miji ya Ruangwa, Ruangwa Mjini pamoja na Kandete?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala la Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali inatambua uhitaji wa masoko ya kisasa katika Kata hizo ambazo Mheshimiwa Atupele Mwakibete amezitaja, lakini pia katika maeneo mengine kote Nchini. Naomba nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira hiyo ya Serikali bado ipo na mipango ya kutafuta fedha kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa masoko hayo ya kisasa inaendelea. Mara fedha hizo zitakapopatikana tutahakikisha tunatoa vipaumbele katika maeneo hayo ambayo tayari yamekwishatambuliwa ili tuweze kuwekeza miradi hiyo ya kimkakati na kuwezesha huduma kuendelea. Kwa hiyo, naomba nimhakikishe Mheshimiwa Mwakibete kwamba maeneo hayo pia tutayapa kipaumbele mara fedha zikipatikana ili ujenzi wa masoko hayo uweze kuanza.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvubi. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalı lake.

Na. 71

### **Mnada wa Magena – Tarime**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza: -

Je, ni lini Mnada wa Mifugo wa Magena uliopo Halmashauri ya Mji wa Tarime utafunguliwa kama ambavyo Serikali iliahidi Mwaka 2016?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvubi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

### **NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba uniruhusu, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika *podium* hii, nimshukuru sana Mwenyezi Mungu na pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini kuhudumia katika Wizara hii ya Mifugo na Uvubi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizi, naomba sasa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi, nijibu swalii la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mnada wa Mifugo wa Magena, ulikamilika kujengwa mwaka 1995 na kufunguliwa mwaka 1996, ambapo ng'ombe 104,000 waliuzwa na jumla ya Shilingi za Kitanzania 260,000,000/= zilikusanywa kama maduhuli ya Serikali. Hata hivyo, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mara mwaka 1997 iliagiza mnada ufungwe kutokana na changamoto zilizojitokeza ikiwemo wizi wa mifugo na sababu za kiusalama. Uongozi wa Mkoa wa Mara uliwasilisha ombi rasmi Wizarani la kufuta mnada wa Magena na kupendekeza mnada huo uhamishiwe eneo la Kirumi *Check Point*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilijenga Mnada wa Kirumi wa Mpakani kwa gharama ya shillingi milioni 321.3 na ulifunguliwa rasmi tarehe 16 Oktoba, 2018. Aidha, tangu uanze kufanya kazi, jumla ya ng'ombe 34,855, mbuzi na kondoo 5,808 wameingia mnadani hapo na jumla ya shillingi milioni 428.9 zimekusanywa kama maduhuli ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia maoni kutoka mamlaka za Mkoa, Wizara itakuwa tayari kuurejesha Mnada wa Magena kwa kufuata taratibu za uanzishwaji upya wa minada na kwa mujibu wa Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swalii la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nasikitika kwa majibu ya Serikali, bado anarejea mwaka 1997 ilhali swalii langu la msingi limerejea mwaka 2016 ambapo Waziri wa Mifugo *by then* alikuja na Watendaji wa Wizara, wakakaa na Kamati ya Ulinzi na

Usalama wa Mkoa Tarime, Rarya na Mkoa wa Mara na tukakubaliana kwa umoja wetu kwamba Mnada wa Kirumi *Check Point* uendelee na Mnada wa Magena uendelee kwa sababu uko mpakani ili ng'ombe zisipelekwe kuuzwa kwenye Mnada wa Maabel. Maswali yangu mawili ya msingi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kama Taifa tunahitaji mapato; na Waziri amekiri kwa mwaka 1996 tu Serikali ilipata maduhuli ya shilingi milioni 260 kwa kuuza ng'ombe 104,000; na huo Mnada wa *Check Point* tangu mwaka 2014 mpaka leo mmeuza ng'ombe 34,000 tu; ni dhahiri mnada wa mpakani una mapato zaidi: Je, ni lini sasa Serikali itarejea muhtasari wa Kikao ambacho tulifanya mwaka 2016 pamoja na kuambatana na Wizara husika ili twende kwenye Mamlaka ya Mkoa kuhakikisha kwamba Mnada wa Magena unafunguliwa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalı langu la pili; Mnada wa Kirumi hauchukui ng'ombe kutoka Serengeti, Rarya wala kutoka Tarime; ng'ombe zinatoka Tarime, Rarya na Serengeti zinaenda Kenya moja kwa moja; na sasa hivi hamna hayo mambo ya usalama, kuibiwa ng'ombe, hayapo kabisa Tarime; mkiendelea kuongea hivi ni kama mnadhihaki wananchi wa kule: Ni lini sasa mtahakikisha kwamba mnajiridhisha hamna wizi wa ng'ombe kutoka Tarime kwenda Kenya au kutoka Tarime kuja huko Kirumi? Ahsante sana. (*Makof!*)

**AIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvubi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba, tunakiri tunahitaji sana mapato na Serikali imejielekeza katika kuhakikisha kwamba mifugo na uvubi inatoa mchango mkubwa katika pato la Taifa. Ni ukweli kwamba Mnada wa Magena uko mpakani na utoroshaji ni mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa rejea yako ya mwaka 2016 iliyo fanywa ziara ya Mheshimiwa Waziri wa wakati huo

na viongozi wengine, Wizara ya Mifugo na Uvuvi tuko tayari kuhakikisha kwamba maoni haya uliyoyatoa Mheshimiwa Mbunge tunayachukua na kuendelea kuwasiliana na mamlaka za Mkoa na kufanya rejea na tathmini ili kusudi tuweze kwenda kwa pamoja na kuhakikisha tunaongeza wigo wa mapato sawa na matakwa na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jerry Silaa. Swalii la nyongeza.

**MHE. JERRY W. SILAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii moja la nyongeza.

Kwa kuwa pale Pugu kwenye Jimbo la Ukonga kuna Mnada wa Upili na tulishafanya ziara pale na Naibu Waziri wa Mifugo na ziko ahadi alizitoa; tukiwa tunaelekeea kwenye kipindi cha Bajeti, naomba kauli ya Serikali kuhusiana na maboresho ya mnada ule hasa miundombinu ya ukuta, njia za kuingilia na vitendea kazi vya watumishi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Abdallah Ulega, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kwamba Mnada wa Pugu ni mnada wa kimkakati na ni katika minada ambayo inaingiza fedha nyingi za maduhuli ya Serikali. Katika Bajeti ya Mwaka 2021/2022, Serikali kuititia Wizara ya Mifugo na Uvuvi tumejipanga kuhakikisha kwamba Mnada wa Pugu unaboreshwaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara kwa wakati huu tuko tayari kuhakikisha tunatumia mbinu za mapato yetu kuuboresha taratibu wakati tunaendelea kusubiri Bajeti Kuu ya mwaka 2021/2022.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, Mbunge wa Mbongwe, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipo, nipo, nipo; nauliza mwenyewe. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga Mbunge wa Mbogwe, nikuombe radhi kwa sababu Mheshimiwa Musukuma aliandika kwamba umefiwa na umesafiri. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA:** Hapana.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, nikuombe radhi kwa hilo, karibu uulize swali lako. (*Makofi*)

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kweli nimefiwa, lakini msiba ni Jumamosi. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 72

### **Kupeleka Maji ya Ziwa Victoria – Mbogwe**

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Wilayani Mbogwe maji kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya matumizi ya Wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusiwe tunafanya masihara kwenye jambo hili. Kama hujapewa hiyo kazi ya kuuliza swali, tusipoteze muda wa Bunge ambao ni wa muhimu sana. Kuna mambo mazito yanajadiliwa humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Eng. Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa Wilaya ya Mbogwe ni wastani wa asilimia 55. Huduma hiyo ya maji inapatikana kupitia miradi minne ya skimu, visima virefu 26, visima vifupi 460 na matanki 55 ya kuvuna maji ya mvua, vituo vya kuchotea maji 61 na maunganisho ya nyumbani 192.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha huduma za maji, Serikali katika mwaka wa fedha 2020/2021, ilitenga jumla ya shilingi bilioni 2.9 kwa ajili ya upanuzi wa miradi ya maji Lulembela na Nyakafuru, ujenzi wa miradi mipyaa ya maji Mbogwe, Nanda na Kabanga-Nhomolwa. Hadi sasa jumla ya shilingi bilioni 1.8 zimetolewa, ambapo kazi zilizofanyika ni ujenzi wa nyumba ya pampu ya kusukuma maji, matenki matano, vituo vya kuchotea maji 48 na ulazaji wa bomba lenye urefu wa kilometra 31. Utekelezaji wa miradi hiyo unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2021 na kuongeza upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kufika asilimia 61 ifikapo mwezi Disemba, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali kupitia Mpango wa Mradi wa Maziwa Makuu kupitia Ziwa Victoria, katika Wilaya ya Mbogwe itatekeleza miradi katika Vijiji vya Kagera, Ilolangulu, Buningozi, Ngemo, Isungabula na Iponya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemus Maganga, swalii la nyongeza.

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza sijaridhishwa na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji kwamba kuna visima 26 Mbogwe. Naomba tu tuongozane naye akanionyeshe pale vilipo hivyo visima virefu vinavyotoa maji, maana mimi ni Mbunge wa Mbogwe na ninaishi Mbogwe na kuna taabu

kubwa sana katika Sekta ya Maji. Ndiyo maana nikaiomba Serikali sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mbogwe ni Wilaya ambayo ipo karibu na mradi wa maji pale Kahama, ni vyema sasa Wizara ya Maji itupelekee mradi mkubwa wa Ziwa Victoria, maana hivyo visima anavyovisema Mheshimiwa, nakuomba twende na wewe, usifuate mambo ya kwenye makaratasi ukajionee na unionyeshe pale vilipo visima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji. Majibu kwa hoja hizo za Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ombi lake namba moja limepita, kwani huo ni moto wa namna ya kutekeleza majukumu yangu; nimekuwa nikiambatana na Wabunge wengi, hata *weekend* hii tu nilikuwa Mbinga.

Kwa hiyo, mimi kutembea huko, kwangu ni moja ya majukumu yangu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Nicodemus mantahofu, tutakwenda na miradi hii tutahakikisha mambo yanakaa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kupitia mradi wa Ziwa Victoria, hili Ziwa litatumika vyema kwa maeneo yote ambayo miradi hii mikubwa itapitia. Mheshimiwa Nicodemus, wewe ni Mbunge katika Wabunge mahiri, umekuwa ukifatilia suala hili, tumeliongea mara nydingi na umeonyesha uchungu mkubwa kwa wana Mbogwe. Nikuhakikishie, Mbogwe maji yatafika na katika mwaka ujao wa fedha mambo yatakwenda vizuri pale Mbogwe. Tuonane baada ya hapa, tuweke mambo sawa, tuone namna gani tunaelekeea. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Venant Daudi Protas, swalil ya nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Matatizo ya Jimbo la Mbogwe yanafanana vile vile na matatizo ya Jimbo la Igala. Tuna Mradi wa Ziwa Victoria katika Jimbo la Igala, lakini mradi ule mpaka sasa hivi umesimama:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa kupeleka maji katika Kata za Goweko, Igala, Kigwa na Nsololo ili wananchi waanze kutumia maji ya Ziwa Victoria? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Eng. Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mradi ambao tayari utekelezaji wake umeanza ni lazima ukamili. Sisi Wizara ya Maji tunapoanza kazi ni lazima zikamili. Kwa mradi huu ambao umesimama napenda nikutoe hofu Mheshimiwa Mbunge, tuonane baada ya hapa, lakini vile vile wiki ijayo tutaangalia fungu la kupeleka fedha ili pale kazi iliposimama, utekelezaji uendelee na tutahakikisha mradi huu unaisha ndani ya wakati ili maji yaweze kupatikana Igala. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii nami niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa, Mkoa wa Tabora ulifanikiwa kupata maji ya Ziwa Victoria; na kwa kuwa, Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye Kampeni alisema kwamba, sasa maji ya Ziwa Victoria yapelekwe Urambo, Kaliua na Ulyankulu:-

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini sasa mnatarajia kuyatoa maji hayo Tabora Mjini na kuyapeleka Urambo, Kaliua, Ulyankulu pamoja na Sikonge? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Eng. Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Maeneo ya Urambo, Kaliua, Ulyankulu na Sikonge, yote haya tumeendelea kuyaweka katika mikakati ya Wizara kuona namna ambavyo tutaendelea kupata fedha ili maeneo haya yote maji yaweze kufika. Tutafanya jitihada za makusudi kuona kwamba tunapeleka fedha mapema na hii itakuja kuingia mwaka ujao wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swalı la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Naipongeza Serikali kwa usambazaji wa maji ya *Lake Victoria*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, tatizo lililo katika ukanda huo linafanana kabisa na lile la Rombo na wanawake hawa wamezeeka sasa na kutoka upara kwa ajili ya kubeba maji:-

Ni lini sasa Wizara hii itaona ni wakati muafaka wa kusambaza maji ya Lake Chala kwa wale wananchi wa Rombo katika Mji ule wa Holili, Kata za Mahida, Ngoyoni na tambarare yote ya Rombo?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Eng. Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Maeneo ya Rombo Mheshimiwa Shally nimeshafika. Nimeacha maagizo ya kutosha na hata miradi ambayo ilikuwa inasuasua pale niliacha maagizo na utekelezaji unaendelea. Nikutoe hofu kwamba nitarudi tena kuhakikisha ule mradi mkubwa tunakwenda kuutekeleza

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana mama yangu, amekuwa ni mfuatiliaji mzuri pamoja na Mbunge Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, wote mmekuwa mkifuatilia kwa jitihada kubwa. Hatutawaangusha. Sisi Wizara hatutakuwa kikwazo kwenu kwa sababu tunahitaji Wana-Rombo waweze

na wao kupata ladha ya mageuzi makubwa ambayo yako ndani ya Wizara ya Maji. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini.

Na. 73

**Mradi wa Maji kutoka Mto Mavuji - Kilwa Kivinje  
na Kilwa Masoko**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza mradi wa maji kutoka Mto Mavuji kwa ajili ya wakazi wa Miji Midogo ya Kilwa Kivinje na Kilwa Masoko?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Eng. Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilipata mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India kuitia Benki ya *Exim* India jumla ya Dola za Marekani milioni 500 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika Miji 28. Mji Mdogo wa Kilwa Kivinje na Kilwa Masoko ni mionganini mwa Miji itakayonufaika. Utekelezaji unatarajiwaa kuanza mwishoni mwa mwezi Aprili, 2021 na unatarajiwaa kuchukua miezi 24 kukamilika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza niishukuru Serikali kwa majibu mazuri na ufuatilaji na usimamizi madhubuti wa mradi huu, lakini nina swalii la nyongeza. Mosi, kwa kuwa mradi huu utachukua miezi 24 tangu kuanza kwa utekelezaji wake maana yake ni miaka miwili, lakini pia utakuwa ni mradi wa kutoka katika chanzo cha maji kuelekea katika mijii hii miwili niliyoitaja ya Kilwa Masoko na Kilwa Kivinje, lakini viko vijiji ambavyo vitakuwa mbali na mradi huu. Je, Serikali itakuwa tayari kwa upendeleo wa kipekee kutenga bajeti kwa mwaka huu kwa ajili ya vijiji angalau vitatu vya Nainokwe, Limalyao pamoja na Mandawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji Mhandisi Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Ally Mohammed Kassinge kutoka Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunapoongelea miezi 24 wakati fulani kwa sababu ya changamoto kubwa ya maji ni muda mrefu, lakini naendelea kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo ameendelea kuwa karibu na sisi na kwa hakika namna ambavyo anafuatilia tutahakikisha tunakamilisha vile vijiji sio vitatu, ila kwa sasa hivi kwa mwaka huu wa fedha tutajitahidi tumchimbie kisima kimoja cha maji, lakini hivi vingine vitaingia kwenye Mpango wa Mwaka ujao wa Fedha. Haya maeneo ya vijiji vyake vitatu ambavyo viko mbali na mtandao wetu wa mabomba tutahakikisha tunakuja kuwashudumia wananchi kwa mtandao wa visima.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swalii la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Tatizo la maji liliopo Kilwa linafanana kabisa na matatizo ya maji

yaliyoko Jimbo la Ndanda hasa zaidi upande wa Magharibi kwenye Kata za Mlingula, Namajani, Msikisi, Namatutwe pamoja na Mpanyani. Swali langu, je, ni nini hasa mpango wa Serikali wa muda mfupi wa kuhakikisha kata hizi nilizozitaja zinapata maji kabla hatujaingia kwenye kiangazi kikuu kinachoanza mwezi Julai na Agosti. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwambe kutoka Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuitia Wizara ya Maji wakati wote tunajitahidi sana kuona tunatatua tatizo la maji kwa kutumia vyanzo mbalimbali kwa sababu tuna michakato ya muda mrefu pamoja na kutumia Mto Ruvuma kwa mwaka ujao wa fedha, lakini katika kuona kwamba wananchi tunakwenda kuwapunguzia makali ya matatizo ya maji kwa mwaka huu wa fedha, Mheshimiwa Mwambe kama ambavyo umekuwa ukifutililia mara zote, tumeongea mara nyingi. Kwa hiyo, hili nalo tukutane tuone tuanze na kisima upande upi ili tuweze kupunguza haya matatizo. Maji Ndanda ni lazima yatoke, mabomba yamwage maji, tuokoe ndoa za akinamama, tutahakikisha hawaendi kukesha kwenye vyanzo vya maji. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika Kata ya Masaka yenyе Vijiji vitatu vya Sadani, Wanging'ombe pamoja na Makota havina kabisa maji hata kijiji kimoja. Je, Waziri sasa wakati anaangalia uwezekano wa kupata maji ya kutiririka anaweza hata akatuchimbia visima ili wananchi wa kule waendelee kunufaika na huduma ya maji? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, *Engineer Maryprisca Mahundi*, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nipende kujibu swalii la Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mbunge wa Kalenga. Mheshimiwa Kiswaga ni Mbunge ambaye kwa kweli nimeshazungumza naye mara nydingi na tayari tuna mradi kule tumekubaliana nakwenda kuuzindua.

Nipende kumhakikishia katika masuala ya visima Waheshimiwa Wabunge, hiki ni kipaumbele kimojawapo cha Wizara, tutafika Kalenga, tutachimba visima viwili, yeye ndiye atakayetueleza wapi zaidi kuna tatizo sugu ambalo mitandao ya mabomba ya maji ya kawaida hayafiki, basi visima Mheshimiwa Kiswaga atavipata.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 74

**Kutenganisha Vote ya Fedha za Mikopo ya  
Elimu ya Juu**

**MHE. JUDITH S. KAPINGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenganisha fedha za maendeleo ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Fedha za Bodi ya Mikopo kwa kuzitengea *Vote* tofauti fedha hizi za mikopo ili kuleta tija ya miradi ya maendeleo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
aliijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu swali la Mheshimiwa Judith Salvio Kapinga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ndiyo yenye dhamana ya kuendeleza mtaji watu kwa ajili ya mipango na maendeleo ya Taifa letu. Aidha, lengo la mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, ni kuongeza mtaji watu katika nchi yetu. Hivyo, utengaji wa fedha za mikopo ya elimu ya juu chini ya Fungu 46, ulizingatia majukumu ya Fungu husika ambayo ni kuandaa na kuendeleza mtaji watu kwa ajili ya maendeleo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuongeza rasilimali fedha katika Sekta ya Elimu kwa lengo la kukabiliana na changamoto zilizopo. Hivyo, Serikali itaendelea kutafuta fedha zaidi ili kuendeleza hatua zake za kutatua changamoto zilizopo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. JUDITH S. KAPINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza napenda kuishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini napenda kuwashukuru kwa kuongeza rasilimali fedha katika miradi ya maendeleo ya Wizara. Nina swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha katika Bunge la Bajeti la 2019/2020 ilitoa maelekezo kwa Bodi ya Mikopo kuangalia uwezekano wa kufanyia kazi suala hili. Je, Wizara halioni umuhimu wa kufanyia kazi mapendekezo haya ya Wizara ya Fedha ili shughuli hii ya kuendeleza mitaji watu kama Wizara inavyosema iweze kufanyiwa kazi vizuri kwa kuitenganisha na Fungu 46? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Kipanga majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la nyongeza  
la Mheshimiwa Judith, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile ilikuwa ni  
mapendekezo na yalipendekezwa na Wizara ya Fedha na  
kwa vile yalikuwa ni mapendekezo ambayo yaliletwa kwenye  
Wizara yetu, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa  
mapendekezo hayo tutaendelea kuyafanya kazi na pale  
muda muafaka utakapofika tutawasilisha mbele ya Bunge  
lako Tukufu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Kilimo,  
Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa  
Muleba Kusini, sasa aulize swalii lake.

Na. 75

**Miradi ya Kilimo cha Umwagiliaji Kyamyorwa  
na Buhangaza**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza: -

(a) Je, ni lini miradi ya kilimo cha umwagiliaji ya  
Kyamyorwa na Buhangaza iliyopo Wilaya ya Muleba  
itakamilika na kuanza kutumika?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza Bonde  
la Mto Ngono kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo,  
Mheshimiwa Hussein Bashe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa  
Kilimo naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Oscar Ishengoma  
Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini kwa Pamoja, kama  
ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Skimu ya Buhangaza na Skimu ya Kyamyorwa zilizoko Muleba Kusini zote mbili kwa ujumla zina eneo la ekari 700. Wizara ya Kilimo imeshafanya kuendeleza jumla ya ekari 215 na ili kuhakikisha kwamba miradi ya kilimo cha umwagiliaji inakamilika na kuanza kutumika ikiwemo miradi hiyo miwili, Wizara imeweka vipaumbele. Cha kwanza, ni kuhakikisha kwamba miradi yote ambayo ni kiporo iliyokwishajengwa ili kubaini kama kuna upungufu unaosababisha kushuka kwa ufanisi wa uzalishaji na kufanya tathmini, kuhuisha usanifu uliofanyika awali kwa utaratibu wa kutumia wakandarasi na kuiweka kwenye mfumo wa usanifu na ujenzi kwa maana ya utaratibu wa *force account*. Kwa hiyo tathmini ya awali inafanyika ili kuweza kuangalia mahitaji halisi ya skimu hizo mbili kuweza kuzikamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uendelezaji wa bonde la Mto Ngono, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Serikali ilifanya upembizi yakinifu katika bonde hilo lilitopo katika Wilaya za Misenyi na Bukoba Vijiji na kubaini eneo lenye hekta 11,700 zinatafaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga kuendeleza bonde la Mto Ngono kwa kuanza na ujenzi wa Bwawa la Kalebe lenye uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo milioni 268 ambazo zitawenza kumwagiliaji eneo lote la hekta 11,700. Bwawa hilo litatumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, kuzalisha umeme, maji ya mifugo, ufugaji wa samaki na kuzuia mafuriko. Aidha, Andiko la Mradi limewasilishwa kwa wadau wa Maendeleo na majadiliano ya kupata fedha za utekelezaji wa mradi yanaendelea. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa lengo la Serikali ni kuongeza eneo la umwagiliaji kutoka hekta

561,383 ya mwaka 2020 hadi kufikia hekta 1,200,000. Je, Serikali haioni busara kuhakikisha kwamba hii miradi ambayo imeshaanza badala ya kukimbilia kuanzisha miradi mipyä tuhakikishe inakamilishwa ili wananchi waweze kuzalisha kwa wingi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Mkoa wa Kagera kwa historia yake na jiografia yake ni Mkoa pekee ambao unapakana na nchi nne na nchi hizo nne zina uhaba mkubwa wa ardhi na hivyo uhaba mkubwa wa chakula. Je, Serikali haioni busara kuendeleza hili bonde kuhakikisha kwamba Mkoa wa Kagera sasa unakuwa soko la chakula kwa hizi nchi ambazo zinapakana na Mkoa huo? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kama Wizara *priority* yetu ya kwanza sasa hivi tunachokifanya na Waheshimiwa Wabunge tutakopokuja kwenye bajeti wataona, ni kufanya tathmini na kukamilisha miradi ya umwagiliaji na tathmini tunazofanya ni za aina mbili; moja kuangalia *efficiency* ya miradi ya umwagiliaji iliyopo sasa hivi kama inafanya kazi kwa kiwango ambacho kinatarajiwa na kufanya marekebisho pale ambapo tunahitaji kufanya marekebisho. Pia kukamilisha miradi ya umwagiliaji ambayo tumeshaanza. Hatutakuja na mradi mipyä wa umwagiliaji isipokuwa kukamilisha miradi tulioianza.

Mheshimiwa Naibu Spika, *priority* ya tatu ni kuwekeza umwagiliaji katika uzalishaji wa mbegu, Serikali ina mashamba 13 ambayo hayana mifumo ya umwagiliaji, mashamba haya 13 ndio tutakayoyapa kipaumbele katika bajeti ya mwaka kesho kuwekeza fedha ili yaweze kufanya kazi yote *at optimal level* ili kuweza kuzalisha mbegu bora na kwa wakati na

kuondokana na tatizo la wakulima kutokupata mbegu za uhakika na kuyaacha mashamba *idle* ambayo hayatumiki. Kwa hiyo hivi ndiyo kipaumbele. Niseme tu ndani ya Bunge kwmaba kipaumbele chetu ni kukamilisha hiyo miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Mto Ngonon na umuhimu wa Mkoa wa Kagera, kwetu sisi kama Wizara ya Kilimo na Serikali Mkoa wa Kagera ni moja kati ya mikoa ambayo tunaipa kipaumbele sana na ndiyo tutakapoelekeza nguvu zetu katika kipindi cha miaka mitano. Sababu ya kufanya hivi, mkoa huu *strategically* umeungana na nchi kama alivyozitaja nne, lakini vile vile ni lango kubwa la kuuza mazao katika nchi ya *South* Sudan. Kwa hiyo Mto Ngonon tutaupa *priority kama* tulivyosema katika jibu letu la msingi kwamba tunatafuta fedha na tutawekeza katika hizo hekta 11,700 ili wawewe kuzalisha mwaka mzima. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Skimu ya umwagiliaji ya Kata ya Ndungu ndiyo skimu kubwa katika Wilaya ya Same na skimu hii sasa inakwenda kufa. Sasa nimembembeleza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa muda mrefu, twende akaione, leo naomba aniambie tunakwenda lini? Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, unakwenda lini? Jibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibui swali la nyongeza la Mheshimiwa Anne Malecela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni bahati kubembelezwa na mama. Nikiri kweli Mheshimiwa mama Kilango ameshaniomba twende jimboni kwake na nimhakikishie mama baada ya Bunge hili tutaenda Jimboni kwake pamoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwantumu Zodo, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza swali la moja la nyongeza. Kwa kuwa Mkoa wa Tanga unazungukwa na milima ya Usambara; na kwa kuwa milima hii inatiririsha maji mwaka mzima hasa wakati wa mvua. Je, Serikali haioni haja sasa ya kujenga mabwawa kuzunguka milima hiyo ili kuchochea kilimo cha umwagiliaji? (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zodo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nikiri mbele ya Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba hatuwezi kutoka katika matatizo ya kilimo bila kuwekeza katika umwagiliaji. Huo ndiyo muelekeo wa Serikali na maelekezo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Jambo la msingi ambalo tunalifanya sasa hivi kama Wizara kwanza ni kubadilisha *modalya* Tume ya Umwagiliaji namna ambavyo inafanya kazi yake; mbili tunachokifanya kama Serikali ili kuweza *ku-take advantage* ya maeneo kama Milima ya Usambara lakini na maeneo mengine ya nchi yetu kwa ajili ya kujenga mabwawa katika bajeti mwaka kesho mtaona tumeweka chanzo kipyä cha fedha kitakachokuwa cha Tume ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tutawekeza kununua vifaa wenyewe ili Tume ya Umwagiliaji iwe na uwezo wa kupeleka vifaa kwa ajili ya kuchimba mabwawa na kujenga miradi ya umwagiliaji yenyewe kwa mfumo wa *force account* ili kupunguza gharama kubwa tunayotumia katika maeneo ambayo tunajenga skimu za umwagiliaji, kwa sababu gharama tunazotumia ni kubwa na hatuoni *value for money*. Kwa hiyo tunabadilisha mfumo tutatengeneza mfumo wa

*force account* na tutanunua vifaa wenyewe ambavyo vitakuwa chini ya Tume ya Umwagiliaji kama tulivyofanya katika Skimu ya Pawaga na Ruaha ambako tumetumia vifaa vyetu wenyewe kurekebisha skimu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwaombe Waheshimiwa Wabunge, wasubiri bajeti ya Wizara, wataona mwelekeo wa Wizara katika Sekta ya Umwagiliaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Kama alivyosema kwenye swali lake alilokuwa akilijibu sasa hivi. Ni kweli ili tuweze kufanikiwa katika kilimo ni lazima tu-*invest* kwenye kilimo cha umwagiliaji. Mbali na miradi ya Serikali, wananchi katika maeneo mengi wamehamasika kwenye kilimo cha umwagiliaji wakiwepo wananchi wa Bunda, Kata ya Nyatwali ambayo ina maeneo matatu, Nyatwali, Serengeti na Tamau na Mheshimiwa Waziri Mkuu...

**NAIBU SPIKA:** Swali Mheshimiwa...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** ... alishaenda kuutembelea huo mradi mkubwa na akatoa ahadi pale. Kitu kikubwa ambacho...

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali Mheshimiwa Ester.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika... ndio naenda kwenye swali. Kitu kikubwa wanachohitaji hawana mashine zenyе uwezo mkubwa wa kutoa maji ziwani na kuleta kwenye mradi. Sasa, ni lini Serikali au ina mkakati gani wa kuhakikisha wananchi ambao wameamua ku-*invest* kwenye mradi wa umwagiliaji wanawezeshwa katika vifaa? (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote. Serikali, hasa Serikali za Mitaa, na tumewaandikia TAMISEMI kuwaomba wa-*involve* Serikali za Mitaa, maeneo ambayo mnadhani kuna *quick wings* ambazo tunaweza kuwa na gharama ndogo za uwekezaji na zinahitaji *cost* ndogo karibuni. Na Mheshimiwa Esther nakukaribisha wizarani njoo tuleteeni andiko kama mnadhani kwamba, kuna mahitaji rahisi ya kuweza kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitumie nafasi hii kuwaomba wakurugenzi wa halmashauri. Suala la umwagiliaji na suala la kilimo sio suala la Wizara ya Kilimo peke yake ni suala ambalo linatuhusu pamoja. Tuwaombe wakurugenzi kwa kuwa, moja ya chanzo cha mapato wanachokipata kinatokana na mazao. Ni lazima asilimia 20 ambayo imeelekezwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu inayotokana na sesi ya mazao wairudishe katika sekta ya kilimo, hasa umwagiliaji na ugani, ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu kuweza kujikwamua katika umasikini. Na sisi Wabunge ni Wajumbe wa Baraza la Madiwani na Kamati za Fedha kwa hiyo, tunaomba tusaidiane katika hili.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Nicholaus George Ngasa, Mbunge wa Igunga sasa aulize swalii lake.

Na. 76

**Kutoa hifadhi ya Bonde la Wembere  
kwa Wananchi**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa eneo la Hifadhi ya Bonde la Wembere kwa Wananchi wa Igunga kwa ajili ya kufanya shughuli za kilimo na ufugaji ili kumaliza mgogoro wa muda mrefu katika eneo hilo kwa kuwa Bonde hilo limepoteza sifa ya kuwa Hifadhi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Mary Francis Masanja, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Jimbo la Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Bonde la Wembere ni ardhi oevu inayofahamika Kitaifa na Kimataifa kwa kuhifadhi ndege wa aina mbalimbali ambao huishi na kuzaliana kwa wingi. Eneo hili ni dakio na chujio la maji ya Ziwa Kitangiri na Eyasi, pia ni mapito, mazalia na malisho ya wanyamapori linalounganisha mifumo ya ikolojia ya ukanda wa Kaskazini, Kati, Magharibi na Kusini mwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umuhimu wa eneo hilo, wananchi wameendelea kuvamia eneo la ardhi oevu la Wembere kwa ajili ya shughuli za kilimo, malisho na ukataji miti. Hali hiyo inasababisha mwingiliano wa shughuli hizo na kusababisha migogoro kati ya wakulima, wafugaji na wahifadhi. Pamoja na uvamizi huo, eneo hilo bado lina umuhimu katika shughuli za uhifadhi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa eneo hili la ardhi oevu la Bonde la Wembere na kwa kuzingatia kuwa ni chanzo muhimu cha maji kwa wananchi wa mikoa ya Tabora, Singida na Simiyu, Serikali itafanya tathmini na kutambua mipaka ya ardhi oevu kwa njia shirikishi ya wananchi na Serikali. Na lengo ni kupanga matumizi ya ardhi kwa vijiji vinavyopakana na eneo hilo kwa ajili ya matumizi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kutoa ushirikiano kwa Serikali na wananchi katika kushughulikia suala hili ili kupata suluhisho la kudumu. Naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, swali la nyongeza.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nashukuru majibu ya Serikali, lakini kwa kuwa, mgogoro huu umekuwa ni wa muda mrefu na umechukua eneo kubwa la Jimbo la Igunga, takribani kilometra za mraba 450. Sasa nilikuwa namuomba Naibu Waziri kwasababu, kumekuwa pia kuna mvutano katika wananchi na Serikali na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya yetu, nilikuwa namuomba Naibu Waziri kama atakuwa tayari baada ya Bunge hili la Bajeti niambatane naye tuende Igunga tukakutane na wananchi na Kamati ya Ulinzi na Usalama tuweze kulimaliza? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu kwa ombi hilo la kwenda wote huko Igunga.

**NAIBU WAZIRI WA UTALII NA MALIASILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaomba tushirikiane Waheshimiwa wote Wabunge ambao tunawakilisha wananchi kutoka katika maeneo yetu husika. Suala muhimu la uhifadhi ni wajibu wa kila mmoja wetu kutambua kwamba, Serikali inapohifadhi maeneo husika ni kwa ajili ya faida ya wananchi wa eneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia jibu langu la msingi ambalo nimelijibu mwanzo, nimeelezea kwamba, eneo hili ni moja ya vyanzo vya maji ambavyo vinategemewa katika Mikoa ya Tabora, Simiyu na Singida.

Kwa hiyo, ninakubaliana na wazo la Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaambatana naye, lakini ni wajibu wa kila Mheshimiwa kuelimisha wananchi wanaomzunguka kwamba, uhifadhi ni wajibu wa kila mtu na faida na hasara za uhifadhi tunaziona, lakini pia tunapohifadhi vyanzo hivi vya maji ni kwa ajili ya wananchi wanaoishi kwenye maeneo husika. Lakini pia tunaepuka mambo mengi ikiwemo kuanzisha majangwa ambayo yanaweza yakasababisha ukame katika nchi yetu. Naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 77

### **Elimu ya Sheria kwa Wanawake Mijini na Vijijini**

**MHE. WANU HAFIDH AMEIR** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha elimu ya Sheria zinazowapa kinga na haki Wanawake inatolewa kwa Wanawake wote Mijini na Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geofrey Mizengo Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, nipende kujibu swali la Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango iliyopo ya kutoa elimu ya sheria si tu kwa wanawake, bali ni pamoja na makundi mengine maalum katika jamii, wakiwemo watoto, watu wenye ulemavu na wazee. Na kuendelea kutoa mafunzo na kusajili watoa huduma ya msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria. Kuanzisha madawati ya huduma ya msaada wa kisheria katika Mahakama, kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatilli zidi ya Wanawake na Watoto. Mkakati huu unalenga kuimarisha na kulinda haki za wanawake na watoto, kuanzisha madawati ya msaada wa kisheria katika Vituo vya Polisi na Magereza, kutafsiri sheria zote kwa lugha ya Kiswahili na kuendelea kutoa mafunzo ya sheria kwa wananchi kupitia mikutano na mihadhara mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2017 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga Sheria ya

Msaada wa Kisheria, Na. 1 ya Mwaka 2017. Madhumuni ya Sheria hii pamoja na mambo mengine ni kuhakikisha msaada wa kisheria, ambao una maana ya utoaji wa elimu na ushauri wa kisheria, uandishi wa nyaraka za kisheria/kimahakama na/ au uwakilishi mahakamani kwa watu wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama za mawakili. Tangu kutungwa kwa sheria hii hadi Machi, 2021, takribani wanawake 3,162,421 kutoka mijini na vijiji wamepatiwa elimu na msaada wa kisheria kupitia madhimisho ya wiki ya sheria, wiki ya msaada wa kisheria ambayo inaadhimishwa kila mwaka katika mikoa yote hapa nchini, vipindi vyta redio na luninga, ziara za viongozi na wataalamu wa Wizara katika magereza na mahabusu za polisi na majukwaa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kutimiza azma ya kuhakikisha kuwa wananchi wanapata haki kwa gharama nafuu na kwa wakati. Aidha nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge kuwashamasisha wananchi kuwatumia watoa huduma wa msaada wa kisheria, wakiwemo wasaidizi wa kisheria, walio katika maeneo yao nchi nzima wanapokabiliana na changamoto mbalimbali za kisheria ili kuifikia haki iliyokusudiwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir, swali la nyongeza.

**MHE. WANU HAFIDH AMEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyotambua kwamba, kuna kazi nzuri ambayo inafanywa na wasaidizi wa kisheria nami natambua kazi nzuri hiyo na ya kizalendo ambayo wamekuwa wakiifanya wasaidizi wa kisheria katika kusaidia wanawake na wananchi kwa ujumla katika *level* ya chini kabisa katika nchi yetu. Swali, Je, Serikali haioni sasa ipo haja ya kuweka utaratibu maalum wa kuwasaidia hawa wasaidizi wa kisheria, ili kuwafikia wananchi wengi zaidi Tanzania, lakini hasa kuwafikia wanawake ambao hasa ndio wanaingia katika matatizo ya kisheria katika nchi yetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geofrey, Mizengo Pinda, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa anachokieleza, lakini Wizara imekuwa na utaratibu mzuri sana wa kutoa mafunzo mbalimbali katika maeneo mbalimbali kwenye haya makundi ya watoa msaada wa kisheria. Tumekuwa tukipita katika kila mkoa kujaribu kutoa hii elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ombi lake kwamba, wanawake wengi washirikishwe kwenye suala hili ni ombi muhimu, lakini nipende tu kuwaarifuni kwamba, kumekuwa na shida moja ya akinamama kushiriki kwenye hili zoezi. Tulitembelea Mwanza akinamama walikuwa wanalamika kwamba, hawaruhusiwi na waume zao kwenda kushiriki kwenye shughuli hii kwasababu, sehemu kubwa sana ya shughuli hii ni kujitolea. Kwa hiyo, kama mtatusaidia Waheshimiwa Wabunge kuwahamasisha akinamama, hii ni kazi huru ambayo mtu yejote anaweza akaifanya kulingana na kuguswa kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nipende tu kusema Wizara haina kizuizi kwa akinamama kushiriki kwenye hili zoezi la utoaji wa huduma za kisheria, lakini sisi wenyewe tuna chuo chetu cha sheria pale Dar-Es-Salaam (*Law School*) inafanya kazi hiyo. Kwa hiyo, wataalamu wengi ambao wanatoa huduma hizi katika maeneo mbalimbali nchini wanapita kwenye hicho chuo, lakini tuna watu wa *Legal Service Facility*; ni taasisi binafsi ambayo nayo imeendelea kutusaidia kuwapa elimu wananchi ambao wamejitolea kutoa msaada wa kisheria katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wizara tumefanya ziara katika maeneo ya Simiyu, Tanga na sasa hivi maafisa wetu wapo Shinyanga na wengine wako Kasulu. Nia ya msingi ni kuwakusanya hawa watoa msaada wa kisheria na kuwapa mbinu mbalimbali za jinsi ya kuwasaidia wananchi wetu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumalizie swalii la mwisho. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwantum Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 78

**Kumaliza Ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa  
Polisi – Kusini Unguja**

**MHE. MWANTUM DAU HAJI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Polisi wa Wilaya Kusini Unguja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Khamis Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, sasa naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Mwantum Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kusini Unguja:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa ofisi ya Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kusini Unguja ulianza mwaka 2008 na gharama ya ujenzi wa mradi ni shilingi 225,000,000/= mpaka kukamilika kwake. Mpaka sasa ujenzi huu uko kwenye hatua ya msingi na unagharamiwa na Serikali kuitia bajeti ya maendeleo, na ujenzi umekwama kwasababu ya kukosekana kwa fedha za kutekeleza mradi wa ujenzi kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuitia Jeshi la Polisi imo katika kufanya jitihada mbalimbali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo wadau wa ulinzi na usalama pamoja na wananchi, ili kuchangia na kukamilisha mradi huo, ili uweze kuwasaidia wananchi na shughuli za ulinzi na usalama ziweze kupatikana katika eneo hilo la Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini Unguja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, swali la nyongeza.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba nimjibu maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, je, katika bajeti ya mwaka huu wa fedha kumetengwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa ofisi hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Je, Mheshimiwa Naibu Spika uko tayari kuambatana ili twende ukajionee katika eneo hilo mwenyewe kwa macho yako hali halisi ya kusaidia kuhamasisha wananchi wako wa Mkoa wa Kusini Unguja, ili na wao wajue kwamba, wewe Naibu wao unafanya kazi vizuri? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Kwa mara ya kwanza nimeombwa kuongozana na Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, majibu. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu langu la msingi, kukwama kwa kituo hiki kulikuwa kunasababishwa na upungufu wa fedha ambaao sasa unatokana na ufinyu wa bajeti. Je, naulizwa, katika bajeti hii tumeingiza hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie kwamba, katika bajeti hii haikingizwa, lakini nimuahidi tu kwamba, katika bajeti ijayo tutajitahidi hii Ofisi ya OCD Wilaya ya Kusini Unguja na ofisi nyingine na maeneo mengine ambayo yana uhitaji wa vituo hivi tutajitahidi tuhakikishe kwamba, tunapeleka au tunaendeleza ujenzi. Hasa ule ujenzi ambaao umekwama wa vituo vyaa polisi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali jingine je, nipo tayari kuambatananaye mama yangu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikwambie. Kwa ridhaa kabisa niko tayari kuambata na Mheshimiwa Mbunge tuende huko tukaangalie hilo eneo. Na itakuwa vizuri kwa sababu, tukifika huko tutawakusanya wananchi...

**MBUNGE FULANI:** Sio wewe.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** ...lakini pia tutakaa na wadau ili kuhakikisha kwamba, tunawashajihisha kujenga kituo hiki, ili wananchi wa maeneo hayo, hasa maeneo ya Makunduchi, Kizimkazi, Mtende, Bwejuu, Paje na Jambiani na maeneo ya karibu waweze kupata huduma za ulinzi na usalama kama wanavyopata wananchi wengine. Nakushukuru.

**MBUNGE FULANI:** Ameombwa Naibu Spika hapo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naona unaninyima fursa ya kwenda Makunduchi, lakini bila shaka nitajialika mwenyewe. Mheshimiwa Ishengoma, swalii la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia swalii la nyongeza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Polisi Kisaki ambacho kiko Morogoro Vijijini kwa umuhimu wake kina matatizo ya usafiri. Je, ni lini kitapewa usafiri angalau pikipiki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nikiri kwamba, bado tuna changamoto ya usafiri hasa katika maeneo ya vituo vy'a polisi, ikiwemo pikipiki na gari na aina nyngine za usafiri. Sasa nimwambie tu Mheshimiwa kwamba, aendelee kuvuta subira, Serikali kama Serikali tumo mbioni kuhakikisha kwamba, vituo vy'a polisi na maeneo mengine ambayo yanatoa huduma za ulinzi na usalama kwa wananchi

tunahakikisha tunapeleka hivyo vyombo vya usafiri, ili sasa wananchi waweze kupata hizo huduma kama inavyotakiwa. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia Shomar swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Suala la Mkoa wa Kusini Uguja ni sawasawa na suala la Mkoa wa Kaskazini Uguja. Je, ofisi iliyokuweko Mkokotoni itamalizika lini? Maana huu mwaka wa tano unakwenda wa sita, bado kumalizika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ofisi ile ipo kwa muda mrefu na ujenzi wake ulikwama hapa katikati, lakini nimhakikishie tu kwamba, Mheshimiwa Mbunge ukarabati na kuendelea kumalizika ujenzi wa jengo lile sasa hivi umo mbioni. Na kama atakuwa ameanza kupita kwa muda huu anaweza akayaona mabadiliko ya ujenzi ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaombe wananchi, hasa wa Mkoa wa Kaskazini Uguja, jambo lao tayari lipo na linatekelezwa na muda si mrefu sana wataanza kutumia kituo kile na wataendelea kupata huduma za ulinzi na usalama katika maeneo yale, hasa ya Mkokotoni, maeneo ya Donge, maeneo ya Mkwajuni na maeneo mengine ya Mkoa wa Kaskazini Uguja. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Eng. Ezra Chiwelesa swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana; na mimi kwa niaba ya wananchi wa Biharamuro ningependa niongezee swali la nyongeza. Wilaya ya Biharamuro ni mionganoni mwa wilaya kongwe kabisa za nchi hii lakini ukiingia katika mazingira ya polisi wa Biharamuro

wanapoishi, bado wanaishi kwenye nyumba zilizojengwa na Mkoloni pale. Lakini mazingira ya kazi ni magumu wote mnajua kumekuwa na majambazi kule lakini vijana wale wanajitahidi kupambana nao usiku na mchana na hali yetu ni shwari kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maswali niliyonayo ni mawili, ni lini tutajengewa kituo kipyga cha Polisi, ikizingatiwa tayari hati iko pale na kiwanja kipo tayari? Lakini pili...

**NAIBU SPIKA:** Moja tu Mheshimiwa moja tu. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa ruhusa yako, nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kukiri tena kwamba bado tuna changamoto hasa kwenye usafiri, makazi na Vituo vya Polisi. Kwa kuwa, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, tayari wana hati ambayo inawamilikisha wao waweze kujengewa eneo zuri waweze kupata jengo zuri ambalo litatoa huduma za ulinzi na usalama kwa wananchi, nimwambie tu kwamba aendelee kustahimili na mimi nalichukua hili tunakwenda kulifanyia kazi ili tuhakikishe kwamba katika eneo lake wanapata kituo kikubwa kizuri na cha kisasa ambacho kitaendelea kutoa huduma kwa wananchi na wananchi wakaendelea ku-*enjoy* hiyo huduma ya ulinzi na usalama katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ravia Idarus Faina swali la nyongeza.

**MHE. RAVIA IDARUS FAINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kumuuliza Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Je, ni lini nyumba za Askari wa Wilaya ya Kusini zitafanyiwa marekebisho kwasababu hali yake ni mbaya

sana? Inafikia hatua kwamba baada ya kupigiliwa misumari hizo nyumba zimewekewa vipande vyatofali na mawe; kwa katika kipindi hiki cha mvua ni hali ngumu sana za wale askari. Je lini nyumba hizo zitafanyiwa marekebisho? (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Ravia Idarus Faina Mbunge wa Jimbo la Makunduchi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sikuwa na uhakika sana kama kuna nyumba zimewekwa mawe badala ya kuwekwa bati; lakini kubwa niseme kwamba hata katika bajeti ambayo tuliyonayo mwaka huu tayari ujenzi wa nyumba hizi umezungumzwa na hatua za ujenzi wa nyumba hizi upo mbioni. Na si nyumba hizi tu tayari tuna mpango wa kujenga kituo kikubwa cha Polisi katika Mkoa wa Kusini na nyumba za kukaa maaskari katika Mkoa wa Kusini. Kikubwa nimwambie Mheshimiwa Mbunge tuendelee kustahimili kidogo. Najua hili linamgusa na linamuumma kwasababu anawaona askari wanavyopata tabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini binafsi nafahamu hili kwasababu huo Mkoa ni wa kwangu. Niseme tu kwamba ninalichukua hili tunakwenda kulifanyia kazi na nyumba za kukaa askari polisi Wilaya ya Kusini hasa Makunduchi zitapatikana Inshallah.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefikia mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu kutoka kwa Serikali. Nilete matangazo;

Kwanza tutaanza na wageni ambaao wapo jukwaa la Mheshimiwa Spika, hawa ni wageni sita wa Mheshimiwa Spika kutoka Kampuni ya *Prime Afro Health care* ya Jijini Dar es Salaam wanaojishughulisha na uingizaji na usambazaji wa kirutubisho kiitwacho *PHYT exponent* ambacho humkinga

mtumiaji dhidi ya virusi vya Korona pia husaidia katika maambukizi ya *HIV* na homa ya ini. Wanaongozwa na Mkurugenzi mkuu Dkt. Edward Masatu, Karibuni sana. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge tunaao pia wageni mbalimbali wa kwenu wabunge. Tunao wageni wa tatu wa Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan ambao ni familia yake kutoka Chakechake Mkoa wa Kusini Pemba wakiongozwa na mke wake Ndugu Maryam Hussein Mohamed pia wapo Watoto wake Ndugu Nadya Ramadhan Suleiman na Ndugu Nadir Ramadhan Suleiman, wamesimama kule juu, ebu, wifi yetu jamani shemeji yetu Maryam Hussein Mohamed haya jamani mmemuona huyo Mheshimiwa Ramadhani Ramadhani ameoa, ana mke. (*Makofii*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Ally Makoa ambao ni Rafiki zake kutoka Kondoa Mkoani Dodoma, ndugu Abdallah Isere na Ndugu abdulazizi Lubuva karibu sana. (*Makofii*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Ally Jumbe ambao ni wadau wa Maendeleo kutoka Kyela Mkoani Mbeya, na hao ni ndugu Alfons Maex na Ndugu Emmanuel M, karibuni sana. (*Makofii*)

Tunaye pia mgeni wa Dkt. Steven Kiruswa ambaye ni mjambe wa Kamati ya Siasa CCM kutoka Longido Mkoani Arusha, na huyu ni ndugu Robert Kaseko, karibu sana.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na matangazo, wageni wetu hawa tuliovatangaza wageni wa Mheshimiwa Spika ambao wanaongozwa na Dkt. Edward Masatu pamoja na kuwatangaza, lakini wapo hapa Bungeni wakifanya maonesho ya hizo bidhaa tulizozisema hapa; na wapo eneo lile la wazi sehemu ile ya Msekwa kule nyuma.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge mpite kule. Hii dawa kama mlivyoolezwa inao uwezo wa kuponya na pia kutoa kinga. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge mwende huko mkasikilize maelezo yao lakini pia muone hicho ambacho wamekileta. (*Makofii*)

Pamoja na yale ambayo nilishayasema dawa hiyo inaimarisha figo, ini au mapafu kama yameharibiwa na maradhi ya aina mbalimbali. Pia huweza kuondoa madhara yanayojitokeza kutokana na *chemotherapy* kama una ndugu ambaye amepata changamoto ya kansa unaweza pia kwenda kuwaona wakakupa maelezo kwa kirefu kabisa kuhusu huduma wanazozitoa.

Waheshimiwa Wabunge lipo pia tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge. Anawatangazia kwamba tumepata nakala ya vitabu vya Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama ifuatavyo:-

*Volume II estimates of Public Expenditure consolidated fund services and supply votes Ministerial, Volume III estimates of Public Expenditure supply votes regional na Volume IV Public Expenditure estimates development votes.*

Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kuwa vitabu hivyo tayari vimeshawekwa kwenye mfumo wa Bunge mtandao kwenye sanduku la vitabu vya mpango na Bajeti. Kwa hiyo ukienda kwenye vitabu vya mpango na bajeti utavikuta vitabu hivi.

Waheshimiwa Wabunge lipo tangazo lingine ambalo linatoka pia kwa Katibu wa Bunge. Mnatangaziwa Waheshimiwa Wabunge kuwa Jumuia ya Umoja wa wanawake Tanzania yaani UWT itakuwa na kikao na Waheshimiwa Wabunge wanawake wa CCM wa majimbo, wa kuteuliwa na Rais na pia wa Viti Maalum siku ya tarehe 15 Aprili, 2021 kuanzia saa 7.30 mchana katika ukumbi wa Msekwa. Lengo la kikao hicho cha pamoja na uongozi wa umoja wa Wanawake Tanzania ni kujadili maendeleo ya wanawake na mstakabali wa nchi yetu. Waheshimiwa Wabunge wanawake mnaombwa kuhudhuria kikao hicho, wabunge wa wanawake wa CCM.

Waheshimiwa lipo tangazo lingine kutoka kwa Makamu Mwenyekiti wa *Bunge Sport Club*, Mheshimiwa

Esther Matiko, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba mazoezi yameanza rasmi uwanja wa Jamhuri *Stadium* kuanzia saa 11.30 asubuhi hadi saa 1.30 asubuhi. Waheshimiwa Wabunge mnaombwa mjiotopeze kwa wingi kwa ajili ya kujenga afya zetu lakini pia kwa ajili ya kujandaa kwa ajili ya mashindano ya hapo baadaye. Huwa kuna safari safari huko hajasema Makamu Mwenyekiti, sasa wakati ya safari kuna watu wanajitokeza kwenye mazoezi alafu inakuwa mtihani.

Lipo pia tangazo la Ibada kutoka kwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya St. Thomas *Moore* iliyopo hapa Bungeni. Mheshimiwa Shally Raymond ambaye ndiye mwenyekiti anawatangazia Waheshimiwa Wabunge, wanajumuiya na wageni wote kuwa, leo kutakuwa na Ibada ya Misa Takatifu ambayo pamoja na nia nyagine za misa, wanajumuya watamuombea Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Ibada itaanza saa 7.00 mchana katika kanisa la Bunge yaani *Bunge chapel* mara tu baada ya kusitisha shughuli za Bunge.

Ninalo pia tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Abdallah Ulega, anawatangazia Wabunge Waislam wote kuwa saa saba mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge, Wabunge wote na Watumishi wote amba ni waislam wanaombwa kwenda kukutana katika ukumbi wa Msekwa ili wakajaribu kuongea huko mambo ambayo yanatuhusu sisi sote lakini wanaoruhusiwa kuhudhuria ni Waislam. Tunaanza mfungo jamani kwa hiyo twende tukawasilize viongozi wetu na mawaidha tuliyonayo.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho maswali kwa Waziri Mkuu siku ya kesho hayatakuwepo kwasababu kwa sasa tunajadili bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa hiyo kwa utamaduni wetu maswali ya Waziri Mkuu huwa hakuna kipindi kama hicho. Nimalizie waheshimiwa Wabunge kanuni zetu zinataka anayekuwa hapa mbele, Mheshimiwa Spika akiwepo hapa mbele au mimi nikiwa nimesimama Wabunge hamruhusiwi kusimama wala kutembea tembea wala kuzungumza, niwakumbushe hilo. Ikiwa umesimama hapa

inabidi msikilize, sasa ukiwa unamwongelesha mwenzio hasikilizi matangazo yanayotolewa. Lakini pia kanuni zetu zinatutaka wote tuwe tumekaa. Ukiona nasimama basi unakaa kidogo unasubiri kidogo matangazo yaish nimalize kuzungumza alafu mambo mengine yanaendelea. Baada ya kusema hayo Waheshimiwa wabunge tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

**NAIBU SPIKA:** Katibu

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA WAZIRI  
MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na majadiliano ambayo yalianza jana na nimeshapata majina hapa ya wachangiaji mbalimbali walioomba fursa ya kuchangia kutoka kwenye vyama vyenye wawakilishi hapa Bungeni. Tutaanza na Mheshimiwa Cosato David Chumi atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya ajiandae.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia katika hotuba ya Waziri Mkuu. Nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Timu ya Simba *Sports Club* kwa ku-*qualify* kuingia robo fainali ya *Club* Bingwa Afrika, lakini pia niwapongeze waliokuja na lile wazo la *visit Tanzania* kwasababu pia inasaidia katika kutangaza utalii. Niwashukuru pia wenzenetu wa Yanga sasa hivi wanatushangilia kwasababu pia wao mwakani, kwa namna moja au nytingine Tanzania itapata nafasi nne, kwa hiyo nao watapata nafasi ya kushiriki. Kwa hiyo nawashukuru sana; lakini pia nawatahadharisha Simba, kwamba hawa hawa wanaotushangilia leo kesho wanaweza wakatuzomea, kwa hiyo tuwe *carefully*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivi, tumeona katika Taifa letu wapo watu ambao; jana Mheshimiwa Kibajaji alisema vizuri sana, Mheshimiwa Msukuma alipendekeza; kwamba ikimpendeza mamlaka Mheshimiwa Lusinde apate *doctorate* ya heshima. Mimi kwa binafsi yangu na kwa mamlaka yangu mimi mwenyewe binafsi tayari Mheshimiwa Kibajaji huwa ninamwita *professor*, nilishampa *professorial* kwasababu zangu binafsi na pia kwasababu katika uwanda wa siasa na ujengaji wa hoja kwakweli vizuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata msiba wa mpendwa wetu Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli nilikuwa naongea na Mheshimiwa Kibajaji, kwamba tuombe sana Mungu; kibajaji akaniambia maana; ye ye huniita mimi tena *professor* sijui kwa nini, kwasabau zake binafsi. Lakini akasema utakuwa unakosea yako ya Mungu halafu yako ambayo sisi lazima tuwajibike kwamba hatuwezi kufanya mambo ya kijinga kijinga alafu tunasema tuombe Mungu, hapana. Yapo ambayo sisi kama binadamu tuna sehemu yetu ya kuyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tulimuona juzi kwenye ziara kule kwenye mradi wa umeme wa Mwalimu Nyerere, lakini pia kumpongeza Mheshimiwa Rais Amini Jeshi Mkuu tulimuona Uganda akishuhudia kutia saini kwa makubaliano yale na kuanza kutekeleza kwa bomba la mafuta. Yote yale ni katika kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi, na kwamba kazi iendelee. Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake amezungumza mambo mengi lakini moja wapo ni jambo la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali langu namba 16 kwenye Bunge liliopita niliuliza kuhusu lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara za lami katika Mji wa Mafinga. Ili kuendeleza sekta nzima ya uchumi wa viwanda ili kupiga hatua na kukuza ajira zaidi ya milioni saba ambazo tumeahidi katika llani yetu ya Chama cha Mapinduzi Ukurasa wa 29

moja wapo ya nyenzo muhimu ni ujenzi wa miundombinu hususan ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninatoka Mafinga, mara zote nimesema, na Mheshimiwa Pacha wangu David Mwakiposa Kihenzile amesema juzi, kwamba bila ujenzi wa miundombinu ya barabara hasa maeneo ambayo yanauzalishaji mkubwa kiuchumi hatua yetu ya kupiga kasi ya uchumi itakuwa ndogo. Kwa hivyo mimi ninapendekeza na kuishauri Serikali, tutakapokuja kujadili suala la *TARURA* tuone namna ambavyo tutaiwezesha *TARURA* ili kusudi tuweze kuweka misingi imara katika ujenzi wa miundombinu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ninapozungumza kuna watu wanasema ukiongeza labda shilingi 50 kwenye lita moja ya mafuta utaongeza gharama za usafiri. Gharama za usafiri hazongezeki kutokana na gharama za mafuta isipokuwa kutokana na barabara mbovu ambazo hazipitiki mwaka mzima. Ikiwa tuna barabara zinapitika mwaka mzima hata gharama za nauli haziwezi kuwa kubwa na wala gharama za usafirishaji haziwezi kuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kutoka Mafinga kwenda Sawala umbali wa kilometra kama 40 nauli kipindi cha mvua inafika mpaka elfu 10,000 - 15,000, lakini umbali huo huo kutoka Dodoma kwenda Iringa ambao ni umbali wa kilometra zaidi ya 260 nauli haizidi elfu 10,000. Kwahiyo gharama za usafirishaji zinaendana sana na hali yetu ya miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kutoka Mafinga kwenda Mtwango kwenda Ifupila baadhi ya magari yamepaki hayawezi kwenda kwasababu mbali ya ubovu wa barabara lakini pia inachangia gharama kubwa za matengenezo ya magari. Kwa hiyo mimi niombe sana, pamoja na kuutazama Mji wa Mafinga tuangalie Barabara ya Mafinga kwenda Mgololo, Barabara ya Mtwango kwenda Nyororo kwasababu inabeba uchumi mkubwa wa Wilaya ya Mfindi Mkoa wa Iringa na nyanda za juu kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema haya si kwamba tunazungumza kama *luxuriously*, hapana, tunasema hivi ili kusudi ku-*bust* kasi ya ukuaji wa uchumi. Leo hii ukienda Barabara ya Mafinga - Mgololo unakuta *semi-trailer* 10 zimepaki kwa muda wa wiki, haziwezi ku-*move*; maana yake ni kwamba tuna *slow speed* ya ukuaji wa uchumi na hata zile ajira milioni nane tulizosisema katika llani hatuwezi kuzi-*realize* kwa wakati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio changu kikubwa mimi leo ni kuhusu barabara. Kama tutaweza kuwekeza nguvu katika ujenzi wa barabara hususan maeneo hayo ambayo yana uchumi mkubwa maana yake tuta-*speedup* ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili napenda kusema, dunia leo hii ndugu zangu inafanya kazi 24/7 saa 24 siku saba. Jana nilikuwa na swali lini Serikali itaruhusu baadhi ya miji hasa ambayo iko kando ya barabara kuu kama vile Mlandizi, Chalinze, Morogoro, Mikumi, Ruaha Mbuyuni, Ilula, Ifunda, Mafinga, Makambako watu hawa wajachie wafanye biashara saa 24, ajira ziko rasmi za Serikali lakini ziko za vijana kujajiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi Mafinga pale inapofika saa nne Polisi wanapofika na kutaka vijana wafunge biashara wakati vijana hawa mchana kutwa walikuwa msituni wakiitafuta shilingi, tutakuza vipi uchumi? Kwa hiyo, nashawishi Bunge hili na Serikali tuangalie baadhi ya maeneo ya miji kama hiyo niliyoitaja na mingine miji kama Korogwe na Mombo kwa shemeji zangu, watu wajachie wafanye biashara. Duniani kote kazi ya dola ni ulinzi na usalama, wao wa-*guarantee* vijana wajachie wafanye biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini masuala ya saa tano kuanza kukimbizana na vijana wafunge biashara zao ambao mchana kubwa walikuwa wanatafuta kipato chao, mimi kwangu naona siyo sahihi na hili kwa kweli siwezi kukubaliana nalo. Ndiyo maana nikasema kwa mujibu wa utaratibu wa

Serikali ziletwe hapa sheria tuweze kuwezesha maana kazi ya Serikali ni ku-*facilitate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake amezungumzia kuhusu sekta ya michezo na amesema *contribution* ya sekta ya michezo kwenye pato la Taifa ni 3% tu kati ya 2013 mpaka 2019. Pia ameeleza kwamba sekta hii inaa jiri vijana wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mambo mawili; kwanza ili tunufaikie na *Media Entertainment and Sports Industry* kama siku zote ambavyo huwa nasema hatuna namna lazima tukiangalie kwa macho mawili Chuo cha Michezo cha Mallya na Taasisi ya Sanaa ya Bagamoyo - TaSUBa, ili kusudi tuweze kuwezesha vijana na nyenzo mbalimbali za masuala haya ya michezo, burudani na utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili lazima tuangalie pia viwanja. Sasa hivi unakuta kwamba kiwanja kama cha Jamhuri kama tuna tamasha labda la Fiesta sijui Mziki Mnene la Wasafi au Mtikisiko unakuta matamasha haya yanafanyika katika viwanja vya mpira. Ni ushauri wangu kwa Serikali tujenge uwanja wa *Standard Olympic* ambao utakuwa kama *One Stop Center*; viwanja vya kuogelea, *table tennis* na kila aina ya michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia lazima tufike wakati tuhamasishe wawekezaji wawekeze katika majumba makubwa na viwanja maalum ambavyo ni kwa ajili ya masuala ya burudani. Kwa sababu *as it is* leo utakuta uwanja pale wa Taifa kuna tamasha iwe la muziki wa injili, iwe la muziki wa kimataifa yote yanafanyikia pale. Kwa hiyo, ama kupitia wawekezaji ama namna yoyote ambayo Serikali itaona inafaa kama tunataka tunufaikie na sekta ya michezo na burudani lazima tuangalie Chuo cha Michezo cha Mallya na Taasisi ya Sanaa ya Bagamoyo lakini lazima tuwekeze katika miundombinu wezeshi ya kuwezesha vijana hawa kuwa na maeneo ya kufanya hizi kazi zao. Michezo sanaa na burudani inaa jiri vijana katika ajira isiyo rasmi siyo chini ya

milioni 2 na huu ukuaji wa teknolojia ya sayansi na teknolojia kwa maana ya matumizi ya *internet*, inaleta sana ukuaji wa uchumi katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja nikisisitiza tufanye kazi saa 24 siku saba, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Azan Zungu atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya na Mheshimiwa Cecil David Mwambe ajiandae.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Waheshimiwa Wabunge wenzangu tumeondokewa na Rais mpendwa Mungu amuweke pema, mwanamme mashine. Tumempata mwanamke mashine Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumpe nguvu, tumuombee dua atimize majukumu yake. Mheshimiwa Rais Samia ameshaanza kuonesha mwanga kufuata nyayo za Mheshimiwa Magufuli, tumsaidie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Afrika lazima iamke kwenye *natural resources* ambazo Mungu ametupa katika Bara hili la Afrika. Ripoti ya Umoja wa Mataifa inasema *the enclave nature of mining industry can limit the trickle down of benefit unless sovereign government participate fully in managing extract industries*, kitu ambacho mara nyingi nchi za Afrika na sisi vilevile bado hatujafikia kiwango kizuri cha ku-manage migodi yetu na *natural resources* ambazo tunazo. Pamoja na marekebisho ya sheria tuliyofanya ambayo tunapata 16% lakini bado tuna haki ya kumiliki migodi hii kwa 100%, kwa kufanya sisi wenye kazi ya ku-extract industries za migodi nchini mwetu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya kuchunguza madini ya almasi na tumeona wawekezaji wa madini haya hawana ujanja mwingine wowote zaidi ya kutumia madini haya kama dhamana. Serikali yetu inaweza na wao tukatumia madini yetu haya yaye dhamana ya kupatia mtaji na hawa wataalamu

tukawakodisha na tukawaajiri na wakawa wafanyakazi wa Serikali. Ni hatari kubwa sana kuacha mali hizi zinaondoka wakati sisi Tanzania hatupati *market value* ya *extract industry* ya *mining* katika nchi yetu. Tunapata pesa kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo dhahabu ni zaidi ya Dola 2,000 tujiulize katika hiso Tanzania tunapata ngapi? Tunachokipata ni kidogo sana, lazima tubadilike na sasa *turn* sisi wenyewe migodi hii. Najua kuna *cartel* kubwa sana ya *multinational companies* kutotaka nchi za kiafrika kuendeleza migodi yao wenyewe. Wanataka lazima waje wao wadanganye kwenye masuala ya mengi sana hasa kwenye *operation cost*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Serikali, najua kuna vitengo katika idara zote ambazo zinaangalia *operation cost* waongeze umakini na ujuzi. Katika Mgodi wa Mwadui tuligundua mtambo unaandikwa dola milioni 8 kumbe mtambo umenunuliwa kwa shilingi milioni 5 Tanzania hapa hapa. Kwa hiyo, vitu kama hivi vinaongeza *operation cost* kuwa kubwa na kufanya faida ya Serikali kupungua, lazima tuamke. Pia lazima tuwe na sehemu ya *National Revenue Management Schemes such as Stabilizing Funds inflected cost of projects. (Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuhakikishe mali ya Tanzania na Afrika kwa ujumla inalindwa na inaendeshwa na Watanzania wenyewe. Siri kubwa ni kuweka dhamana migodi tufanye wenyewe, tusiwape wawekezaji, wao waje na teknolojia tuikodishe, tuwalipe mishahara wabaki kama wafanyakazi wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye ATC inajitahidi kutoa huduma na kufanya kazi vizuri. ATC haiwezi kupata faida au kujidoresha kwa ununuzi wa *ticket*. ATC kama ni *national carrier* lazima Serikali iwapunguzie baadhi ya *operating cost. (Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndege ya Shirika la Ethiopia hailipi *landing fee, parking fee, navigation fee*, hailipi

gharama nyingi sana wanapunguziwa au kufutiwa ili kuwasaidia wakue. Sasa ATC ina gharamia gharama zote hizi, inafanya kupunguza mapato yao. ATC hii mpya chini ya Mheshimiwa Matindi, 100% mishahara ilikuwa inalipwa na Serikali leo Serikali inatao *only 17%*, inaonesha wanaanza kuja na wakianza kusaidiwa watakuwa vizuri sana. (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndege hazitakiwi kukaa chini ya ardhi, anayepumzika ni rubani na *crew*, ndege inaruka *twenty-four seven*. Sasa kama hatuna viwanja vyenye ubora wa ndege kuruka usiku, Serikali lazima iwekeze. (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Dodoma zimebekwa taa *intensity* yake haiwi-*controlled* na *Control Tower* ambapo siyo jambo la kawaida. Hii inaweza ikaleta madhara wakati wa giza nene taa zisiweze kuwaka vizuri kama *Control Tower* hawawezi ku-*control intensity* ya taa zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba tuboreshe viwanja vyetu, hapa Dodoma waweke *Vertical Approach Slope Indicators (VASI)* na ILS ambayo inasaidia hata kwenye mawingu ndege zinatua. Mara nyingi tu ndege za ATC zinarudi sababu zinashindwa kutua. *ILS* ni chombo ambacho kinaleta usalama kwa abiria, kwenye kiwanja na kwenye ndege. Uwanja wetu huu sasa hivi unapitiwa na watu wengi sana lazima tuboreshe viwanja vyetu kuwe na usalama wa hili shirika letu. (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu mradi wa *DMDP*, Mkoa wa Dar es Salaam. Naomba Serikali iendelee kufanya maamuzi, Dar es Salaam 2025 itakuwa na *population* ya watu milioni 10. Deni lolote ambalo Serikali imelikopa kwa niaba ya Mkoa wa Dar es Salaam linalipika kwa michango na uchumi amba Dar es Salaam wanao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine huu ni mwezi wa Ramadhan tende jamani siyo chakula cha Waislamu, tende ni chakula alikula Yesu Kristo na katika vyakula alivyopenda Yesu Kristo ilikuwa tende na mkate wa mana. Ukisoma

Wagalatia 5:22-23, chakula cha kwanza ambacho kina *spirit* tende imetajwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi sababu Waislamu wako katika mfungo na tende hizi ni sadaka, Serikali ifikirie kutoa ushuru wa tende ili wananchi wa dini zote wawewe kula tende. Wakristo wale tende sababu Yesu kala, Waislamu wale tende sababu Mtume Muhammad naye amekula. Kwa sisi Waislamu ni suna na kwa Wakristo ni suna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkisema Waziri haruhusiwi kubadilisha sheria tumeanzisha mtindo wa *force account*. *Force account* ni uwekezaji au utendaji wa kazi unaofanywa bila kulipa VAT. Kwa hiyo, tende nazo vilevile Waziri aseme tu tunaruhusu, itoke *executive order* tende ziruhusiwe bila ushuru tupate kula tende, tupate kufuata suna za Mitume wetu waliopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na tende hizo ukitizama wana wa Israel walivyotoka kwa farao walivyoingia jangwani ukisoma Exodus 15:27 chakula chao cha kwanza ni tende.

Kwa hiyo, naomba Serikali ili nchi iendelee kuwa na neema ruhusuni tende bila ushuru ili Waislamu na Wakristo tule tuweze kupata neema za Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye suala la wafanyabiashara, Serikali mmekaa sana na wafanyabiashara...

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga, ahsante sana.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Amos Bulaya atachangia kwa dakika 7, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mheshimiwa Maimuna Mtanda ajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami niwatakie Waislamu wote mfungo mwema wa Ramadhani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikizungumzia sana suala la Serikali kuhakikisha inalipa madeni kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Leo nasisitiza Serikali mlipe madeni kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, hizi pesa siyo zenu nyinyi mnatunza tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilikuwa najaribu kupitia ripotimbalimbali, ripoti ya BoTmeonyesha 26% ya deni la ndani la Serikali wanakopa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Ukienda kwenye ripoti ya *CAG latest* imeonyesha Serikali inadaiwa trilioni 2.7 bado haijalipa. Hapo sijazungumzia yale madeni ya kurithi ya kabla ya ile Sheria ya mwaka 1999 Serikali kuamuru madeni yalipwe wakati hakukuwa na michango. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini hata mnapokopa kopeni kulingana na taratibu zilizowekwa na mifuko. Nitolee tu mfano Mfuko wa Bima ya Afya, Serikali ilikopa shilingi bilioni 220 kwenye sekta mbalimbali ikiwepo Wizara ya Mambo ya Ndani, 60% ya huo mkopo ambayo ni shilingi bilioni 132 walikopa hakuna makubaliano yoyote ya kimaandishi wala hakuna riba. Sheria Na. 5, kifungu kidogo cha (1)(f) cha Sera ya Uwekezaji wa Mifuko ya mwaka 2020 imeeleza bayana kwamba Serikali ikikopa ikope kibiasara na ilipe riba. Msipolipa riba mnachangia mifuko kukosa mapato, hilo hamfanyi. Hii ni kinyume kabisa na lengo kuu la mifuko kwa mujibu wa kifungu cha 33 cha Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2015. Kopeni, lipeni na fuateni taratibu. Hii ilishajitokeza hata kwenye mkopo wa *UDOM* kipindi hicho, mmechukua pesa kule hamkuingia mkataba, mkataba mkaingia baadaye, tuache! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala ambalo ni muhimu sana kwa wafanyakazi. Tumelahirisha, liliwekwa kiporo baada ya sintofahamu iliyotokea mwaka 2018, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli akaingilia katika akasitisha kunyonya wafanyakazi kwa kikokotoo kibovu ambacho tulizungumza kwenye Bunge hili. Nimeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 60 ameligusia kidogo lakini hawajasema bayana ni lini suala hili mtalitatua kisheria kwa kuleta mabadiliko Bungeni ili yale wanayoyataka wafanyakazi; kikokotoo chao kilichobeba hatma ya maisha yao baada ya kutumikia Taifa hili kwa jasho na damu kiwe cha neema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliwaambia mwanzo kikokotoo hiki mkiweke kwenye sheria kisiwe kwenye Kanuni ya Waziri hawakutusikia na hawakushirikisha wadau matokeo yake wakaleta kikokotoo kibovu cha 1/580 kuliko hata kile kilichokuwa mwanzo cha 1/540. Tulitegemea kingekuwa chini ya 1/540 basi hata ingekuwa ya 1/520 kama walivyokuwa wamependekeza awali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mstaafu anastaafu unamwambia ile *full pension* unampa 25%, asilimia 75% utamlipa kidogo kidogo, haiwezekani kumpangia mtu pesa zake. Yeye mwalimu anayelipwa *pension* yake labda milioni 40 umlipe 25%, 25% ya milioni 40 akajenge, anasomesha huyo huyo mwalimu, bado hajaweka sawa mazingira mmeyaweka mabovu. Haiwezekani kwa nini tuwapangie mbona nchi za wenzetu wanachukua 50% wengine 75%, 25% siyo sawa kwa wafanyakazi wa Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia michango haipelekwi, sasa hivi wastaafu wengi hawalipwi. Ukienda huko Mbeya utasikia kilio hicho hicho, Bunda na maeneo mengi hawa Wabunge wanajua wastaafu hawalipwi na hawalipwi kwa sababu michango maeneo mengi haipelekwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano tu *NSSF* michango ya wanachama ya shilingi bilioni 284 mwaka

mzima hajakusanya. Ukienda pale Bima bilioni 24, ukienda Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi milioni 116 ziko nje wastaifu watalipwaje? Serikali hailipi madeni na michango haikusanywi, siyo sawa! Hizi pesa siyo zetu ni za watumishi wa nchi hii, tuwape *morale*, tuwarudishie kikokotoo chao, tukusanye michango yao ili wastaifu wetu wawe na uhakika wa kulipwa kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Iakini pia miaka mitano hawa watumishi sisi tunapanga mambo hapa wanaenda kuyatekeleza kwa kinyongo, *five years* hatujawapandishia mishahara. Wana *stress* ya kupandishiwa mishahara, wana *stress* ya kikokotoo kibovu, wana *stress* ya pesa Serikali wanachukua kwenye mifuko yao hawalipwi, wana *stress* wenzao wanaostaifu hawalipwi kwa wakati, wao waliokuwa kwenye utumishi hawajui hatma yao itakuwaje, siyo sawa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala hili Mheshimiwa Hayati Rais JPM alisema, hivi sisi Wabunge tukimaliza tunapewa kitita chetu, hawa ambao tunatunga mambo yetu humu ndani wanaenda kuyatekeleza unawapangia 25%. Tutekeleze kazi hii kwa uadilifu, Mungu atulipe tuache *legacy* ya kuwatetea wafanyakazi wa Taifa hili ambao wanashinda usiku na mchana kutekeleza hiyo miradi mnayojivunia leo kwamba imetekelezwa, siyo ninyi ni hawa ambao mazingira yao ya kazi, hatma ya kiunua mgongo chao ni mabovu, tutimize wajibu wetu. Tulinde Taifa letu kwa kuhakikisha haki za wafanyakazi zinakuwa nzuri. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecil David Mwambe atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Mtanda na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa namna ya pekee kwa kunipa nafasi ya kuchangia leo ambayo ni siku ya pili ya mjadala wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nianze kwa kutoa shukrani kwako wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waheshimiwa Wabunge wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mtwara wakiongozwa na Mheshimiwa Chikota, viongozi wa chama na Serikali wa Mkoa wa Mtwara, mikoa ya jirani na majimbo Jirani, wananchi wote wa Jimbo la Ndanda na majimbo jirani, kwa namna ya pekee walivyoshiriki kwenye msiba wa mke wangu mpendwa Beatrice na walivyotupa faraja. Ahsanteni sana, nawashukuru. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimerudi hapa kuendelea kufanya kazi zangu nilizotumwa na wananchi wa Jimbo la Ndanda na nimesimama ili nami niweze kuchangia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikiliza vizuri sana Hotuba ya Waziri Mkuu, nami nimeamua kuchagua maeneo manne au matano hivi ambayo ningependa nichangie kwa sababu ndiyo yanagusa Watanzania na wakazi wa Ndanda. Sehemu ya kwanza kabisa ni suala la kilimo; nitatumia hapo muda mrefu kwa sababu nataka kuona wananchi wale, wakazi wa Ndanda na Watanzania ambao ni zaidi ya asilimia 75 wanapata manufaa kutokana na kazi za mikono yao na kazi zao za shambani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameongea suala la umeme, nami nitachangia hapa pia masuala ya afya na masuala ya barabara na mwishoni mambo mengine ya mtambuka kwa ujumla. Kwenye suala la kilimo, nimefanya mazungumzo kwa kina na Naibu Waziri, Mheshimiwa Bashe na kujaribu kumweleza mambo yanayotusibu sisi wakulima na hasa wakulima wa Korosho kwenye sekta hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwakumbushe tu Wabunge wenzangu wote kwa ujumla kwamba, mtakumbuka katika mazao makubwa matato yanayotajwa kimkakati ni pamoja na korosho, lakini kwa masikitiko makubwa sana, mwaka 2020 uzalishaji wa Korosho ulipungua msimu uliopita kutoka msimu

ule wa mwanzo. Mwaka 2020 tulipata tani 205 tu, wakati msimu uliofuatia nyuma ulikuwa ni tani 330. Hii imetokana na kutokutimiza wajibu wetu sawa sawa kwenye kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo naiomba Serikali ifanye sasa; na tumesikia hapa na kupata majibu kwamba kuna mkakati mzuri kabisa ambapo Serikali inakwenda kununua pembejeo kwa pamoja na kuzigawa kwa wakulima ili ziweze kuwafikia kwa wakati na vile vile tunaamini zitakuwa na ubora unaotegemewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana na nimsisitize sana Mheshimiwa Hussein Bashe, kama mpango huu umepangwa na Serikali, basi utimizwe kama vile ambavyo mmekusudia ili kuweza kuongeza uzalishaji wa korosho. Inasikitisha kuona wafanyabiashara wanajinufaisha sana inapofika misimu ya wakulima kuweza kupata pembejeo pamoja na virutubisho vingine ambavyo vinatumika kwenye mikorosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimu uliopita na misimu mingine huko nyuma tumeshuhudia *sulphur* ikiuzwa mpaka kati ya shilingi 35,000/= mpaka shilingi 50,000/= kwenye maeneo mbalimbali, jambo ambalo ni bayaa sana kiasi kwamba wakulima walikuwa wanashindwa kununua na kuhudumia mikorosho yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumefurahi kuona nia njema ya Serikali hii ya Awamu ya Tano na Awamu ya Sita kwamba ambapo wanatuahidi kwamba bei za *sulphur* sasa itapungua mpaka kufikia shilingi 29,000/=, tena zitatolewa kwa wakulima kwa njia ya mkopo ambayo baadaye mnunuzi atachangia kiasi na mkulima naye atakatwa baada ya kuuza korosho zake. Hii itawasaidia sana kwa sababu tutajiondoa kwenye ile mikopo mikubwa iliyoko kwenye mabenki ambayo ilikuwa na tozo kwa riba kubwa kiasi kwamba wakulima walikuwa hawanufaiki na hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba pia Wizara ya Kilimo waboreshe na mifumo ya ununuzi wa Korosho, wasimamie vizuri sana masuala ya ushirika kwa sababu ndiyo yanayoumiza wakulima kila mara. Pia tuboreshe na ule mnyororo mzima wa zao la Korosho, tusiishie tu kununua Korosho; na kila mara nimekuwa nalisema hili jambo ndani ya Bunge hapa, japokuwa wengine hawataki kulielewa sana, kwamba unapovuna Korosho magunia 100 unapata pia na Kochoko au mabaki ya korosho, yale mabibo; na yenewe unaweza kupata takribani gunia 75 mpaka gunia 100, zinakaribiana. Hizi kule kwetu kila mara nimesema, tunazitumia kupika gongo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie Waheshimiwa Wabunge, ninachokiomba sasa, Serikali warasimishe na kurekebisha haya mambo, kwa sababu hatuwezi kuyakwepa. Tumeishi namna hiyo, sasa isiwe tena tunasema ni pombe haramu kabla hatujawaeleza ili iweze kuwa halali, nini kifanyike? Nia nzuri ya Wizara iwe ni kuona wakulima wananaufaika na mazao yao ya shambani kama wanavyonufaika wakulima wa mazao mengine kwenye maeneo mengine; wakulima wa Kahawa, wakulima wa Miwa na wenyewe wote wananaufaika na wanapata mazao makubwa na faida kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la umeme. Nimemsikia hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu anasema, mpaka sasa kuna vijiji takribani 1974 na ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri naye tulikuwa tukiongea mara nyingi kwamba kwenye Jimbo Ndanda mpaka sasa kuna vijiji 29 ambavyo havina umeme kabisa na hasa zaidi kuna Kata mbili ambazo na zenyewe hazina umeme kabisa; Kata ya Msikisi pamoja na Kata ya Mpanyani. Naomba mfanye kwa haraka sana kuhakikisha vijiji hivi vinapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri; na haya mambo yapo kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kama ambavyo kila mara nimesema, nimefurahi sasa kusimama hapa nikiitetea Ilani ya Chama cha Mapinduzi, achilia mbali sera zetu na mambo mengine,

lakini nataka nione ilani hii inatekelezwa na sisi tusimame kwa kifua mbele kwamba ilani yetu imetekelezwa katika eneo letu na watu wa Ndanda nao wajivunie kwamba wamepata sasa msimamizi kwa ilani inayotekelze na Serikali hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye masuala ya afya, nawaomba sana Waziri wa afya na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba tuhakikishe sasa Hospitali ile ya Kanda ya Mtwara inamaliziwa ili wananchi wale waweze kupata huduma. Sasa hivi tunatumia Hospitali ya Ndanda ambayo watu wengi wanailalamikia kwamba ina gharama kubwa sana kwenye kutoa huduma. Nami nataka niwaambie, ukubwa wa gharama huu ni kwa sababu ya uhaba wa Vituo vya Afya vilivyopo kwenye maeneo haya. Kwa mfano, wakazi wa Ndanda walijitahidi sana kujenga boma lao kwa ajili ya Kituo cha Afya, limekamilika mpaka kufika *level* ya lenta katika Kata ya Mpanyani, Kata ya Mihima na Kata ya Namajani na kwenye maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba badala ya kuwafanya watu wa Ndanda wakatibiwe kwa gharama kubwa kwenye Hospitali ya Mtakatifu *Benedict* ya pale *Ndanda Mission*, basi sasa tukamilishe kujenga kile Kituo cha Afya kilichopo pale ili gharama ziweze kupungua na pia tuwapunguzie adha ya kusafiri safari ndefu ya kwenda Jimbo la Ruangwa huko kwenye Kijiji cha Nandanga kwenda kupata matibabu jambo ambalo siyo zuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nisisitize pamoja na lille suala la korosho ni suala la barabara. Kwa kipindi kirefu sana tumekuwa na tatizo kubwa sana la barabara. Kuna hii barabara ambayo sijasikia kila mara inatajwa, lakini ni *introduction* ya barabara inaitwa *Cashewnut Ring Road*. Barabara hii inaanzia Nangurukuru – Liwale – Ruagwa – Nachingwea – Masasi – Newala – Nanyamba - Mtwara yenye wastani wa kilometra kama 400. Naomba sana, ili bandari yetu iweze kutumika vizuri, basi tuhakikishe hii barabara tunaikamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipatia na ninawashukuru sana vijana wa Bunge wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maimuna Mtanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Rashidi Kawawa na Mheshimiwa Miraji Mtaturu, ajiandae.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri pamoja na wale wote waliosaidia kuandaa hotuba ile. Nimeipitia hotuba yake, lakini naomba nami nichangie baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la watumishi, ambao ni walimu. Nilipata kusikia kuhusu ajira mpya za walimu kwamba sasa hivi Wizara imeweka mpango kwamba anayeomba ajira ya walimu anataja sehemu ambako anatakiwa kwenda kufanya kazi. Yaani kwenye *application*, katika maombi yake anaandika, mimi nataka kwenda sehemu fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo ni zuri, lakini linaweza kuwa na changamoto kwa upande mwingine kwamba kuna maeneo hali yetu, maeneo yetu tunayafahamu, kuna maeneo miundombinu ni hafifu kiasi kwamba hayatapata watu wa kuomba moja kwa moja. Katika mazingira hayo kuna maeneo yatanufaika, yatapata watu wengi na kuna maeneo yatakosa kabisa watu wa kuomba kutokana na hali ya kijografia. Kwa hiyo, naomba tuangalie upya, wazo ni zuri kwamba litapunguza ile hali ya mtu akishapangiwa eneo, anakwenda kuomba abadilishwe, lakini italeta athari kwa upande mwingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala la uhaba wa walimu katika maeneo yetu. Sasa hivi nchi yetu iko kwenye uchumi wa kat, lakini tunataka tutoke hapo.

Katika hali hiyo ni lazima kujimarisha kuwekeza katika elimu ili hivyo ambavyo tunavitarajia viweze kwenda vizuri. Kuna uhaba mkubwa sana wa walimu katika shule zetu hasa za msingi pamoja na sekondari. Maeneo mengi ambayo yameadhirika ni yale ambayo yapo *remote* sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ukija kwenye Jimbo la Newala Vijiji, kutokana na umbali kati ya kijiji na Kijiji; na sera yetu ni kwamba kila kijiji kiwe na Shule ya Msingi, unakuta jumla ya wanafunzi katika Shule ya Msingi kwenye shule fulani iliyopo katika kijiji fulani haizidi 100. Hesabu zinazopangwa kwa *ratio* ya mwalimu na mwanafunzi ni mwalimu mmoja na wanafunzi 45. Kwa hiyo, unakuta shule hiyo; mathalani shule yenye wanafunzi 80 au 90 inakuwa na walimu wawili tu, lakini ina madarasa kuanzia awali mpaka la Darasa la Saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, walimu hao wana mzigo mkubwa sana. Kwa hiyo, naomba tuangalie, sawa *ratio* ni hiyo, lakini naiomba Wizara na kuishauri iangalie upya maeneo yale ambayo yako mbali lakini yana uchache wa wanafunzi ili angalau walimu waweze kuongezwa kwenye maeneo hayo na watoto wapate stahiki yake ili Tanzania ya viwanda iweze kuendelea vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naiu Spika, ukienda kwenye afya, kuna uchache pia wa watumishi katika maeneo hayo. Unaenda kwenye *Dispensary* unakuta mtumishi ni mmoja, anahudumia watu wote; wajawazito awapime yeye, wagonjwa wa Malaria awatibu yeye, kila kitu ni yeye.

Mheshimiwa Naiu Spika, kama binadamu anachoka, wakati anapochoka, anakuja mgonjwa ambaye anatakiwa apatiwe huduma ya haraka, naye ana mlundikano mkubwa wa wagonjwa, anashindwa. Anaposhindwa, mgonjwa analalamika kwamba sijapata huduma ipasavyo; lakini siyo kwamba kwa matakwa ya yule ambaye yuko pale anatoa huduma, ni kwa sababu ya uchache wa watoa huduma katika eneo lile, wagonjwa hawapati matibabu stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Wizara iangalie eneo hili ili wananchi wapate huduma ipasavyo. Ukienda kwenye Jimbo la Newala Vijijiini hali ya Watumishi wa Huduma za Afya ni mbaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni ukosefu wa bei za uhakika kwenye mazao mchanganyiko hasa Mbaazi, Njungu pamoja na Mihogo. Wananchi wanajitahidi sana kulima, lakini mazao hayo hayapati bei. Matokeo yake kule kwangu Newala vijijiini wanaamua kuhama makazi yao, wanaenda mikoa ya jirani kulima ufuta angalau ambaao una nafuu ya bei. Matokeo yake, maendeleo ya Newala Vijijiini yanazidi kuzorota; na kwa sababu wazazi wamehama, wanaondoka na watoto wao na kwa hiyo, kunakuwa na utoro mkubwa wa wanafunzi na mimba zisizotarajiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Wizara ya Kilimo iangalie suala la bei ya mazao mchanganyiko kwa jicho la kipekee ili wananchi watulie kwenye maeneo yao waweze kufanya shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na suala la *TARURA* ambalo jirani yangu Mheshimiwa Cecil ameliongea. Hali ya barabara zinazohudumiwa na *TARURA* kule kwetu siyo nzuri sana. Hatuwalaamu wao, lakini tatizo ni fedha chache ambazo zipo katika mfuko huo. Barabara nyingi hazipitiki. Wakulima ambaao wanazalisha mazao yao pemberi au walioko pemberi mipakani mwa Newala na Wilaya jirani wakati mwengine wanashindwa kusafirisha hasa zao la Korosho kutoka kule wanakolima kuleta kwenye maeneo yao ili wauzie kwenye vyama vyaa msingi ambavyo viko kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake Jimbo la Newala Vijijiini kwa sababu ya ukosefu wa miundombinu ya barabara nzuri, linajikuta linapoteza mapato kwa sababu wanazimika kwenda kuuza mazao yao kwenye wilaya na vijiji vyaa jirani hatimaye tunakosa mapato. Hasa ukienda Kata ya Mikumbi; barabara ya Mikumbi - Mpanyani haipitiki,

barabara Namdimba - Chiwata haipitiki, barabara Mkoma - Chikalule haipitiki na barabara nyinginezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana suala la *TARURA* lionezewe mapato ili barabara ziboreshwne na Jimbo la Newala vijijini liweze kupata kile ambacho kinatarajiwa kutokana na mazoa yanayolimwa na wananchi wa jimbo hilo. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Mtaturu na Mheshimiwa January Jusuf Makamba, ajiandae.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru nami kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwasilisha vyema hotuba yake ilio-coverna kusheheni maeneo yote kwa ujumla na ufasaha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa majukumu ya Kikatiba ya Ofisi ya Waziri Mkuu ni kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali, lakini pia kusimamia shughuli za Serikali Bungeni. Kazi hiyo imefanyika vizuri sana katika kipindi kilichopita; wameisimamia Serikali katika miradi ya kimkakati vizuri na mafanikio ya miradi yote tunayoiona ni kwa sababu ya kazi nzuri iliyofanywa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nzuri iliyokuwa inafanyika Bungeni humu ni kazi ambayo imefanywa chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu chini ya Waziri Mheshimiwa

Dada Jenista Mhagama. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa kazi nzuri walioifanya. Kubwa ni ile kazi iliyotukuka na ikatufanya tukakaa kwa amani kabisa wakati wa kipindi cha msiba kwa aliyekuwa Rais wetu. Walifanya kazi ya uratibu mzuri wa maziko ya Rais wetu aliyetutoka na tukafanya kazi ile ya maziko kwa mafanikio makubwa sana na dunia imetupa heshima kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze katika kutoa ushauri wangu. Kazi kubwa ya miradi ya kimkakati imefanyika, sasa naiomba Serikali ijielekeze sana sasa hivi katika kuweka mazingira bora ya uwekezaji wa sekta binafsi katika miundombinu inayojengwa au iliyokamilika. Kwa mfano, sekta mtambuka ziangalie ni jinsi gani zitaweza kutumia fursa ya *SGR* ambayo inajengwa, inaenda kukamilika sasa hivi.

Je, kwa mfano Wizara ya Ardhi na Wizara ya Viwanda na Biashara zimepitia na kutambua ardhi na kuweka mkakati wa viwanda katika maeneo ambayo itapita *SGR* ili tuweze kuvutia wawekezaji kwenda kuwekeza katika maeneo hayo tuweze kuitumia *SGR effectively?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili pia Wizara ya Kilimo inaweka mpango gani kushawishi wawekezaji au wakulima wakubwa wakatambue maeneo inakopita *SGR* wakaweka kilimo kikubwa pale ili tuweze kutumia reli ile ya kati? Pia Wizara ya Maliasili nayo ina mpango gani wa kushawishi kuweka mashamba makubwa ya miti katika maeneo inapopita *SGR*? Hapa nina maana fedha nyingi zimewekezwa katika ujenzi wa reli hii, lakini inapopita reli kwa eneo kubwa ni kwenye mapori ambayo yalikuwa hayatumiki. Sasa ni fursa kwa sisi kama Serikali kushawishi sekta binafsi kuwekeza katika maeneo hayo ya kilimo, ya viwanda vitakavyo *support* kilimo, lakini pia kuwekeza katika mazao ya misitu ya mbao ambayo yana soko kubwa katika nchi zetu zinazotuzunguka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze jimboni. Naishukuru sana Serikali Waziri Mkuu ameelleza mafanikio yaliyofanyika katika kipindi hiki cha nyuma. Sisi wa Namtumbo

tunawashukuru sana, Serikali imewekeza karibu billioi 27 katika usambazaji wa umeme, katika kuunganisha umeme wa *grid* katika Wilaya yetu na maeneo makubwa katika vijiji vyetu vimewekwa umeme na vingine vilivyobakia changamoto iliyopo ni katika vitongoji, lakini baadhi ya maeneo katika kuunganishwa umeme. Kwa hiyo tunaomba sana katika eneo hili mafanikio makubwa tumefanikiwa. Katika Sekta ya Afya Serikali ilituingizia bilioni moja na milioni mia nane na imetujengea hospitali ya wilaya. Haya ni mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengine, Serikali imetujengea Chuo cha Elimu cha VETA kilichogharimu bilioni sita na milioni mia tano na chuo sasa kinatumika. Tunachoiomba Serikali sasa iwekeze kwenye rasilimali watu katika maeneo haya ya elimu na afya ili waweze kuja kwa kutosha waweze kutoa huduma iliyokusudiwa kwa sababu tumeweka fedha nydingi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika maeneo ya kilimo sisi ni wakulima wakubwa sana wa mazao ya mahindi na tunategemea sana pembejeo, lakini katika wakati pembejeo za kilimo zinasambazwa bei inabadilika kila siku. Tunaomba Serikali kwa kuwa kwenye mpango Serikali imesema kutakuwa na tathminini ya ufuatiliaji wa miradi, lakini pia ifanyike tathmini ya masoko ya pembejeo. Tuangalie pia masoko ya mazao yetu mchanganyiko, tunaiomba sana Serikali ifungue masoko haya ya mazao mchanganyiko. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia barabara; katika llani yetu ya Chama Cha Mapinduzi ambao tulikabidhiwa na sisi ndio tulienda kuinadi katika uchaguzi, tuna barabara mbili kubwa za lami ambazo tunatakiwa tujengewe kutoka Mtwara Pachani kwenda mpaka Tunduru na kutoka Lumecha kwenda Kitanda hadi Malinyi Ifakara. Tunaomba sana Serikali katika mpango wake wa bajeti iziweke barabara hizo mbili katika utekelezaji kama ilani yetu inavyoolekeza. Tumeinadi ilani hiyo, tumeisema kwa wananchi kwa msingi mkubwa kwetu Wilaya ya Namtumbo Wizara ikianza

kututekelezea ujenzi wa barabara hizi mbili; kwanza, barabara ya kutoka Lumecha kwenda mpaka Ifakara kupitia Malinyi inapunguza kilomita 350 kwa barabara tunayopita sasa hivi. Kwa hiyo tunaomba sana Serikali itutetekelezee ujenzi wa barabara hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Miraji Mtaturu, atafuatiwa na Mheshimiwa January Makamba na Mheshimiwa Doroth Kilave ajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo ipo mbele yetu.

Kwanza, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwiningi wa rehema kutujalia uzima na kuweza kuwepo hapa leo asubuhi kwa ajili ya kutoa mchango katika maendeleo ya Taifa letu. Pili, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kuanza vizuri na kutoa mwelekeo wa Taifa letu ambalo, hivi karibuni tumeondokewa na Rais wetu mpendwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, mwanamapinduzi wa kweli, mzalendo na anayeipenda nchi yake. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahala pema peponi.

**WABUNGE FULANI:** Amina.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa wasilisho lake aliota jana, lakini nimpongeze yeye pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuratibu shughuli za Serikali. Kama ambavyo tunajua wao ndio waratibu wa shughuli za Serikali, kwa ujumla wake Wizara zote wanazisimamia wao. Nimpongeze sana mama yangu Jenista Mhagama pamoja na Manaibu Waziri ambao wako katika ofisi hiyo kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo nichukue nafasi hii kupongeza kwa kazi kubwa iliyofanyika katika kipindi kilichopita. Taarifa tullyosomewa hapa na Mheshimiwa Waziri Mkuu inaonyesha wazi kwamba Serikali ina dhamira ya dhati katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. Tumeona huduma za kijamii ambazo zimetajwa hapa zimefanyika katika kipindi kilichopita. Tumeona pia barabara kwa maana ya miundombinu lakini pia tumeona katika maeneo ya elimu, umeme, pamoja na usafirishaji ikiwemo na utalii kazi imefanyika kubwa katika kuhakikisha kwamba Tanzania inasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya ni pamoja na miradi ya kielelezo, miradi mikubwa ambayo imeanzishwa katika kipindi kilichopita ikiwemo *SGR*, ununuzi wa ndege, uboreshaji wa shirika letu pamoja na umeme wa Mto Rufiji. Kwa hakika hii ni misingi mikubwa ya kuleta maendeleo katika nchi yetu. Uchumi wetu lazima uimarishe kupitia mambo kama hayo makubwa.

Kwa hiyo, leo hii ukisikia mtu anabeza juhudini zilizofanya na Serikali katika muda huu, mtu huyo hajui maana ya maendeleo. Watu hao *sometimes* utakuta wanalamika kwamba Serikali haijaweka mipango mizuri, tukija kutekeleza wao wanarudi wanageuka kuanza kuilaumu Serikali. Naomba nimwombe Waziri Mkuu tusonge mbele na kama alivyotuambia jana miradi yote itekelezwe illyoanzishwa na Serikali ambayo inaweza kuleta matumaini makubwa katika maendeleo ya nchi yetu, tusirudi nyumba kwa sababu tumejipanga vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunajivunia tumefikia uchumi wa kati au kufika uchumi wa kati bila kuweka mipango kama hii. Leo hii tunapunguza gharama za usafirishaji kwa kujenga barabara nzuri. Leo tunahakikisha tuna shirika letu wenyewe la ndege, tunaambibiwa sasa zitafika kumi na mbili ni shirika au nchi itakuwa na uwezo wa kuwa na usafirishaji na kuvutia watalii katika nchi yetu, mwisho wa siku tutaweza kuongeza fedha za kigeni na kuweza kuongeza uwezo wa Serikali kuhudumia wananchi wake. Kwenye hili

nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na naomba niseme sisi Wabunge tuunge mkono Serikali yetu katika kazi nzuri inayofanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikieleza hivi hayo ni maono ya viongozi wetu, lakini maoni ya viongozi wetu pia yanasisimamiwa na Ilani bora kabisa ya Chama Cha Mapinduzi ambayo imepanga mipango na imetafsiriwa vizuri sana katika Dira ya Maendeleo pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Kwa hiyo, niseme tu kwamba maendeleo haya yanayofanyika yanaenda kulenga kumkomboa Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maendeleo haya yaliyofanyika huwezi kuondoa viongozi walioshiriki kwa muda wao katika kuhakikisha kwamba wanaisaidia nchi hii. *Legacy* ambayo imewekwa katika nchi hii, Mwenyezi Mungu amemtanguliza mbele ya haki Rais wetu Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, hatutamsahau kwa kazi kubwa aliyofanya katika nchi yetu. Ndio maana kama Bunge tuliazimia kwa pamoja kumpongeza na kutambua juhudzi zake. Kutambua juhudzi za Hayati Dkt. John Pombe Magufuli ni kuwafanya akina Dkt. John Pombe Maguguli wengine waendelee kufanya kazi kama aliyofanya yeye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sisi tuwe na vivu wa kuona mtu aliyefanya kazi vizuri; mapungufu madogo madogo kila mmoja hapa ana yake, inawezekana, lakini kwa yale mengi aliyofanya mazuri lazima tumuenzi na kumpongeza sana na kumuunga mkono katika mambo haya. Mfano mdogo, alikuwa ni jasiri katika kupambana na vita ya majangili wa tembo, wote tuajua, miaka ya nyuma tulikuwa na tatizo kubwa la majangili wa tembo. Tulifikia tulikuwa na tembo karibu 100,009 miaka ya nyuma ya 2014, lakini leo tembo walipungua mpaka kufika 43,000, lakini leo kwa sababu ya kazi nzuri iliyofanywa na wenzetu wa maliasili, tunafikisha tembo 60,000 katika nchi yetu. Maana yake nini? Maana yake ni kwamba tumeweza kusimamia vizuri kazi ambayo tumeachiwa rasilimali au maliasili tulioachiwa katika nchi yetu. Kwa hiyo, niwaombe sana twende kifua

mbele, kazi inayofanyika ni nzuri, tusibabaishwe na kelele za pembeni, sisi tumejipanga vizuri kuhakikisha Tanzania inakwenda mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili la utalii mafanikio yake yameonekana, leo hii tunavyoongea hapa tumeongeza kuvutia watalii. Mwaka 2015 watalii 1,137,000 mpaka kufikia 2019 tumeongeza watalii, wamefika 1,527,000; maana yake ni kwamba kupitia hivi vituo vyetu tumeongeza watalii kiasi hicho, kuja katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hapo tumeongeza fedha kama ambavyo ametuambia Mheshimiwa Waziri Mkuu, kufikia mwaka 2015 tuliongeza fedha dola bilioni 1.9 ziliongezwa katika utalii, lakini kufikia mwaka 2019 tuliongeza fedha za kigeni bilioni 2.6 ambazo zinakwenda kuongeza uwezo wa Serikali wa kutoa huduma za kijamii katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii ni kubwa ni nzuri, niwaombe sana wenzetu wa maliasili, Tanzania lazima tuongeze nguvu katika maliasili kwa sababu ndipo tunapopata fedha nyingi za kigeni. Leo hii Simba wamesema *visit Tanzania*, naomba niongeze tena, niseme *visit Tanzania, the land of Kilimanjaro, Serengeti and Zanzibar* iliweze kuvutia zaidi tunapokwenda kwenye ile robo fainali ili dunia nzima ione kwamba tuna vivutio vikubwa vya Serengeti na Zanzibar ni sehemu nzuri ya kupumzika pamoja na maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kupongeza kazi nzuri iliyofanyika, lakini naomba nikuhakikishie kwamba Watanzania wanajua kazi nzuri inayofanywa na Serikali ya CCM pamoja na viongozi wake. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa January Makamba atafuatiwa na Mheshimiwa Dorothy Kilave na Mheshimiwa Said Khatib Haji, ajiandae.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa nafasi uliyonipa ya kutoa mchango na mimi katika hoja iliyoko mezani, namshukuru Mungu kwa neema zake na baraka zake za afya na uhai na leo tumeuanza mwezi Mtukufu wa Ramadhani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa naongea mara ya kwanza tangu uchaguzi uishe, napenda kuwashukuru wananchi wa Bumbuli kwa heshima waliyonipa ya kuendelea kuwa Mbunge wao. Nampongeza pia Mheshimiwa Spika, wewe Naibu Spika, Wabunge wote waliochaguliwa na wananchi kwa kuaminiwa na dhamana hii kubwa na muhimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza wetu mpya Mheshimiwa mama Samia Suluhu Hassan kwa kushika hatamu za uongozi wa nchi yetu. Nampongeza ndugu yangu Dkt. Philip Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais, nawapongeza Mawaziri wote kwa imani ambayo Marais mawili wameonyesha kwao na tunawatakia heri na baraka wakifanikiwa katika kazi zao nchi yetu na sisi imefanikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mawili napenda kuyazungumza leo siku ya leo. La kwanza ni mambo ya Jimboni kwangu Bumbuli; mambo ya barabara, umeme, kiwanda chetu cha chai na kadhalika na la pili ni suala zima la umoja, mshikamano, utulivu na upendo mionganoni mwetu na nitaanza na hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pole za dhati kabisa kwa sababu tunaelekea mwisho wa arobaini kwa Watanzania kwa kuondokewa na kiongozi wetu jasiri na

shupavu Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Pole zaidi kwa familia hasa mama Janeth na Watoto. Msiba huu umetuingiza katika kipindi cha mpito ambacho hatukukitarajia na mpito siku zote una mashaka, wasiwasi, hofu, mshtuko na huzuni. Kwa hiyo wananchi kote waliko wana hayo mambo ya hofu, shaka, mshtuko, huzuni na wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi ambacho Watanzania wanahitaji uongozi wetu, sisi ambaao ni viongozi, ni sasa. Bahati nzuri Mheshimiwa Rais wetu mpya ametoa kwa kauli zake na vitendo vyake, ametoa mwelekeo mpya ambaao unaleta matumaini mapya ya kutupunguzia huzuni, mashaka, mshtuko na wasiwasi. Mwelekeo alioutoa Mheshimiwa Rais una sehemu nne: Ya kwanza ni kupunguza maumivu ya jeraha la msiba; sehemu ya pili ni kutuunganisha Watanzania; sehemu ya tatu ni kuendeleza mema na mazuri aliyofanya Rais wetu aliyepita; na sehemu ya nne ni mwelekeo alioutoa Mheshimiwa Rais ni kufanya maboresho, marekebisho na mabadiliko pale panapostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama leo kwa heshima na tahadhima mbele ya ninyi viongozi wangu kutoa wito wangu kwamba nasi tujielekeze huko katika mwelekeo huo huo ambaao ameutoa Mheshimiwa Rais. Kipindi ambacho nchi yetu inahitaji umoja, utulivu na mshikamano ni sasa. Kkauli za utengano, kauli za kutiliana shaka, kauli za kutuhumiana, kauli za kuhukumiana, hazijengi na zinawachanga wananchi. Mambo makubwa aliyoyafanya Rais wetu aliyepita Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli hayatafutika, hayatafutwa, hayatapotea na hayatapoteza kwa kauli yejote ya kubezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale mionganoni mwetu ambaao wanatoa maoni na ushauri wenye nia njema wa kuweka mambo sawa, wa kuyatengeneza vizuri, wasibezwe, wasihukumiwe katika dhamira zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya kauli na ushauri na maoni ipo ndani ya moyo wa mtu. Mtu anaposifu kwamba

mama Samia ameanza vizuri asihukumiwe kwamba anatafuta cheo, anapokosoa isionekane ni nongwa na anapokaa kimya isionekane amesusa. Naomba sana tusihukumiane katika dhamira za kauli na vitendo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi aliyotufanya Rais Dkt. Magufuli naweza kuichukulia kama vile ametushonea nguo nzuri kabisa ya kupendeza, akitokea mtu akaona kwamba ile nguo kuna uzi umejitokeza tuukate, isionekane dhambi; akijitokeza mtu akasema katika hii nguo kifungo kimelegea hebu tukiweke vizuri, isionekane huyo mtu ni msaliti. Mtu huyo anapofanya kazi hiyo ya kukaza kifungo au kukata uzi, nguo ikapendeza, bado sifa ni ya mshonaji. Kwa hiyo, naomba sana kwa sababu dalili nilizoziona sio nzuri sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kwamba sisi kama viongozi tunayo haki na wajibu wa kutoa maoni kuhusu mambo yetu yaendeje, lakini njama, vikundi, vigenge vyatatuweka mashinikizo kwamba kipi kifanyike, hatua zippi zichukuliwe, zippi zisichukuliwe, si sawa kabisa na haitujengei umoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wa nchi ni jukumu kubwa na la kihistoria, Rais wa nchi yetu ana madaraka na nguvu na mamlaka makubwa sana na kwa vyovyote vile katika uongozi wake anaacha alama. Mwalimu Nyerere ameacha alama, Mzee Mwinyi ameacha alama, Mzee Mkapa ameacha alama, Kikwete ameacha alama na Rais Dkt. Magufuli ameacha alama, ndio asili ya urais. Sasa wajibu wetu sisi kama viongozi tulipo ni kulinda yale mema ambayo viongozi wetu wameyafanya kuanzia wakati wa Mwalimu, mpaka Rais Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tupiganie kuyalinda yaliyofanywa na Rais Magufuli, lakini tusipigane wakati tunafanya hivyo. Tukipigana kwa mambo ya nyuma, tutashindwa kupigania mambo mazuri ya mbele ambayo Rais mpya anataka kuyafanya. Vikumbo vyatatuweka nani ni mnazi zaidi wa Rais Dkt. Magufuli, nani mnazi zaidi wa Rais Samia

na viwiko vikali ambavyo watu wanataka kupigana havisaidii wala kujenga. (*Makofi*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imegonga.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba upendeleo wa dakika tatu nimalizie.

**NAIBU SPIKA:** Hapana, majina ninayo mengi sana hapa mbele, ahsante sana.

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na makubwa mbele...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba tuheshimiane, tusihukumiane na tumsaidie kiongozi wetu, tuwe na umaja na upendo kwa sababu utulivu ndani ya Bunge ndio utasaidia kiongozi wetu atawale vizuri. Ahsante sana. (*Makofi*)

Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Dorothy Kilave, atafuatiwa na Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mheshimiwa Ali Hassan King ajiandae.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema, aliyeweza kutukutanisha mahali hapa na hata tukaweza kuanza mfungo siku nzuri hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Waziri Mkuu kwa hotuba iliyojaa matumaini na maendeleo kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa mama Samia Suluhu; najivunia kuwa mwanamke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kuwapongeza sana Mawaziri wote mlioteuliwa kwa kazi nzuri ambayo najua iko katika nafasi zenu ambayo tunakwenda kuitendea haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba nimeweza kuona mambo mengi ambayo yamesemwa katika hotuba ile ya Waziri Mkuu, kwamba tutakwenda kutekeleza miradi yote ya kimkakati ambayo imepangwa, lakini pia nimeona kwamba yako malengo mazuri ya Serikali iliyoko madarakani bila kusahau kuibua miradi mipya inayokwenda kuendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende sana pia kuwapongeza sana kwamba tutakwenda kuitendea haki llani ya Chama Cha Mapinduzi. Kwamba mengi tumeyaandika katika llani yetu ya Chama Cha Mapinduzi, na ninaamini kwa jinsi ambavyo tunakwenda, tutakwenda kuikeleza kwa ukamilifu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado naomba niendelee kuipongeza Serikali yetu, kwamba imefanya kazi nzuri sana katika miundombinu, hasa miundombinu ya barabara kubwa ambazo zimeonekana kila mahali tunakopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuipongeza kwamba tumeweza kuunganisha mkoa kwa mkoa, wilaya kwa wilaya na hata tunafikia sasa kuona kwamba tunapita kwa ujasiri wote tukitaka kwenda katika mikoa fulani fulani bila kuwa na msongamano wala kuwa na makorongo ya namna tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kwamba pamoja na kwamba nawapa hongera kwa kutengeneza miundombinu ya barabara, lakini niseme sasa umefika wakati wa kuona ni namna gani sasa miundombinu ya barabara

hizi inakwenda kuunganisha kati ya kata na kata, hata tuweze kuunganisha Kijiji na Kijiji ili tuweze kuona sasa yako mambo mazuri ambayo Serikali yetu imeyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejengewa zahanati nzuri sana katika kata zetu, tumejengewa masoko, tumejengewa stendi za mabasi, hasa kwetu Dar es Salaam. Lakini kutoka kwenye kata yako kufika kwenye kata nyingine kwa ajili ya kwenda kwenye zahanati au kwenye soko au kwenye stendi ya mabasi, hizi barabara kwa kweli ni tatizo. Hazina mwonekano mzuri. Naamini si kwa Dar es Salaam tu lakini naamini kwa hata mikoa mingine, nasemea kama Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuombe sasa basi, kama kuna namna yoyote ya *TARURA* kuongezewa au kutafutiwa fedha za kuweza kufanya barabara hizi zипитке, niombe sana Bunge lako Tukufu tuweze kupitisha au tuweze kuona namna gani ya kujadiliana ili tuweze kupata fedha za kuwapa hawa *TARURA* maana naamini tumeongea nao sana lakini fedha walizokuwa nazo ni ndogo sana kiasi kwamba hawawezi kufanya miundombinu katika barabara zetu zile za ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama jinsi mwenzangu jana aliongea kuhusiana na Mradi wa *DMDP* Mkoani Dar es Salaam, Mheshimiwa Bonnah aliongea vizuri sana, lakini bado naomba nisisitize, kama alivyosema sisi Dar es Salaam tunatamani kulima lakini hatuna maeneo ya kulima. Sasa inapendeza sana kama tutapata Mradi huu wa *DMDP*ili sasa mafuriko yaliyoko katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam yaweze kukatika na hata tuone kwamba barabara zetu zinaweza kupitika vizuri na vilevile kufanya maendeleo katika kata zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana, pamoja na mambo mazuri ambayo Serikali imefanya. Lakini naomba pia niweze kuona kwamba Jimbo langu la Temeke nilisemee ya kwamba hakika kabisa kata zile 13 tumekaa vizuri, tumepata

maeneo mengi mazuri, lakini bado nalilia barabara hizi za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Temeke wako vijana wengi waliopitia JKT na vilevile walikwenda katika huduma ile ya kujenga ukuta ule wa Mererani lakini pia waliweza kuingia katika kujenga ukuta wa ikulu. Lakini sasa hivi wamerudi na makaratasi tu ya kwamba wamehitimisha kufanya yale mambo lakini tunapokwenda kuomba ajira, vijana wetu hawa wa JKT hawaangaliwi wala hawapewi chochote kwenda kufanya kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sasa Serikali yako kwa usikivu kabisa waangalie basi hizi hatma za vijana wetu illi waweze kupata kazi maana ndiyo hasa tunaowategemea katika kipindi kijacho, sisi tunakwenda kuzeeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Temeke tuna tatizo kubwa sana la umeme kukatika kila wakati. Umeme huu sasa sijui umekuaje, mwenzangu wa Mbagala aliliongelea hili. Nami niseme, hata sasa hivi hapa nina meseji ambayo tayari umeme umekatika, kwetu Temeke imekuwa ni salamu sasa hivi kwamba ikifika asubuhi lazima ukatike ama saa mbili au saa tatu au saa nne. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sioni namna gani ambavyo *TANESCO* watatusaidia ili tuweze kupata umeme kama wenzetu. Na ukizingatia sana kwamba Jimbo letu la Temeke tunayo miradi mingi ya wafanyabiashara na makampuni mengi ya uzalishaji ambayo yanazalisha kuitia huo umeme ili hata sisi wenyewe kama manispaa tuweze kupata fedha za ndani katika makusanyo ya viwanda hivi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu kuunga mkono hoja, lakini niombe haya niliyoyasema tuweze kuangaliwa na kutimiziwa. Ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khatib Said Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan King, Mheshimiwa Yahya Mhata ajilandeae.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuweze kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote nipende kuwataki Watanzania wote heri na baraka ya Mfungo wa Mwezi wa Ramadhan ambao tumeuanza leo, Mwenyezi Mungu atujalie tuifunge kwa heri na tumalize kwa heri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru wenzetu ambao si Waislamu lakini wameonesha kutuunga mkono kwa njia zote. Nikiangalia leo Bunge lako hijabu zimeongezeka, si kwa Waislamu peke yake, na mavazi ya staha yameongezeka sana. Na hii ni kutuunga mkono na kutusaidia kutupunguzia majaribu; ahsanteni sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia hotuba hii kwa kusema yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, sisi wote ni Watanzania na tunajenga Tanzania moja. Tuna wajibu wa kuyaenzi yale mema yote ambayo... katika nchi yetu. Binafsi toka imeanza hotuba ya mpango na mpaka tunakwenda hotuba ya bajeti, nimesikiliza sana, nimekaa kimya sana kuyazingatia sana yanayosemwa na naomba niseme tu, hoja hujibiwa kwa hoja, hoja haipigwi rungu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapotoa hoja ikaonekana hoja zetu wakati mwingine zinakinzana na yale mawazo waliyonayo wenzetu, wajaribu kutujibu kwa hoja zile zile ili mwisho wa siku tufikie mwafaka katika kujenga Taifa letu hili moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitamke bayana, sioni aibu, hata kama ni mpinzani, kusifia lolote jema linalofanywa na

Serikali hii. Lakini hali kadhalika, msione soo! Pale tunapolisema lolote baya linalofanywa na Serikali hii kwasababu lengo linarudi palepale, kwamba lengo letu ni kujenga nchi moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia kuhusu miradi ambayo ilianza katika utawala wa Awamu ya Tano. Niseme wazi, wako wasomi, wachumi, walioongelea sana kuhusu miradi lakini nitamke bayana, miradi ambayo imetumia fedha nyingi za Watanzania kwa malengo ya kuliletea tija Taifa hili, hata kama kuna kasoro zinazoonekana katika utekelezaji wa miradi ile, hatuwezi kui-*dump* miradi ile kwasababu ya kasoro hizo. Na kufikiria kui-*dump* miradi hii na kuitelekeza kwasababu ya kasoro zilizopo ni kosa moja ambalo kizazi kijacho kitatuhukumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesiklia baadhi wakisema kwamba mradi wa bwawa la umeme hauna tija na utupiliwe mbali, nimesikitika sana. Mama mwerevu anapopika chumvi ikazidi kwenye nyungu, watoto wanashibiri chakula, haendi kulitupa lile sufuria watoto wakafa njaa, ataongeza maji ukali wa chumvi upungue na watoto waweze kula; huyo ndio mama mwerevu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Watanzania, Wabunge sisi, tuna wajibu wa kuyaona makosa yaliyomo kwenye miradi ile, tusiwe wanafiki wa kusifia kila kitu wakati tunajua yako mapungufu ambayo yanatakiwa kurekebishwa ili kazi iendelee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono mradi wa bwawa uendelee (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, naomba kasoro zilizopo katika Mradi wa Bandari ya Bagamoyo tuangalie tena upya, mahitaji ya Bandari mpya ya Bagamoyo bado ni muhimu kwa uchumi wa Taifa letu, ni muhimu kwa ustawi wa viwanda viliviyotarajiwa kujengwa maeneo ya Bagamoyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wasafiri wa kwenda Zanzibar tunapopanda boti mara kwa mara, hakuna siku utakuta hapana meli chini ya 50 ambazo zinasubiri kufunga geti katika Bandari ya Dar es Salaam, hakuna. Inaaishiria bado kuna mapungufu katika Bandari ya Dar es Salaam. Kupata Bandari ya Bagamoyo ni ukombozi wa eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipofikiria kujenga Bandari ya Bagamoyo wenzetu wa Kenya hawakuwa hata na wazo la kujenga Bandari ya Lamu, walipotusikia tu wao walianza, na tayari Bandari ya Lamu imekamilika. Sisi bado tunakaa tunabishana tukidhani kwamba kuna kasoro; kasoro zirekebishwe na kazi iendelee, hayo ndiyo mawazo yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na katika hili, kipekee sana nampongeza kiongozi wangu wa chama, Mheshimiwa Zitto Kabwe. Katika maoni yake yote ameonesha kukubaliana na mapungufu lakini akitaka kazi nzuri iliyoanza tufikirie namna ya kuifanya, kazi iendelee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie katika ukurasa wa 22 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameongelea suala la uendeshaji mashtaka na utoaji wa haki. Nipende kusema kwamba huu ni Mwezi Mtukufu wa Ramadhani; tarehe 03 Novemba, 2014, nilisimama hapa kuongelea ucheleweshwaji wa kesi na niligusia sana kuhusu kesi ya Mashekhe wa Uamsho kutoka Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema – wakati huo kesi ile nadhani ikiwa kama na miaka minne – leo tena ni Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, nasimama hapa kusema, tayari umefika mwaka wa nane, tunakwenda mwaka wa tisa. Kesi ile imechelewa sana na wanasiwa wanapenda kusema *justice delayed, justice denied*, lakini wanazungumza mdomoni, hawaitafsiri kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mshtakiwa anapokwenda mahakamani anachokisubiri ni hukumu ya

makosa yake. Haki ya mtuhumiwa ni kuhukumiwa, siyo kukaa gerezani katika kipindi kirefu. Kunyongwa ni hukumu, kufungwa maisha ni hukumu, kufungwa miaka kadhaa ni hukumu; ni haki ya mshtakiwa kulingana na makosa yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unapomnyima hizo hukumu wakati ilikuwa ni haki yake tayari unamyima haki yake ya msingi. Matokeo yake ni nini; kwa mujibu wa sheria zetu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri anayo mamlaka ya kumsamehe mfungwa yeoyote aliyeko gerezani. Lakini Mheshimiwa Rais hana mamlaka ya kumsamehe mtuhumiwa aliye na makosa. Kuchelewesha kumpa hukumu mtuhumiwa aliyeko gerezani ni kumnyima Rais wa Jamhuri haki yake ya kuwahurumia baadhi ya wafungwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano tulionao leo, akina Babu Seya leo wasingegekuwa huru kama wasingegekuwa wamehukumiwa. Kama wangekuwa wanaendelea kushutumiwa na kukaa pale mahabusu, bado wangekuwa wako mahabusu. Lakini kwasababu walihukumiwa, Mheshimiwa Rais alitumia nafasi yake ya kikatiba kuwasamehe watuhumiwa wale, na leo wako huru na familia zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda mwaka wa tisa, sheria zetu Waheshimiwa Wabunge, tuna dhima kwa Mwenyezi Mungu tunapopitisha sheria ya kwamba anayehukumiwa kwa kosa la ugaidi, utakatishaji fedha, uhujumu uchumi, akishtakiwa kwa makosa hayo hapewi dhamana. Tuangalie upya namna gani ambavyo tunakiuka haki za msingi za binadamu. Kwasababu laiti ingekuwa anayeshtakiwa kwa makosa haya ana hukumu ya kukaa katika hali ya kuwa mahabusu, ingekuwa bado tumetenda haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwendesha mashataka anapoamua tu kwamba shtaka hili linaangukia katika maeneo haya matatu basi huyo haki yake ni kukaa rumande katika muda usiojulikana. Waheshimiwa Wabunge,

kama tunalamikia kupanda kwa bei za *bundles* na tukapiga makelele ikasimama, kikokotoo kikasimama; kwa nini tusilalamikie haki za wananchi wetu ambao wakishtakiwa kwa makosa hayo wanasona magerezani kwa muda wa miaka kadhaa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *Walahi* juzi kuna mama mmoja alikwenda kumuangalia mtoto wake katika washtakiwa wale wa uamsho, alipotoka mahakamani tu umauti ukamchukua. Alipotoka Segerea hajarudi kwao Zanzibar, umauti ukamchukua kwa uchungu aliopata kwa watoto wake kukaa gerezani muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaapa kwa Mungu kila siku atuongoze kufanya mema na tumshauri Rais katika mambo ili nchi hii ipate tija kwa Mwenyezi Mungu.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, ahsante, kengele ya pili imeshagonga, ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Ali Hassan King, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahya Mhata, Mheshimiwa Neema Mgaya ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Na mimi awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na kupata uzima katika siku hii ya leo kuja kuchangia kwenye bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza katika mjadala wangu ambao nataka kuchangia ni ukurasa wa 22 ambao Mheshimiwa Khatib amegusia. Lakini nitagusia katika utoaji wa haki, na hasa katika ujenzi wa mahakama ambazo zinajengwa na utaratibu unaotumika sasa hivi ambao unachangia katika utoaji wa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ukurasa huo, nitaunganisha na ukurasa wa 74 mpaka 76 wa hotuba ya Waziri ambapo ameelezea utatuzi wa changamoto za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mimi niipongeze Serikali katika kutatua zile changamoto tano za Muungano ambazo zimeelezwa pale, zimefanyiwa kazi, na tunaipongeza na kuishukuru sana Serikali yetu kwa kutatua changamoto hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika kuondosha umaskini, kuna Mfuko wa *TASAF* unatumika vizuri; kuna Mfuko wa Mazingira unatumika vizuri katika pande zote mbili za Muungano. Sasa kwa mujibu wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ambayo ukurasa wa 278, katika kifungu 227(c) ambacho kinasema kwamba tutahakikisha masuala muhimu ya Muungano yanaratibiwa kwa faida ya pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili nirudi katika ile miradi. Kuna miradi ya utoaji wa haki ambayo inafadhiliwa au ni mkopo kutoka *World Bank*. Miradi hii inafadhiliwa na *World Bank* katika upatikanaji wa haki kwa Tanzania nzima. Na miradi hii inahusisha mkataba ambao ulisainiwa na Mheshimiwa Rais wa dola milioni 65 ambazo ni sawa na bilioni 135, kwa ajili ya upatikanaji wa haki.

Nachozungumzia hapa kwamba mgao wa Zanzibari mpaka hivi sasa hivi tunazungumza haujapatikana katika fungu hili, hicho ndicho ambacho hoja yangu ya kwanza niliyotaka kuizungumza. Kwenye bilioni 135 Zanzibar haijaenda hata elfu mbili,

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ikumbukwe kwamba Zanzibar sio mwananchama wa *World Bank*, mwanachama wa *World Bank* ni Tanzania na Zanzibar anakuwa kupitia Tanzania naye ni mwanachama kwa hiyo anastahili kupata mgao wake kupitia fungu hili. Na hili nilizungumze katika majukumu ya Tume ya Pamoja ya Fedha

ambayo katika Katiba ibara ya 133 na 34 inazungumzia kwamba itakuwa na kazi ya kuchunguza kwa wakati wote mfumo na shughuli za fedha za Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika masuala ya kifedha kati ya Serikali mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hapo mimi ndiyo kwenye hoja yangu ambapo nazungumzia kwamba kuna fungu lilipaswa kwenda Zanzibar kwa ajili ya kufuatilia utoaji wa haki. Kwa hiyo naishauri Serikali ilifanyie kazi hili. Katika hotuba ambayo Rais wetu mama Samia alivyokuwa anawahutubia mawaziri wakati anawaapisha na Katibu Mkuu Kiongozi alizungumzia changamoto hiyo, kwa hiyo tulikuwa tunaomba ipatiwe ufanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la pili, tunazungumzia masuala ya uhusiano wa kimpira, *football* kuna *TFF*, *TFF* inatuwakillisha Tanzania nzima, *TFF* anapopata msaada wa fedha au ruzuku ya fedha kutoka *FIFA* inapaswa pia na Zanzibar nao wapate. *FIFA* kila mwaka inatoa dola 1,500,000 kwa ajili ya maendeleo ya soka Tanzania lakini kwa miaka mingi hakuna hata senti tano ambayo imekwenda Zanziba.

Mheshimiwa Naibu Spika, na Zanzibar hawezi kuwa mwanachama wa *FIFA* kwa sababu Zanzibar hawezi kujunga na shirikisho lile la kimataifa. Au, kama inavezekana basi kama hizi fedha haziwezi kugawiwa iruhusiwe na Zanzibar ijiunge kwenye haya mashirika; na kama haiwezi kujunga sheria haikubali basi huu mgao ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna mkataba umesainiwa na Korea Kusini pamoja na Falme za Kiarabu, lakini *TFF* amesaini peke yake, Zanzibar haiwezi kwenda kusaini mkataba huo. Kwa kuwa haiwezi kwenda kusaini mkataba huo, ilikuwa tuiombe Serikali sasa iiambie *TFF* kama wao wanaweza kwenda *FIFA* basi labda na Zanzibari iruhusiwe kwenda *FIFA*, hilo nalizungumiza hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, linguine ni kuhusu ushirikishwaji wa Timu ya Taifa. Kuna jambo jana nililisikiliza

sana nikasikitika sana, na hili nilikuwa naomba Wabunge wanisikilize vizuri. Nimesikiliza maelezo yaliyotolewa na Mwenyekiti wa Chama kimoja cha upinzani ambayo anasema ye ye anawahutubia Watanzania kwamba Watanzania wamsikilize ye ye maneno ambayo anayasema.

Nimeisikiliza hotuba yake kuanzia mwanzo hadi mwisho, Lakini kitu, alichokuwa anazungumza ni kana kwamba Watanzania wote wadai haki ya kuchaguliwa kuwa na mamlaka ya kama labda kuwa Rais au kuwa Wabunge. Hakuongea jambo la kijamii hata moja. Sasa Watanzania hawa hawapo kama hivyo, hakuna haki kama hiyo ya kwamba watanzania wote wanahitaji haki moja tu, watanzania wanahitaji haki nyingi. Miongoni mwa haki ambazo Watanzania wanahitaji ni kupata elimu, kupata maji safi na salama, kupata usafiri, maisha yao yawe mazuri, wapate na mambo mengine, sasa haya yote hajagusia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania hawa hivyo leo wanasomeshwa bure hivyo kweli wakatazame haki moja tu? Watanzania wanazunguka kila nchi, watu wa Dar es Salaam pale safari zao wanakwenda vizuri, hivyo kweli ukawashauri Watanzania kwa matakwa yako wewe kwamba wadai haki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa mfano, mmoja tukienda kule katika Jimbo la Hai kati ya watu 300,000 waliotaka Ubunge ni wawili tu, kwa hiyo wewe uliyekosa usiwashawishi wengine kwamba hii nchi haikutenda haki. Watu hawa wamepatiwa haki katika elimu, afya, usafiri, pamoja na masuala yao chungu nzima ya kijamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tuwapeleke darasani, kuna *Abraham Maslow's hierarchy of needs*. Katika *hierarchy of need* cha kwanza ni *basic needs*, nicho watu wengi wanachohitaji. Hawa wanaohitaji mahitaji mengine ni wachache, kwa hiyo huwezi kuwashawishi Watanzania katika mahitaji haya machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *basic needs* kuna elimu, chakula na vitu vingine. Watu wamepatiwa umeme pamoja na mahitaji yao muhimu. Hivi hatuoni umuhimu wa kumuheshimu huyu ambaye aliyefanya hizi huduma za jamii na muhimu zikapatikana?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi maoni yangu kwa Watanzania hawa tuwapuuze na tuwapuuze kama ushuzi wa ngomani, maana ushuzi wa ngomani hata mtu hashughuliki na harufu, tuwapuuze kama ushuzi wa ngomani...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana mheshimiwa.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Yahya Mhata atafatiwa na Mheshimiwa Neema Mgaya, Mheshimiwa Hawa Chakomo Mchafu ajiandae.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake kwa bajeti ambayo waliwasilisha jana. Naomba nijiongoze katika maeneo yafuatayo;

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ahadi ambazo viongozi wetu wa juu wanazitoa ambazo kwa kweli zinahitaji kutekelezwa kwa sababu ahadi ya viongozi hao ni maagizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2011 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa awamu ya nne alitoa ahadi pale Nanyumbu kujenga kituo cha afya katika Kata ya Mkangaula. Ahadi ile imekuja kutekelezwa mwaka jana. Katika utekelezaji wa ahadi ile zilitolewa milioni 200 lakini

milioni 200 mpaka sasa hivi hazijatolewa. Kwa hiyo naomba Ofisi ya Waziri Mkuu, jambo hili liangaliwe katika utekelezaji wa ahadi za viongozi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hiyo haitoshi Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwahi kufika Mangaka tarehe 26/2/2018 na akatoa ahadi ya kujenga barabara zetu za lami kilometra tano; mpaka sasa hivi hakuna hata kilometra moja iliyotekelzeza. Kwa kweli naomba sana, ahadi hizi zinapotolewa wananchi wana imani na viongozi wetu, na zisipotekelezwa tunatoa mashaka kwa wananchi wetu kuwaamini viongozi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mama yetu Rais, Samia Suluhu Hassan alipokuja kwenye kampeni pale Nanyumbu alitoa ahadi ambayo ipo ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kujenga barabara ya lami itakayounganisha Mkoa wa Mtwara na Morogoro kupitia Seluu; na barabara ile inaanzia ndani ya jimbo langu. Ni matarajio yangu kuwa utekelezaji wa ahadi ile utaanza katika mwaka huu wa fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba sana niungane na Waheshimiwa Wabunge ambao jana walizungumza, kwamba kuwe na kitengo maalum cha kuratibu ahadi za viongozi wetu. Mheshimiwa Rais wetu mpenzi ambaye ametangulia mbele ya haki kuna ahadi nyingi alizotoa, ni matarajio yangu zitatekelezwa ndani ya awamu hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mfuko wa wanawake, vijana, na wenyе ulemavu; mfuko huu unategemea mapato ya Halmashauri. Halmashauri nyingi mapato yao ni madogo sana. Wanaonufaika na mfuko huu ni zile Halmashauri ambazo zinauwezo wa kimapato. Lakini mimi *concern* yangu ipo katika asilimia mbili ya walemovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mlemavu na ni Mbunge wa Jimbo, tunazo changamoto kubwa sana sisi walemovu halafu mnatupangia asilimia mbili, jamani

hamtuonei huruma. Ninyi wazima mnaweka asilimia nne na sisi walemavu mnatupa asilimia mbili pamoja na changamoto zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kuishauri Serikali, lazima mfuko huu wa wawalemavu uangaliwe na usitegemewe fedha za Halmashauri. Serikali Kuu itenye fedha kwa kila Halmashauri kuwasaidia hawa walemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, walemavu tuna changamoto kwenye elimu. Tunasoma katika mazingira magumu na baada ya kusoma tunategemea tupate ajira. Ukisoma sheria ya ajira kifungu cha 31 (2) ajira za walemavu imeeleza bayana kila mamlaka itakayoajiri watu kuanzia ishirini na kuendelea asilimia tatu wawe walemavu. Najiuliza sheria hii inatekelezwa? Ni kweli taasisi zetu, Wizara zetu zinaasillimia tatu ya walemavu? Na mimi namshukuru sana Mheshimiwa Rais, ndani ya Wizara hii Naibu Waziri ni mlemavu, naamini ataisimamia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nyingine naomba nijielekeze kwenya afya. Kule Jimboni kwangu kuna mgogoro wa afya. Kuna fedha zilitakiwa ziletwe ndani ya Jimbo langu kujenga kituo cha afya Nanyumbu...

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mhata kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa

## TAARIFA

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimsahihishe tu Mheshimiwa anayeongea pale, asahihishe, watu wenye ulemavu sio walemavu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Spika, Yes

**NAIBU SPIKA:** Toa taarifa yako

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yangu ni kwamba nataka nimsahihishe kwamba ni watu wenyewe ulemavu na sio walemovu. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Mhata unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana mlemavu mwenzangu amenisahihisha, ni watu wenyewe ulemavu, na ulemavu ni wa aina zote; nashukuru sana kwa masahisho hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze tatizo la Wizara ya Afya katika Jimbo langu. Tuna kituo cha afya ambacho killitengewa fedha kwenye Hospitali, kwenye Kituo cha Afya Nanyumbu. Fedha zile hazikuja Nanyumbu, fedha zile kuna mahali zimepelekwa. Uthibitisho wa hili vifaa tiba vikaletwa Nanyumbu; sasa tukawa tunajiuliza vifaa hivi vinakuja kwa hospitali gani? tumeshindwa kuelewa. Kwenye hili naomba Ofisi ya Waziri Mkuu itusaidie. Fedha hizi wamezipeleka wapi kujenga kituo cha afya? kwa sababu tumeletewa *machine* kwa ajili ya kituo cha afya ambacho hakipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo nawaomba sana, wananchi wapale wanamasikito makubwa kwamba kuna fedha Serikali yao ililetu kwa ajili ya kituo cha afya lakini fedha zile hazikufika na badala yake waletewa mitambo (*machine*) kwa ajili ya kituo cha afya ambacho hakijajengwa. Kwa hiyo mimi nina imani kwamba hizi fedha kuna mahali zimekwenda kimakosa, naomba huko zilikokwenda zijereshwe ili wananchi wa Jimbo langu wanufaikie na huduma hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nijielekeze katika suala la ufundi ndani ya wilaya yetu tuna majengo yaliyoachwa na kampuni ya kichina ambayo walikuwa wanajenga barabara ya kwenda mpakani Mtambaswala. Majengo yale ni mengi na yapo pale ndani ya Kijiji cha

Maneme ndani ya Tarafa ya Nanyumbu; majengo yale yangeweza kutumika kikamilifu kwa shughuli ya elimu ya ufundi. Naomba niishauri Serikali, majengo yale yapo pale *idle* na yanazidi kuharibika ni bora yakatumika kwaajili ya elimu ya ufundi. Uwekezaji wake hautakuwa mkubwa kuliko kuuanza upya. Kwa hiyo naomba sana wizara inayohusika tuyatumie majengo yale ili kufufua elimu ya ufundi ndani ya wilaya yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nazungumzia kwenye kilimo. Mheshimiwa Mwambe amezungumza kwamba kilimo chetu kimeathirika sana, uzalishaji wa kilimo wa zao la korosho umeathirika kutoka tani 324 hadi tani mia mbili na kitu, na sababu kubwa zinajulikana na mojawapo ni mbegu bora ambazo tulitegemea wakulima wazitumie hazikutumika. Kwa maana ya *Sulphur I mean* pembejeo za kilimo na mambo mengine. Wananchi wa jimbo langu walitumia fedha, walitumia nguvu zao kuzalisha mbegu za korosho ambazo miche ile waliwauzia Bodi ya korosho, lakini huu ni mwaka watatu mpaka sasa hivi hawajalipwa pesa zao...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Mgaya atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Mchafu, Mheshimiwa Mansoor Shanif ajiandae.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kutoa pole kwa watanzania wote kwa msiba mkubwa uliotupata lakini vilevile nitambue mchango mkubwa uliofanywa na Hayati Dkt. Magufulsi kwa kushirikiana na mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Ni mchango mkubwa sana uliofanyika ndani ya muda mchache sana na mafanikio makubwa sana, tumeyaona na tutayaendelea kuyaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nijielekeze katika masuala ya kilimo na mazao ya mbogamboga. Ni zaidi ya asilimia 90 ya mazao ya mbogamboga yanayosafirishwa kuititia bandari ya Mombasa, kitu ambacho kinawapa gharama kubwa sana wafanyakibashara na wakulima wa mazao haya ya mbogamboga. Natambua Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda wamekaa kwa pamoja na kuweza kuanzisha mradi wa *Kurasini Agricultural Logistic Hub* itakayokuwa *once stop center* ambayo ndiyo itakuwa *cold chain* ya mazao haya ya mbogamboga yanapokuwa yanasubiri kwenda kusafirishwa nje ya nchi kwa kutumia bandari yetu ya Dar es Salaam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mradi huu ni mradi ambaao umehusisha sekta binafsi. Niwapongeze sana Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda kwa kuwa wasikivu kwa sababu haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ambayo aliyatoa wakati akiwa Makamu wa Rais mwaka jana. Kwa kweli viongozi wa namna hiyo ndio ambaao tunawahitaji katika Taifa letu la Tanzania; pale mkubwa anapotoa tu maelekezo na kuweza kuyafanyia kazi mara moja. Lakini kwa kuwa *Kurasini Agricultural Logistic Hub* ndio muarubaini wa mazao ya mbogamboga kusafirishwa kuititia bandari kwenda nje, nilitaka kujua, ni lini mradi huu utakamilika na kwa sasa hivi mradi huu umefikiwa wapi? Ili tuweze kujua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo tunatambua kwamba imeanzisha mchakato wa Bodi ya *Horticulture*. Nataka kujua pia bodi hii ipo kwenye *stage* gani na lini itakamilika. Sababu katika mazao ya mbogamboga kuna zao ambalo linakuja kwa kasi sana, zao la parachichi.

Na kama tunavyojuu ni mikoa zaidi ya kumi Tanzania inalima zao hili la parachichi ikiwemo mkoa wa Njombe, Iringa, Songwe, Mbeya, Rukwa, Tanga na mikoa mingine. Kuna umuhimu sana wa bodi hii ya horticulture kukamilika ili zao hili la parachichi pamoja na mazao mengine ya mbongamboga yawe yanafanyiwa kazi kwa utaratibu mzuri na kuweza kuleta tija kwa wakulima wa mazao haya ya mbogamboga likiwemo na zao la parachichi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika zao hili la parachichi, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja Njombe akatembelea baadhi ya mashamba ya parachichi, nilimuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba zao hili sasa ikiwezekana liwekwe katika zao la kimkakati kutokana na umuhimu na unyeti wake. Zao hili kama tutalismamia vizuri tutaweza kuongeza mapato ndani ya Taifa letu lakini vilevile tutawakwamua wananchi kupitia ajira kupitia ajira mbalimbali zitakazotokana na zao hili la parachichi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, fursa hii tunayoionna sisi ya kulima zao la parachichi na kusafirisha nje, imeonwa na nchi nyiningi nydingi. Ombi langu kwa Serikali ni kuhakikisha kwamba wanawasaidia wananchi ambaowanalima zao hili la parachichi kwa kuweka mikataba mizuri na nchi walajji kwa maana kwamba watakapokwenda kuuza hili huko nje Serikali imeshaweka mikataba itakayokuwa inawasaidia wananchi wetu wasikandamizwe. Kama hii fursa imeonwa sasa hivi na nchi nydingi baadaye soko linaweza kuharibika. Kama sisi tutakuwa tumewahi kuweka mikataba mizuri ina maana tutakuwa tumewasaidia kuwalinda wananchi wetu wasiweze kutaabika siku zijazo kutokana na *supply* kuwa kubwa na *demand* kupungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa Serikali imefanya kazi nzuri, imeshaagizia ndege ya mizigo kwa ajili ya kuweza kusafirisha mazao haya ya mbogamboga ikiwemo na parachichi na vilevile natambua kwamba Serikali imeandaa mfumo mzuri wa *cold-room* katika Kiwanja cha Ndege cha Songwe, lakini bado siyo wote wanaweza kusafirisha kwa kutumia ndege wengine watatumia Bandari

ya Dar es Salaam. Pamoja na kuanzisha mradi mzuri ule wa Kurasini, bado kuna umuhimu wa kuboresha mfumo wa *cold room* kwenye baadhi ya mabehewa katika Reli yetu ya TAZARA ili wale wananchi wa Nyanda za Juu Kusini ambao wanalima zao hili la parachichi waweze kusafirisha parachichi yao kuanzia ile *process* ya kutoa shambani, kusafirisha sasa kutoka kule Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, kupelekeka Dar es Salaam waweze kutumia reli hii ambapo gharama ni nafuu kuliko usafiri mwagine watakaotumia mfano kama vile maroli na kadhalika ambayo gharama ni kubwa sana.

Kwa hiyo, kwa kutumia reli, wanaweza wakasafirisha kwa gharama nafuu na hapo ndiyo tutaona umuhimu wa kutumia ile Bandari ya Dar es Salaam baada ya kumaliza mradi ule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuzungumzia Bima ya Afya. Tunashukuru Bima ya Afya iko vizuri lakini kuna maboresho makubwa yanatakiwa yafanyike kwa wananchi, kwa sababu wanalamika, wanapotumia Bima ya Afya ya Serikali kule hospitali hawapati dawa, kuna umuhimu wa kuboresha. Vilevile, ukija kwa Wabunge humu ndani, Wabunge wengi Bima hii ya Afya haiwafaidishi kwa sababu utakuta watu wengine ni wazee, kwa mfano, Mzee Mheshimiwa Athuman Maige, mama yangu Mheshimiwa Margaret Sitta, hawana watoto wenye chini ya miaka 18. Vilevile utakuta kuna Wabunge vijana humu, hawana watoto wadogo, hawajazaa kabisa. Kwa hiyo, bima hii ijielekeze kutumika kwa watu tegemezi, kwa maana kama mama yangu pale Mheshimiwa Margaret Sitta na baba yangu Mzee Mheshimiwa Athuman Maige, bima ile ikasadie wazee wao maana wazazi wao wapo. Vilevile kwa vijana hawa ambao hawana watoto ikasaidie wazazi wao.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Bima hii ya Afya iangaliwe na ifanyiwe maboresho makubwa kwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini vilevile kwa wananchi wetu ili iweze kuleta tija na maana halisi ya Bima ya Afya. Kwa sababu nia yetu ni kusaidia wananchi lakini vilevile kuwasaidia Wabunge ukiwemo na wewe na Mheshimiwa Naibu Spika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, ahsanteni sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na siyo kwamba nafagilia kugombea Ukamishna. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Aaah, kwa hiyo hugombei tena? Ndiyo unamaanisha hivyo?

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nagombea ila hoja muhimu. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. (*Kicheko*)

Naona umemtaja hapo Mheshimiwa Maige, sina uhakika unataka kumsemea kuhusu kuwa na watoto wadogo lakini Mheshimiwa mama Sitta labda huyo unaweza ukamsemea. (*Kicheko*)

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Hawa Chakoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Shanif, Mheshimiwa Oran Njeza ajiandae.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Nianze kwa kusema naunga mkono hoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujielekeza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujikita zaidi katika Kamati ya Masuala ya UKIMWI. Sote hapa tutakubaliana kwa namna moja ama nyingine kila mmoja ameguswa na janga hili la UKIMWI, kama siyo yeye mwenye basi ndugu yake, jirani yake ama rafiki yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu nchini Tanzania zinaonesha kila siku iendayo kwa Mungu watu 200 wanaambukizwa UKIMWI na Virusi vya UKIMWI, watu 6,000 kwa mwezi na watu 72,000 ndani ya mwaka. Bado tukiziangazia takwimu, Mkoa wa Njombe ndiyo mkoa nchini Tanzania unaoongoza kwa maambukizi ya makubwa kwa asilimia 11.4, ukifuatiwa na Mkoa wa Iringa wenyе asilimia 11.3, ukifuatiwa na Mkoa wa Mbeya wenyе asilimia 9.3. Hii ndio mikoa *top three* nchini Tanzania inayoongoza kwa maambukizi ya UKIMWI na Virusi vya UKIMWI. Hivyo, ni kuonyesha ni kwa namna gani UKIMWI bado ni janga la Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na takwimu hizo na hali ya maambukizi nchini, napenda kuipongeza Serikali kupitia Tume ya Kudhibiti UKIMWI yaani *TACA/DSkwa* namna inavyopambana na kudhibiti UKIMWI na Virusi vya UKIMWI. Hili linadhihirishwa na *survey iliyo*fanywa mwaka 2013, kiwango cha maambukizi kilikuwa asilimia 5.1 ukilinganisha na *survey iliyo*fanywa mwaka 2017 kiwango hicho cha maambukizi kilishuka mpaka asilimia 4.7. Kwa hiyo, hii ni kusema kwamba maambukizi ya UKIMWI yamekuwa yakipungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hiyo ya kupungua kwa maambukizi ya UKIMWI na Virusi vya UKIMWI nchini, inachagizwa na jitihada nzuri zilizofanywa na Serikali kufikia zile 90, 90, 90. Sasa tunabakiwa na jukumu moja kubwa ya kufikia malengo tarajiwa ya mkakati wa Kitaifa kwamba mpaka kufikia mwaka 2025 tuhakikishe tumefika zile 95, 95, 95 kwa maana maana 95 ya kwanza asilimia 95 ya Watanzania tuwe tumepima virusi vya UKIMWI, lakini asilimia 95 ya Watanzania ambao wanaishi na virusi vya UKIMWI

wawe wanatumia dawa na asilimia 95 ambao wako kwenye kutumia dawa wahakikishe hawawi watoro kwenye kufuata dawa hizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaweza kuzifika hizi 95 tatu ifikapo 2025 ama hizi sifuri tatu ifikapo mwaka 2030, endapo Serikali itaendelea kujidhatiti katika masuala mazima ya kuhakikisha tunatenga bajeti kwa kutumia fedha zetu ndani. Kwa kiasi kikubwa bajeti ya UKIMWI hususan kwenye upande wa miradi ya maendeleo tumekuwa tukitegemea wahisani. Kama tutaendelea kutegemea wahisani, siku wakijitao au wafadhili wakiacha kutupatia fedha hizi ina maana lile lengo tulilolikusudia kama Taifa ifikapo 2030 tufike zile sifuri tatu itabaki kuwa historia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba katika kulidhihirisha hilli kwa namna gani tupambane kufikia 95 tatu ama kufika 0 tatu kwa kuangalia mwenendo wa bajeti hii tunayoenda nayo. Tume yetu ya Kudhibiti UKIMWI yaani *TACA/DS* kwenye bajeti hii tunayoenda nayo iliidhinishiwa shilingi bilioni 4.9, kama fedha za miradi ya maendeleo ambapo shilingi bilioni 1 ndiyo fedha ndani, zilizobaki ukitoa katika bilioni 4.9 ni fedha kutoka kwa wa hisani. Nini tafsiri yake? Asilimia 76.6 ya fedha ya masuala ya UKIMWI zinatokana na wahisani. Fedha zinazotokana na wahisani sio vyanzo endelevu, lakini pia niseme kutenga bajeti ya masuala haya ambayo bado ni janga la Kitaifa, maambukizi ni kwa asilimia 4.1, kwa kutegemea wafadhili kama Taifa tunakuwa hatuendi sawasawa. Rai yangu kwa Serikali tujitahidi tuhakikishe kwamba asilimia 75 ya fedha za miradi ya maendeleo katika masuala mazima ya UKIMWI yatokane na fedha zetu za ndani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa pengine niishauri Serikali, tunazo taasisi, *NGO* lakini pia tunazo zile Asasi ambazo kimsingi ziko chini ya *TACA/DS* au ambazo zinaangaliwa na *TACA/DS* hasahasa zile zinazopewa *technical supports* na *TACA/DS*, Serikali sasa wakati umefika wa kuangalia namna bora ili taasisi hizi kuititia maandiko yao watenge sehemu ya mchango angalau *percent* fulani ili iweze kuingia kwenye

Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI. Tukifanya hivi, tutakuwa tumepesta chanzo endelevu katika kutafuta afua hizi za UKIMWI. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikigeukia upande wa Mfuko huu wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (*Aids Trust Fund*) ambao wenyewe umetengewa shilingi bilioni 1. Pesa hizi ni za juzi juzi tu kwa msaada wa Mheshimiwa Spika baada ya kuitisha Kamati ya Uongozi na Kamati yetu ya Masuala ya UKIMWI kulibeba jambo hili kama jambo mahsusini ndipo Serikali ambapo mmetoa shilingi milioni 500. Kwa hiyo, nachopenda kuishauri Serikali tutoe hizi fedha kwa wakati. Hizi shilingi milioni hizi 500 mlizozitoa ambazo ni nusu ya bajeti, napenda sana kuiomba na kuisisitiza Serikali mpaka kufika Juni, 2021 mhakikishe mmemaliza sehemu iliyobaki ili afua za UKIMWI ziweze kupatikana kwa unafuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa mwisho nitajielekeza kwenye masuala ya madawa ya kulevyta. Tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevyta, Mamlaka imekuwa haitengewi fedha za miradi ya maendeleo. Kama hatutatenga fedha za miradi ya maendeleo, changamoto ya kwanza ni ile iliyosemwa na Kamati kwamba tutakuwa ubaha wa Vituo vya Waraibu wa Madawa ya Kulevyta ambao wanapatiwa ile dawa ya *methadone*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taifa tunapambana na pia kuitia wadhamini ama wafadhili wanaotusaidia kupambana na masuala ya UKIMWI pamoja na madawa ya kulevyta, tunahangaika kuwasaidia vijana wetu kuwapatia afua za UKIMWI na *methadone* ili watoke kwenye ule *uzombi* warudi katika hali ya kawaida, lakini hatuna miradi ya maendeleo. Wanaporudi katika hali yao ya kawaida, tukikosa kuwajengea uwezo, wakikosa shughuli za kufanya, *it's obvious* watarudia tena kule kwenye kuvuta haya madawa ya kulevyta. Ndiyo maana tunaitaka Serikali kutenga miradi ya maendeleo ili kuweza kusadia kundi hili na hususan wengi wake ni vijana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunafanya ziara ya ukaguzi wa miradi, tumetembelea hizi *sober house*, unakutana na wale waraibu wa madawa ya kulevyia, ambao tayari wameshapewa dawa ile ya *methadone* wamerudi kwenye hali ya kawaida, wanasema wakirudi mtaani hawana cha kufanya, wakienda kwenye familia wananyanyapaliwa, kwa hiyo wanajikuta wanarejea tena kwenye uvutaji wa madawa ya kulevyia. Kwa hiyo, nachopenda kukisisitiza hapa, tutenge fedha za miradi ya maendeleo ili tuweze kuokoa nguvu kazi ya vijana wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja, nakushukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shanif atachangia kwa dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Abdallah Chikota ajiandae.

**MHE. SHANIF M. JAMAL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana umenipa nafasi na mimi nichangie hoja ilio mbele yetu. Kwanza kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema niweze kusimama kwenye Bunge lako Tukufu nichangie hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nitoe pole kwa Mama Janet Magufuli, watoto, familia na Watanzania wote ambao tumepeata msiba mkubwa wa kuondokewa na Rais wetu wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Kamati yake ya Mazishi kwa kutenda haki kumpa heshima zote ambazo Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli alilikuwa anastahili, tangu siku ilipotangazwa...

## TAARIFA

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mansoor, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nafikiri wote tunajua kwamba tumepewa dakika chache, dakika tano, dakika saba. iti chako kilishatoa mwongozo kwamba kutoa pole na pongezi tushafanya kama Bunge hapa ndani wasifanye *repetition*. Sasa kama Mbunge anaona dakika ni nyangi kwake atupunguzie wengine walau tuweze kuchangia kwa manufaa ya Taifa hili. Ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni kweli, niliwasomea Kanuni hapa, nadhani ni Kanuni ya 175, naomba tuipitie Kanuni hiyo inasema nini kwa sababu wakati ule nilieleza kwa kirefu, Mbunge ambaye anaanza moja kwa moja kwenye hoja tunaweza kipeleka ujumbe huko nje kama hajali hivi ama ye ye hataki kutoa pongezi au hataki kutoa pole lakini huyo ndiye atakayekuwa anafuata Kanuni zetu zinavyosema. Kwa hiyo, tukitaka kuzungumza hayo tutafute hoja ambayo hayo tunaweza kuyasema kwa namna tofauti kuliko kuzisema moja kwa moja kwa sababu Kanuni tuliyotunga wenyewe hii hapa 175 inatutaka tufuate utaratibu huo. Karibu umalizie mchango wako Mheshimiwa Shanif Jamal.

**MHE. SHANIF M. JAMAL:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naongea kwa niaba ya wananchi wa Kwimba na hapa ndiyo sehemu ya kusema pole kwa wanafamilia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shanif tuelewanie vizuri, humu ndani kila mtu ni mwakilishi wa watu fulani lakini Kanuni tulizozitunga zinasema hivyo, kwa hiyo tufufate tu Kanuni , endelea na hoja yako. (*Makofii*)

**MHE. SHANIF M. JAMAL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee na hoja kwamba siku ya msiba wakati mazishi yalikuwa yanafanyika Kitaifa Dodoma, nakata Bunge hili litambue kwamba watu takribani bilioni 4 walikuwa wanafuatilia kwenye runinga mbalimbali mazishi ya Rais wetu

Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Maana yake ni kwamba Rais wetu alikuwa anapendwa na watu wengi sana ulimwenguni, ni Rais wa kipekee, ni Rais wa mfano. Kwa hiyo, mimi nimeona ni vema niseme hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wananchi wa Jimbo la Kwimba tunamshukuru sana Rais wa Awamu ya Tano kwa mambo makubwa mengi ambayo amewafanya wananchi wa Tanzania. Niseme machache tu, la kwanza ametupa elimu bila malipo, wananchi wa Kwimba tunamshukuru sana, watoto wetu wanakwenda shule mpaka sekondari bila malipo. La pili, nataka nishukuru *SGR* inayojengwa itapita kwenye Wilaya ya Kwimba, italeta uchumi kwenye maeneo yetu, mambo ni mengi ametufanya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano. Pia ametoa heshima kwa Machinga, wafanyabiashara wadogo wadogo miaka hii mitano hawasumbuliwi, hawakimbiziwi wana heshima. Hii heshima yote ametuletea Rais wetu wa Awamu ya Tano. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuapishwa kwa Mujibu wa Katiba kuwa Rais wetu wa Awamu ya Sita. Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan ametoa hotuba mbalimbali za maelekezo. Hotuba aliyotoa siku ya kuapishwa Mawaziri aliongea takriban dakika 87 na kuendelea, alikuwa anatoa maelekezo kwa kila Wizara, hiyo ilikuwa ni hotuba ya darasa. Naomba hotuba hiyo ingeletwa hapa Bungeni ikatusaidia wakati tunachangia Wizara ili tuendane na maelekezo ambayo Rais wetu mama Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ametoa kwa Wizara mbalimbali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kuongea kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naomba niseme mambo machache. La kwanza, Jimbo la Kwimba tumekuwa na miradi mingi ya maji ambayo imetekelezwa na imeshamalizika, lakini tatizo kubwa tullilonalo, tumejengewa tenki la lita milioni mbili la maji ambalo linategemewa maji yatoke Ziwa Victoria yapande juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo letu ni kwamba bomba linaloleta maji kwenye hilo tenki limeharibika siku nyingi, leo ni takribani miezi sita. Tenki limekamilika la lita milioni mbili ili litoe huduma kwa wananchi wa Mji wa Ngudu na maeneo mengine, leo maji hayajafika, wananchi wa Jimbo la Kwimba wanateseka kwa maji, kwa sababu ya bomba hilo limeharibika. *KASHWASA*, wameshapeleka maombi kwenye Wizara ya Maji kuomba wasaidiwe ili waweze kukamilisha. Nina imani na Mheshimiwa Waziri Aweso, kilio chetu ameshakisikia, tunaomba atusaidie wananchi wa Kwimba wapate maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la barabara. Tuna barabara ya lami ya Hungumarwa - Ngudu - Magu, sasa ni miaka mitano barabara yetu tayari imeshafanyiwa upembuzi yakinifu, lakini hatujui lini Wizara ya Ujenzi itatangaza hiyo barabara. Tunaomba tupate mwelekeo, Wizara ya Ujenzi ituambie lini itatangaza?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Oran Manase Njeza, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Chikota na atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate ajiandaye.

Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bilakwate, kama muda wetu utaturuhusu, tutamalizia na Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja iliyoko mezani kwetu. Nami nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mawasilisho ya hotuba yake; pili, nimpongeze Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri alioianza, lakini na ahadi yake ya kuyaenzi maono ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza katika Sekta ya Kilimo na nitaanza na kuchangia kuhusu zao la Korosho. Tangu mwaka 2004 - 2017 tumeshuhudia ongezeko la uzalishaji wa Korosho na hii ilitokana na uwekezaji mkubwa ambao Serikali iliweka kwenye zao la Korosho. Kwa sababu mwaka 2004 tulikuwa na tani 72,000 na mwaka 2017 tulifikisha tani 313,000 za Korosho. Kwa hiyo, kulikuwa na uwekezaji mkubwa na ndiyo maana tukafanikiwa kwa kiasi hicho. Kuanzia mwaka 2018 kuna kushuka kwa uzalishaji wa Korosho na hii ni kwa sababu tulipunguza fedha katika Sekta ya Korosho. Nachukua nafasi hii sasa kuipongeza Wizara ya Kilimo, hususan Waziri na ndugu yangu Mheshimiwa Bashe kwa jitihada ambazo wanazichukua sasa hivi kuhakikisha pembejeo za uhakika zinapatikana kwa wakulima ili uzalishaji uanze kuongezeka. Hongereni sana Wizara ya Kilimo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nizungumzie kuhusu Soko la Korosho. Ukurasa wa 30 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameweka kinagaubaga kwamba ushirika utaendelezwa na vile vile mauzo kwa mazao ya kimkakati utaendelea kuwa chini ya minada chini ya mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Naiomba Wizara kurekebisha dosari chache zilizopo. Mfumo huu umeleta mafanikio makubwa sana kwenye zao la Korosho, naomba tuulinde ili wakulima wetu wanufaika na Korosho ambazo wanazalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo suala la *TMX* kwa sasa hivi kwa sababu tumeona kuna upungufu ambao umeanza kujitokeza, ni kama alivyowasilisha Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa, litumike katika kutafuta masoko ya nje, lakini soko la ndani tuendelee na mfumo wetu wa Stakabadhi Ghalani, kwa sababu *TMX* imeonekana bado ina changamoto ambazo hazijapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nijielekeze kwenye suala la miundombinu. Ukurasa wa 30 unaelezea vile vile suala la miundombinu, nami nijielekeze katika matumizi ya Bandari yetu ya Mtwara. Kuna uwekezaji mkubwa sana umefanywa katika Bandari ya Mtwara, zaidi ya shlingi bilioni 57 zimebekwa pale; na sasa hivi Bandari yetu ya Mtwara ina uwezo wa

kupokea tani milioni moja. Naomba ule mradi wa kujenga reli kutoka Mtwara Mbambabay sasa uanze kutekelezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mradi wa Mchuchuma na Liganga sasa uanze ili bandari hii iweze kutumika ipasavyo. Sasa hivi tunasema Bandari ya Mtwara haitumiki kwa sababu Mradi wa Mchuchuma na Liganga bado hatujautekeleza, lakini tukiutekeleza mradi huu Bandari yetu ya Mtwara itakuwa *effective*. Kwa hiyo, muda umefika sasa, tutekeleze Mradi wa Mchuchuma na Liganga na pia tujengeta reli kutoka Mtwara kwenda Mbambabay. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nzungumzie suala la maji. Juzi hapa niliuliza swali kuhusu Wizara au Serikali imejipangaje kutumia maji ya Mto Ruvuma kwa ajili ya kutatua changamoto za maji zillizopo katika Mikoa ya Mtwara? Kama tumeweza kuthubutu kutekeleza kutoa maji kutoka Ziwa Victoria mpaka sasa tunafikisha mpaka Nzega, ni matarajio yangu sasa tutaanza kutumia maji ya Mto Ruvuma ili kujenga miradi mikubwa kwa ajili ya Mtwara Mjini, Lindi, Masasi, Tunduru hadi Songea. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muda muafaka sasa wa kuhakikisha kwamba, maji haya ya Mto Ruvuma yanatumika kutatua changamoto za maji iliyopo katika miji yetu ya Kusini ili kuhakikisha tunatekeleza llani ya Chama chetu ambayo inasema ifikapo 2025, basi vijijini tuwe tumepeleka maji kwa asilimia 85. Kwa Mkao wetu wa Mtwara hali bado ni tete kwa sababu tumefikisha asilimia 60 tu. Tutazipata asilimia 25 zillizobaki tukianza kutumia maji ya Mto Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Maji kwa sababu wameshatuhakikishia kwamba Bajeti ya mwaka huu wataanza kutumia maji ya Mto Ruvuma, kwa ajili ya kutatua changamoto za maji katika Mkao wa Mtwara na maeneo ya jirani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa suala la mabadiliko katika Sekta ya Elimu. Kuna mjadala mkubwa

unaendelea sasa hivi kuhusu elimu yetu. Naiomba Wizara ya Elimu ikubali hicho kilio cha Watanzania. Kwa kweli elimu yetu sasa hivi inahitaji mabadiliko makubwa. Kuanzia elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vikuu. Hakuna mtu ambaye anabisha sasa hivi, kwa sababu falsafa yetu ya elimu ni Elimu ya Kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko zamani ilikuwa mtoto wa Shule ya Msingi akimaliza anaweza kutumia maarifa yale kuishi katika mazingira yake. Sasa hivi tumebadilisha Elimu yetu ya Msingi inamwandaan mtoto kuingia sekondari. Tumeapotoka, tufanye kila kiwango cha elimu kuwa kinajitosheleza. Elimu ya msingi ijitosheleze, Elimu ya Sekondari ijitosheleze na Elimu ya Chuo Kikuu iwe kamili, ijitosheleze. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivyo, hakutakuwa na malalamiko kwamba *graduates* wetu wakifika mitaani, wakifika mahali pa kazi, wanapwaya, hawatakuwa na maarifa ambayo yanasaidia katika kuzalisha katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Seba Bilakwate, tutamalizia na Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa afya na nguvu kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kabla sijaanza kuchangia, kipekee nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya. Ni ukweli usiopingika, kazi kubwa zilizofanywa na Awamu ya Tano huwezi ukamweka pemberi Makamu wa Rais ambaye leo hii ni Rais wetu na pia na Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nakushukuru kwa ziara yako uliyoifanya Wilaya ya Kyerwa ambayo mimi kama Mbunge nimeanza kuona matunda yake. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru sana. Kabla sijaanza kuchangia, nikukumbushe ahadi ambazo tulikueleza na wewe ukaahidi. Mheshimiwa Waziri Mkuu ulipokuja, kabla hujafika kwenye Kituo cha Mkutano, ulipita Kata ya Nkwenda. Pale Nkwenda kuna upungufu wa kukamilisha jengo la mama na mtoto, nawe uliahidi ukiwa pale kwenye Kata ya Nkwenda, kuwa jengo hili litakamilishwa na ukaahidi pia kuongeza Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine Mheshimiwa Waziri Mkuu, ulipopita kwenye barabara ya Murushaka kwenda mpaka Mulongo ulijionea na wewe mwenyewe ukaahidi barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami. Nashukuru kaazi imeanza. Mheshimiwa Hayati Rais Dkt. John Pombe Magufuli alipofika, aliahidi kilometra 50. Nimpe majibu dada yangu aliyekuwa anasema kuna sintofahamu; hakuna sintofahamu yoyote, barabara inajengwa kuanzia Rubwera kwenda Karagwe. Kwa hiyo, hilo nimpe majibu. Jambo lingine ukitaka kuuliza, mwulize mwenye nyumba, anaweza akakupa majibu kuliko kumwuliza mpangaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni upande wa maji. Nashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja, tulimweleza changamoto tunayoipata kwenye maji na ninaishukuru Serikali kwa jitihada ambazo zinaendelea. Kwa kweli kwa sasa hivi tuna hatua nzuri. Tumeshakutana na Waziri na Katibu Mkuu; kwa kweli mimi kama Mbunge naridhika na ninawaahidi wananchi wa Jimbo la Kyerwa kuwa nimejipanga vizuri pamoja na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuwapelekea majisafi na salama. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la umeme Mkoa wa Kagera. Kwa kweli tunayo changamoto kubwa kwenye Mkoa wa Kagera. Umeme wetu ni umeme ambao kwa kweli hautabiriki, unaweza ukawaka asubuhi, saa nne umezimika, saa sita unawaka. Kwa hiyo, naiomba sana

Serikali hili suala la umeme Mkoa wa Kagera lipatiwe majibu.  
*(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la kilimo. Tumekuwa tukiongea sana hapa kuhusiana na kilimo, lakini mimi niseme zipo jitihada ambazo kwa kweli bado hazijaridhisha. Ni jambo ambalo linasikitisha, ukiangalia nchi nydingine ambazo zimeendelea na nchi hizi hazina mvua ya kutosha, lakini ukija kwetu tuna mvua nydingi, Mungu ametujaalia ardhii yenyeye rutuba, lakini hatujaona hii neema ambayo tunayo ni namna gani tunaweza kuitumia.

Naiomba sana Wizara ya Kilimo, tujikite kwenye kufanya utafiti, ni kitu gani ambacho tunahitaji kukifanya ili kilimo chetu kiwe na tija? Vinginevyo tutakuwa hapa tunaimba bila kuwa na majibu ambayo ni sahihi. Kilimo ni afya, killmo ni uhai, killmo ni blashara na killmo ni viwanda. Leo hii tunasema tumeanzisha viwanda, viwanda viko vingi zaidi ya 8,000, lakini hivi viwanda vinahitaji malighafi. Tutaenda kutafuta malighafi nje wakati tungeweza kuzalisha kwetu na neema ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwenye mazao ya kimkakati. Mazao haya hayajapewa kipaumbele. Pamoja na kusema haya mazao tumeyatenga kimkakati, lakini mimi niseme bado hayajapewa kipaumbele. Kwa mfano, kwenye zao la Kahawa; pamoja na kulima hili zao, bado hatuna soko la uhakika. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara tujikite kutafuta masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeondoa biashara ya butura na mimi kama Mbunge ninajua biashara hii ilikuwa inawanyonya wakulima. Ni mkakati upi ambao tumekuja nao kama Serikali? Huyu mkulima anapolima kabla hajaenda kuvuna kupeleka hii Kahawa kwenye soko, anapataje pesa ya kumsaidia ili aweze kuhudumia hii Kahawa? Tunasubiri mwishoni ndiyo tunakuja kwa mkulima na huyu mkulima hatujamsaidia mwanzo. Kwa hiyo, naomba sana tutafute masoko. Wizara tokeni mkatafute masoko. Naomba hili tuliangalie. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ili kilimo chetu kiende vizuri, lazima tuboreshe miundombinu ya barabara. Barabara zetu ambapo huku kwa mkulima ndio kuna mزالىشاجى siyo nzuri, hali ni mbaya. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iboreshe barabara za *TARURA* ambako huku ndiyo kuna mزالىشاجى mkubwa. Kwa hiyo, naomba sana hili tuliangalie ili tuweze kumsaidia mkulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo nilisemee...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Nakushukuru. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Shukrani sana. Mheshimiwa Athuman Almas Maige.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru sana kuniruhusu kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu yenye mambo ya Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumpenda sana Marehemu Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na kumchukua. Mungu aiweke roho ya Marehemu Magufuli mahali pema peponi.

**WABUNGE FULANI:** Amen.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, leo ni siku ya 29 tangu ametutoka na kumpoteza mpendwa wetu huyu. Kwa hiyo, msiba huu kwetu sisi bado ni mbichi. Kwa mila zetu za Kitanzania ni mwiko au *taboo* kumwongelea Marehemu kwa mabaya, bali kumwombea ili Mungu

ampokee na aiweke roho yake mahali pema Peponi.  
*(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami niendelee kukemea wale watu wenye hulka ya kubadilika kama kinyonga, waache kumsema kwa mabaya Marehemu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, bali waendelee kumwombea na waone aibu na wamwogope Mungu. Kwangu mimi, Marehemu Rais Mheshimiwa Dkt. Magufuli anaishi bado kwa alama kubwa alizotuvekea ambayo ni pamoja na reli, vituo vya afya, bwawa la umeme, hospitali, barabara, ndege, kuhamia Dodoma, madaraja, vituo vya VETA, elimu bure na miradi mengine mingi kama maji na kadhalika. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, alama hizi zote sasa ziko mikononi kwa Mama shupavu, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. Tunamwomba Mungu ampe nguvu mama huyu, achukue jahazi hili na kulibeba kama ambavyo walilibeba wakiwa na Marehemu Mheshimiwa Dkt. Magufuli. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hotuba ya Waziri Mkuu, ametaja mambo mengi, lakini mimi nijikite kwenye sekte binafsi ambayo ina sheria za kazi. Sheria hizi zilizopo katika matumizi kwa sasa zimepitwa na wakati. Kwa mfano, Baraza la Usuluhishi la *RESCO* halijakutana kwa muda mrefu sana na hili ndiyo lingekuwa nafasi ya kujadili matatizo ya waajiri na wafanyakazi. Tungependa Ofisi ya Waziri Mkuu inayohusika na sera na kazi na ajira iziboreshe sheria hizi. Kwa mfano, sasa hivi tulipata tatizo kubwa sana tulipozuiwa mambo ya *Covid*; waajiri walipata taabu sana kuendelea kulipa mishahara kama tungelifunga hata pale ambapo wafanyakazi hawafanyi kazi. Sheria za sasa zingeweza kuchukua nafasi hiyo na kulisahihisha tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la umeme wa *REA* ambapo viji vyote vya Tanzania vitakuwa na umeme ifikapo mwaka 2022/2025 lakini pia umeme huo utakuwa na matumizi makubwa, kwa hiyo, kuna umuhimu wa kulipa nguvu wazo au mradi ule wa Bwawa la Nyerere likamilike ili kuleta umeme

katika maeneo ambayo yatapatiwa umeme wa REA.  
*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la reli ya *SGR* ukurasa wa 50, kuna mtu amesema mradi huo utakamilika mwaka 2102, yaani miaka 81 kuanzia leo. Nimemshangaa sana kwa sababu, kanuni za miradi ni kuwa na tarehe ya kuanza na tarehe ya kumalizia. Kwa hiyo, miradi yote ya reli hii ya *SGR* inajengwa kwa awamu na vipande kutoka Dar es Salaam – Morogoro na Morogoro - Dodoma na baadaye Mwanza - Isaka na miradi hii yote ina tarehe ya kuanza na kwisha...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, haitafika muda mrefu huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maige, kuna kanuni inavunjwa. Mheshimiwa Halima Mdee.

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 67(8), Mbunge hatasoma maelezo isipokuwa kwa madhumuni ya kutilia nguvu maelezo yake, anaweza kusoma dondoo kutoka kwenye kumbukumbu zilizoandikwa au kuchapishwa na anaweza pia kujikumbusha kwa kuangalia kwenye kumbukumbu alizozianidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa mkongwe mwenzangu nimekuwa namvumilia, naona anasoma tu, sasa naomba umshauri mkongwe *a-note* tu, halafu atiririke. Kwa hiyo, naona hii Kanuni inavunjwa. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige nadhani ulikuwa unakumbushwa. Unajua pale hasomi maelezo anayosema, isipokuwa ameamua kuinamia kwenye *mic* yake. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Maige, hicho kisemeo hata ukitazama pembedi kinashika mawimbi, kwa hiyo, usiwe na wasiwasi. Karibu umalizie mchango wako. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mkongwe mwenzangu nakushukuru sana, lakini sikuwa nasoma, maana nilikuwa nimefanya *notification*, lakini mambo niliyoyaongea kabla ya kuanza kuongea haya, nilifikiri kwamba ningepotea. Nimeongea mambo mazito ndiyo maana ikanilazimu niwe na kumbukumbu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, afya. Jimbo la Tabora Kaskazini lina Kata 19 na Kituo kimoja tu cha Afya. Mimi nafikiria kwamba ipo haja ya Serikali kufikiria Jimbo la Tabora Kaskazini ambalo lina Kituo cha Afya kimoja tu, liweze kupata vituo vingine na hasa kusaldia vituo ambavyo vimejengwa kwa nguvu ya wananchi katika Kata ya Mabama, Kata ya Usagari na Kata ya Shitaghe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu kwa sehemu ya kwanza kwa siku ya leo. Nitasoma majina machache tutakaoanza nao kuchangia mchana.

Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Mohamed Monni, Mheshimiwa Vincent Mbogo, Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan, Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Grace Tendega na Mheshimiwa Shamsia Mtamba. Wengine tutaendelea kuwasoma kadri tutakavyokuwa tunaendelea na uchangiaji wetu.

Waheshimiwa Wabunge, ratiba imebadilika kuanzia leo. Kwa hiyo, nitakapokuwa nasema hapa msije mkahisi kama tumekosea muda hivi, lakini siku ya leo ndiyo tutakayoanza kukutana saa 10.00.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 alasiri leo.

*(Saa 7.04 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00Jioni Bunge Lilitrudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Oran Njeza atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Hasunga na Mheshimiwa Mohamed Moni ajiandae.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa hii ya kuchangia bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa kuanzia kabisa naomba kwa kipekee nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu mama Samia Hassan Suluhu kwa kushika nafasi ya Urais. Ameanza vizuri na wote tumeona.

Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Mpango naye kwa kuteuliwa na kushika nafasi ya Makamu wa Rais. Naye kwa kweli tumeona ameanza vizuri sana na kweli timu imekamilika. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda nimpongeze Waziri Mkuu. Kwa kweli Waziri Mkuu amefanya kazi kubwa sana. Ofisi yake inafanya kazi ya *coordination* ya Wizara zote, kwa hiyo mafanikio ambayo tumeyapata katika Serikali yetu ya Awamu ya Tano na yanayoendelea mpaka sasa hivi yote ni juhudhi ya ofisi yake ambayo imeweza kuzi-*coordinate* Wizara zote na Serikali kwa ujumla. Wote ni mashuhuda wa mikakati ambayo tunayo mpaka sasa hivi ambayo ni endelevu. Pamoja na mafanikio yaliyoko kwenye miradi ya mkakati, lakini hata huko chini kwenye Halmashauri zetu tumeona mafanikio makubwa mno. Kwenye maji, kwenye umeme hata kwenye miundombinu tumeona mafanikio makubwa mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye jimbo langu tumeona mafanikio makubwa ya ujenzi wa hospitali, vituo vya afya vitatu ambavyo ni vya kihistoria na sasa hivi tunakamilisha tu ili viweze kuanza kufanya kazi vizuri. Kwenye miundombinu vile vile kwa mara ya kwanza kwenye historia tumeona barabara za kiwango cha lami zikianza kujengwa vijiji kwa ajili ya kwenda maeneo mahsus ya wakulima wetu ili kuweza kufanya miundombinu ya vijiji iwe rahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye umeme nako tumefanya vizuri sana. Kwenye Halmashauri yangu tulikuwa na vijiji vingi sana, vijiji karibu 200 lakini sasa hivi ndiyo Serikali inamalizia vijiji 40 vya mwisho ili tuweze kufikia asilimia mia moja ya vijiji vyote kuwa na umeme. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo hapawezi kukosa changamoto, lakini changamoto zetu tulizonazo naona suluhisho lipo na tunategemea sana Serikali ya mama yetu Samia Suluhu Hassan. Ataweza kuzikabili hizo changamoto, sio kubwa kiasi hicho, ni ndogo na ukiangalia mpango wetu ambao tumeupitisha sasa hivi ni mpango ambao ni mzuri, unaangalia Taifa letu la Tanzania ni namna gani litakuwa shindani kwenye ukanda wetu lakini vile vile na kidunia. Kwa hiyo, kikubwa hapo ni kuangalia miundombinu ambayo itatufanya sisi tuwe washindani, tuweze kufanya vizuri ukitulinganisha na wenzetu huko duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ambazo tunaziona hasa kwa sisi tunaotoka majimbo ya vijiji ni miundombinu ya barabara. Barabara za vijiji ambazo zinahudumiwa na TARURA kwa kweli kwa asilimia kubwa zina hali mbaya sana. Tukiongelea kilimo bila ya kuwa na miundombinu mizuri ya barabara hatuwezi kufanikiwa kwa sababu gharama ya pembejeo itakuwa kubwa, tutashindwa kushindana. Lakini mazao yetu yatashindwa kwenda sokoni. Kwenye halmashauri yangu nina kilometa zaidi ya 1,000 ambazo zinahudumiwa na TARURA, lakini leo hii zaidi ya asilimia 90 hazipitiki. Wakulima wanashindwa kupeleka mazao yao sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hilo tu, vile vile hata halmashauri haiwezi kukusanya kwa sababu halmashauri yetu ambayo inakusanya karibu bilioni tatu kwa mwaka kutokana na mazao ya kilimo kwa miezi yote ambayo mvua zinanyesha wameshindwa kukusanya ambao ni karibu nusu mwaka. Sasa hii inaweza kutupeleka mahali pabaya sana. Tunakuja na bajeti zetu, ambazo ni nzuri kiasi hicho, lakini tunashindwa kutekeleza yale malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kulikuwa na ahadi ya Mheshimiwa Rais, hata Mheshimiwa Rais Samia naye aliahidi pale kwetu Mbeya. Kuna barabara yetu, kipande cha barabara ambacho kinasababisha sana ajali, Mlima Iwambi pale Mbalizi na wewe ni shuhuda, hatuna barabara nyagine zaidi ya hiyo, ukiachilia mbali msongamano wa pale Mbeya Mjini lakini ile barabara imeua wananchi wetu wengi. Mwaka 2018, Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli aliahidi ijengwe haraka kwa kiwango cha lami. Nina Imani hata Viongozi Wakuu wengine waliwijibika kwa ajili ya hilo. Alikuja mama, wakati huo akiwa Makamu wa Rais naye akaahidi ijengwe haraka. Mpaka leo hakuna chochote kinachofanyika, sasa ukiangalia ile barabara ndiyo inabeba mzigo wote ambao ni karibu asilimia 75 ya mizigo yote inayotoka bandarini kwa ajili ya majirani zetu na hiyo barabara inapita katikati ya Jiji. Kunapita na ma-tankerya mafuta pale ambayo ni hatari kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waziri wa Ujenzi atuambie ni nini kinakwamisha hilo kwa sababu tuliambiwa mwanzoni kwamba hata wadau wetu wa maendeleo walikuwa tayari kujenga hiyo barabara ya Mlima Nyoka sehemu za Uyole kwenda Songwe, lakini mpaka leo hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara zingine pia ambazo ni za kimkakati; barabara ya Isyonje – Kikondo kwenda mpaka Makete ambayo tunategemea iweze kubeba mazao mengi sana, matunda matunda pamoja na sasa hivi kuna utalii kwa jirani zetu wale wa Makete. Hiyo barabara nayo pamoja na kuwekwa kwenye bajeti hatuoni

kinachoendelea. Kuna barabara nyingine ambayo nayo ni ya kimkakati; barabara ya Mbalizi – Galula – Makongolosi ambayo inatokea mpaka kwa majirani zetu wa Mikoa ya Tabora na Singida. Hiyo barabara imekuwepo kwenye bajeti kwa miaka mingi, lakini mpaka leo na hivi juzi juzi ilikuwa haipitiki. Kuna barabara yetu nyingine ambayo ni ya kimkakati; barabara ya Mbalizi – Shigamba ambayo nayo inaenda mpaka Isongole karibu na mpaka wetu na Malawi, hii ni barabara ya kimkakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hizi barabara zote zipewe kipaumbele ikiwemo na barabara zetu za vijijini, zina hali mbaya sana na ikiwezekana Waheshimiwa Wabunge tuangalie ni namna gani tuiwezeshe *TARURA* itusaidie ili wakulima wetu waweze kusafirisha mazao yao kutoka vijijini tuweze kupunguza gharama za mazao yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi nadhani umetilia maanani hizo barabara alizokwu anazitaja hasa barabara ya Uyole – Igawa, kilometra 113; Uyole – Tunduma, kilometra 116; Uyole – Songwe, kilometra 40. Zote ziko kwenye llani ya Chama Cha Mapinduzi. Tuko kwenye kipindi cha bajeti hiki, kwa hiyo tafadhali muisome llani jamani.

Tunaendelea na michango ya Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Japhet Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Monni na Mheshimiwa Anatropia Theonest ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana kwa kunipatia hii nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu. Jambo la kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa. Hotuba ambayo imekuwa ni pana, imekwenda kwa mapana na uwanda mpana sana.

Karibu kila kitu amekizungumza vizuri sana. Kwa kweli tunampa hongera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nchi yoyote, kiongozi yoyote anayekuwepo katika taasisi au kwenye nchi lazima awe na maono. Kuwa na maono maana yake ni kuwa na dira na dira hiyo ukiwa nayo lazima uwe na uwezo wa *ku-share* na wengine wote na wenzako waweze kuiimba hiyo dira na hao waliofanya hivyo ndiyo walioweza kufanikiwa kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baba yetu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, aliyekuwa Rais wetu alikuwa na maono makubwa, alikuwa na mtazamo na dira kubwa. Ile dira aliweza *ku-share* na wenzake na ndiyo maana nataka niseme Magufuli alikuwa akisema, wa pili mama yetu Samia Suluhu Hassan, ye ye alikuwa anaenda kutekeleza na kufuatilia utekelezaji. Msimamizi wa Serikali, Kassim Majaliwa Majaliwa ye ye ana wahi *site*, ikishasemwa tu anawahi kwenye utekelezaji na ninayo mifano michache ninayoweza kusema.

Nakumbuka wakati ule hayati Dkt. Magufuli aliposema atahakikisha Serikali yake inahamia Dodoma, alipotamka tu ile neno niliona wale viongozi walivyotekeliza yale maono. Wa kwanza alikuwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu, akasema ndani ya miezi mitatu nahamia Dodoma na kweli akafanya hivyo. Makamu wa Rais kahamia Dodoma maana yake ile dira ilikuwa *shared*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, alipotamka kwamba tunatakiwa tujenge bwawa kubwa la kuzalisha umeme, walichokifanya nilimwona Waziri Mkuu ameenda *site* kwenda kuangalia mahali ambapo daraja litajengwa. Ukiangalia Makamu wa Rais ameenda huko, kwa hiyo mambo yote walikuwa wana-*share* na ndiyo maana hatuna wasiwasi na miradi yote ambayo imeanzishwa katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano kwamba yote itatekelezwa vizuri kwa sababu viongozi waliokuwa wanayaimbwa hayo ndiyo hao ambaobado wako madarakani. Kwa hiyo hatuna wasiwasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichukue nafasi hii kuwapongeza. Kuna watu wana wasiwaso kwamba mradi wa *SGR*, eti hautakamilika, nani anasema? Ule mradi ni wa muhimu, reli ya *Standard Gauge* alianzisha Dkt. Magufuli, viongozi wetu wakatufundisha, Bunge likapitisha fedha, leo hii usikamilike, tutakuwa kwa kweli hatujaitendea haki nchi hii. Mradi wa Bwawa la kuzalisha umeme la Nyerere, walipolisema tulipitisha hapa Bungeni, lile bwawa lazima likamilike na litaleta maendeleo makubwa katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hiyo tu, barabara nydingi zimejengwa za juu, za chini; madaraja tumeona, viwanja vyatia ndege vimejengwa, ndege zimenunuliwa, nani leo hii anaweza akaiambia hii nchi kama wewe hujawezu kupanda hata hiyo ndege una tatizo lako binafsi, lakini ndege zipo. Hizi zote ndiyo zimebeba uchumi wa nchi yetu. Hawakuishia hapo, wameenda kwenye afya, elimu, maji na kadhalika. Tumeenda mpaka kwenye kujitosheleza kwa chakula. Nchi hii tulikuwa hatujitoshelezi kwa chakula, alipoingia Hayati Dkt. Magufuli akasema kokote kutakakokuwa na njaa, huyo Mkuu wa Mkoa na Wilaya watanikoma na kweli hatujawahi kupata njaa mpaka sasa hivi na ndiyo maana uzalishaji uko wa kutosha. Wananchi sasa hivi wanacholalamikia ni soko, wapi wauze mazao yao. Hilo ndiyo limekuwepo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninachotaka kusema walifanya kazi kubwa, alifanya kazi nzuri na mimi nasema tutaendelea. Miradi ya maji pale Vwawa alitoa fedha mradi wa maji, maji pale bado pana tatizo. Fedha zimekwenda, mradi umetekelozwa lakini maji bado hayatoki. Tuliahidi kwamba hospitali ya rufaa itajengwa pale Vwawa, Ilembo, imeletwa fedha imejengwa ilitakiwa ianze mwezi Novemba mpaka sasa hivi haijaanza. Naomba watendaji waende wakashughulikie hayo kwa sababu ni ahadi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Sasanda kulikuwa na kambi ya kuendeleza vijana. Kambi ile ni muhimu ikaendelezwa ili vijana wa nchi hii waende sasa wakajfunze

maarifa, uzalendo na miradi mbalimbali ili waweze kuchangia katika maendeleo ya nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo soko la mazao. Mheshimiwa Rais aliyeondoka alituahidi, yote hayo lazima tuyakamilishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nilichangie ni upande wa watumishi. Mahali popote ili uweze kukamilisha kitu cha kwanza ni watumishi na zamani tulikuwa tunasema mteja ni mfalme, siku hizi mteja ni namna mbili, wa kwanza ni mtumishi. Mtumishi yule ukim-*treat* vizuri ndiyo atakayefanya hata wateja waongezeke na wapatikane na waende vizuri. Kwa hiyo basi, kwa kuwa tumetekeleza miradi mikubwa na tunaendelea kuitekeleza na ahadi na llani ya Chama Cha Mapinduzi ilikuwa ni kwamba sasa tunaingia kwenda kuhakikisha watumishi wetu wanapata maslahi mazuri ili wale ambao madaraja yalikuwa hayajapandishwa, zile *promotion* ambazo zilikuwa hazijafanyika, mishahara ambayo ilikuwa haijaongezeka, basi sasa ni kipindi naiomba Serikali yetu sasa iwatazame hawa watumishi wa Serikali waweze kuongezewa ili waishi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hao tu, watumishi wa Sekta Binafsi. Serikali ilipanga vima vy'a chini vy'a mishahara ya Sekta Binafsi zote, vima vy'a chini vile waajiri wengi hawajavizingatia. Ningeomba ili Watanzania wawe na maisha mazuri ili wananchi wawe na maisha mazuri waweze kuchangia basi naomba Serikali ikaangalie maeneo hayo. Ninachotaka kusema, miradi mikubwa hii ya vielelezo, ndiyo imebeba uchumi. Uchumi wa nchi yetu umefika kuwa ya kipato cha katika sababu ya hii miradi ya vielelezo na miradi hii tusimame pamoja isitokee hata mmoja wetu mara anaanza kubeza, mara mwengine anaanza kusema huu mradi tuuache tutakuwa kwa kweli hatujaitendea haki nchi hii. Miradi ya umeme, umeme kule wanahitaji, una shida sana kwenye Mkoa wa Songwe. Kule vijiji vyote ambavyo havijapata vinahitaji umeme, lakini hata mahali ambapo uko bado kuna changamoto unakatikakatika. Tunaiomba Serikali

ikasimamie, ikatekeleze ahadi zake ili umeme ule upatikane. Zile barabara ambazo ziliahidiwa tulifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ninalotaka kusema ni kuhusu Mradi wa Chuma wa Liganga, huu lazima tuutekeleze. Ni mradi mpya lazima tuutekeleze, tutengetfedha, tukautekeleze huo, tukipata chuma chetu tutaweza kujenga viwanda imara, tutaweza kupata malighafi hapa hapa nchini na tukiwa na umeme wetu ndiyo maendeleo makubwa yataweza kuwepo. Bila kufanya hivyo, tutashindwa kwa kweli kuweza kufanikiwa kama nchi na kufikia yale malengo tuliojipangia kwamba ifikapo mwaka 2020 tutafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naamini kwa jinsi tulivyojipanga na kwa jinsi Bunge hilli linavyofanya kazi nzuri na kwa Watanzania ambavyo sasa tunataka kuona nchi yetu inaendelea, naamini tutaweza kufika kuwa nchi ya kipato cha katicha uwanda wa juu na hayo yanawezekana kwa kufanya kazi kama timu, kwa kushirikiana, tuondoe ubaguzi, tuondoe utengano, tuwe kitu kimoja. Mungu awabariki. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mohamed Monni, atafuatiwa na Mheshimiwa Anathropia Theonest na Mheshimiwa Vincent Mbogo ajiandae.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hotuba ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kuchangia naomba niseme maneno machache. Kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, ambaye amekuwa akitupa uhai na afya njema ya kuendelea kuwatumikia Watanzania. Pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais ameanza vizuri na tuna uhakika wa asilimia zote yale ambayo tumeahidi kwenye llani yetu ya Uchaguzi yataktekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda naomba mimi nianze kuchangia. Kwanza kabisa nataka nimpongeze sana Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri. Hotuba hii imegusa kila eneo, lakini kwangu imekuwa nzuri zaidi kwasababu ameeleza namna gani tunaenda kujenga lile Bwawa la Farkwa. Mradi huu wa Bwawa la Farkwa ndio mradi peke yake ambao unaenda kumaliza matatizo yote ya maji kwenye Jiji letu la Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na bahati nzuri mradi huu ukitekelezwa hautamaliza tu changamoto za maji kwenye Jiji la Dodoma, utamaliza pia kwenye wilaya zetu zote za Mkoa wa Dodoma. Bahati nzuri sana Waziri Mkuu mwenyewe ametembelea kwenye huu mradi na yapo maelekezo ambayo aliyatoa, lakini bahati mbaya sana kuna changamoto kwenye maelekezo mengi ambayo ameyatoa hayajatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya changamoto hizo ni kwamba, tayari Serikali ilitoa *1.8 billion* kwa ajili ya kulipa fidia ya watu wote waliokuwa kwenye maeneo yale na fidia hiyo tayari imelipwa. Wametengewa maeneo ambayo wanatakiwa waende kuishi, lakini bahati mbaya sana tumechukua shule zao, lakini kule hatujaenda kujenga shule. Wamelipwa fidia tunawaondoa, lakini wanaenda sehemu ambapo hakuna shule ya msingi, hakuna zahanati, wametengewa eneo waende, lakini miundombinu ile ya kuwafanya waishi haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri Waziri Mkuu alipofika aliwaambia msiwaondoe hawa, jengeni kwanza shule, jengeni zahanati na akaelekeza fedha zitolewe, lakini mpaka leo hii bado ni changamoto kubwa sana. tunaendelea kuwaondoa watu wahame, lakini tunawapeleka sehemu ambako watoto wao watacaa bila kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali, tuna mipango mizuri na sisi watu wa Chemba pamoja na Dodoma kwa ujumla tuna uhitaji kweli huo mradi. Na huo

mradi ndio peke yake ambao unaenda kuondoa changamoto yote ya maji kwenye maeneo yote yanayozunguka. Lakini bahati nzuri uksoma andiko la mradi ule limeeleza namna gani kwenye maeneo yale watatengeneza skimu za umwagiliaji kwa hiyo, kwa namna yoyote ile mradi ule una faida kwetu zaidi. Changamoto ni moja tu ni hiyo ambayo nimeeleza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Wizara ya Maji itoe fedha kama tulivyokubaliana kwa ajili ya ujenzi wa shule na zahanati, ili watu wale wahamie kule. Tukiendelea kwasababu, sasa hivi kuna kama kigugumizi cha watu kuondoka, watu wengine wamehamia, lakini watu wengine bado wapo. Na nikifika kule naulizwa Mheshimiwa Mbunge wanatuambia tuje hapa, watoto wetu wasoma wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kuhusu maji ni huu, lakini pia naishukuru Serikali, tuna mradi pia katika ile miradi ya miji 28 Halmashauri yetu ya Chemba ni moja ambayo inanufaika na bilioni 11 zile. Na bahati nzuri watu wale wanaotekeleza ule mradi tumefika tukafanyanao vikao tukawaomba watu wale waliokuwa wanadai fidia za watu kupisha mabomba ya maji wamekubali wanaondoka na hawahitaji fidia. Niiombe sasa Serikali ifanye haraka kwa ajili ya kutekeleza ule mradi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niongee kidogo kuhusu kilimo. Sisi sote tulipo hapa tunafahamu asilimia 77 ya ajira za Watanzania zinapatikana kwenye kilimo, lakini si hivyo tu, tunafahamu asilimia 90 ya ardhi iliyopo Tanzania hii inalimwa na wakulima wadogowadogo. Sasa ni mawazo ya kawaida tungefikiria kwamba, huku ambako watu waliko wengi ndiko tuingize fedha nyingi kwa ajili ya matokeo makubwa, lakini ukweli ni kwamba, bajeti ya Wizara ya kilimo ni ndogo sana na hii ni changamoto kubwa sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe sana kuwa tuangalie namna sehemu ambako tunatakiwa kuwekeza ni sehemu ambako idadi ya wanaochangia uchumi ni kubwa.

Idadi ambayo ya waliojiajiri ni kubwa, ili tuweze kutatua changamoto na kwasababu hiyo, tunaweza tukaongeza pato la Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hivyo kuna changamoto kubwa sana kwa wakulima wangu. Moja ya changamoto kubwa ni kile kitu kinachoitwa stakabadhi ghalani. Serikali ina dhamira njema kwelikweli, lakini changamoto iliyopo unawalazimisha watu mpaka kwa bunduki ili wakauze huko kwenye stakabadhi ghalani, sijui ni nini? Unalima mwenyewe, unavuna mwenyewe, unapalilia mwenyewe, Serikali hujapeleka hata mbegu, unashika bunduki ili mtu akauze kwenye stakabadhi ghalani? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linaleta kero kubwa sana, kule kwangu sasahivi wameanza kuvuna. Nilikuwa na mkutano *weekend* hili wameanza kuniulliza tumeambiwa tena tuanze kupeleka mazao kule; hivi kweli kama hiyo stakabadhi ghalani ina faida kwa wananchi kwa nini wao wasihamasike kwenda kuuza huko? Unamlazimisha mtu mwenye debe moja aende akasubiri mwezi mzima ndio aje alipwe fedha yake? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hili haliwezi kuwa sawa, nashauri Serikali kwa baadhi ya maeneo au kwa baadhi ya mazao waachane na huu utaratibu kwa sababu kwa namna yoyote ile ungekuwa na faida wakulima wenyewe wasingeukataa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongee kidogo kuhusu barabara, kuna barabara yetu ambayo na Mheshimiwa Rais, Hayati, alivyofika kwenye Jimbo langu la Chemba aliahidi. Barabara inatoka Kibarashi inaunganishwa mikoa minne, Kibarashi – Kiteto – Chemba hadi Singida. Barabara hii kwenye llani imekuwa ikiandikwa mara zote, lakini hakuna hata mwaka mmoja ambaeo imetengewa fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwasababu ya hayo naomba kuwakilisha. Naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Theonest, atafuatiwa na Mheshimiwa Vincent Mbogo. Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan ajlandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mchango wangu utajikita katika sekta binafsi ambavyo zimechangia katika uchumi au katika pato la Taifa. Ukiangalia tathmini ya mpango wa pili wa miaka mitano unaokwisha imeeleza bayana kwamba, sekta binafsi haijafanya vizuri kwamba, mchango wako ni chini ya asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninataka nioneshe masikitiko yangu kwasababu sisi leo sio nchi tena ya ujamaa kwa hiyo, tunahitaji sekta binafsi iweze kuchangia, ili tuweze kuona mabadiliko katika uchumi wa nchi hii. Na uklongelea sekta binafsi ni pana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiongelea leo, wengi wakisimama hapa wanaongelea kilimo...

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** ...kama kilimo kinafanya vizuri, kilimo ni sekta binafsi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Charles Mwijage.

## TAARIFA

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpe taarifa mzungumzaji. Tanzania ni nchi inayofuata siasa za ujamaa na kujitegemea. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest nunapokea taarifa hiyo?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Sijui bado kuna nafasi za uteuzi au? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaelewa mchango wa sekta binafsi kama tukiandaa mazingira mazuri ya watu binafsi, ya wafanyabiashara kufanya kazi katika mazingira wezeshi wataweza kuchangia sana katika uchumi wa nchi yetu. Nimeainisha kuna baadhi ya changamoto nyingi ambazo huwa tunaziongea hapa na zote zinafahamika zinazoikuta sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mlolongo wa tozo, tozo ni nyingi kila mmoja anajua. Tunakuja usumbufu na mlolongo wa kupata vibali, kila mmoja anajua sitaki kueleza, lakini ambacho nataka nongelee *specific* ni upatikanaji wa mikopo. Sekta binafsi itawezaje kufanya biashara au kujidoresha bila mikopo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto ya riba kubwa ya mikopo, nilikuwa napitia Taarifa ya *BOT* katika mwaka wa 2027 walifanya *review* ya riba za benki na wakawashushia kutoka asilimia walizokuwa wanatoa, leo wako asilimia 12, tisa mpaka asilimia tano kwa mwaka 2020 *reviewya* mikopo ambayo wanapata, lakini ukienda kwenye benki *specific* wananchi wafanyabiashara wakienda kuchukua mikopo wanachukua kwa shilingi ngapi? Huwezi kupata hata kwa asilimia 11. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mwingine wa kawaida; wataeleza sababu za kuweka riba kubwa waseme *risk* ni kubwa. Nimesoma pia kwenye ripoti anasema mikopo chechefu imeanza kupungua imetoka asilimia 11.6 imeenda mpaka asilimia 11.1 japo *projection BOT* wanasema ifike mpaka asilimia 5. Ni kwa nini tunakuwa na mikopo chechefu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu riba zinakuwa juu. Watu wanakopa fedha, biashara ni ngumu, *automatic wata-default*. Niiombe *BOT* niombe kuangalia au ku-review

sera yake ya fedha kuangalia namna ambavyo watawalazimisha mabenki waweze kushusha riba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano mwingine, na-*declare interest*, ni Mbunge na mnufaika wa mikopo, lakini mfano benki zikiwakopesha Wabunge, Wabunge ambao wana mishahara mikopo yao inakatwa *automatic*. Yani resk ya ku-*default* kwa watumishi au watu walioajiriwa ni ndogo kwa nini riba hazishuki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni lazima hili suala tuliangalie kama tunataka ku-*favor* sekta binafsi ziweze kufanya vizuri, ziweze ku-*access* mikopo na ni lazima mikopo iweze kushuka riba. *Otherwise* watakuwa wanachukua fedha benki wanafanya kazi za kwenda kusaidia benki na sio kuweza kupata kipato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini changamoto nyingine, changamoto ya vitambulisho vya *NIDA*. Ukienda kama mfano wilaya ninayotokea mimi, kuna mtu aliongeaongea hapa nataka nimpe taarifa; Kyerwa ninyi leo tumepata Rais wa Tanzania Kyerwa walikuwa tayari na Rais mwanamke kwa hiyo, Kyerwa wana Marais wawili wa Tanzania, mmoja Mama Samia mwingine sio mwingine ni mimi na yeje anajua. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Hoyo hoyo!

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nikiongelea changamoto ya vitambulisho vya *NIDA* naihusianisha...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia, ngoja tuelewane vizuri. Ulikuwa unagombea ubunge ama urais, ili tuelewe ni urais gani unaouzungumzia?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nagombea ubunge. Sasa ubunge ukishafikia *level* kubwa wanakuita Rais, yaani unakuwa Mbunge Rais. Rais wa jimbo. (*Makofi*)

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza changamoto ya *NIDA*. Naeleza changamoto ya *NIDA*...

**NAIBU SPIKA:** Kuna Taarifa Mheshimiwa Anatropia. Mheshimiwa Innocent Bilakwate.

## TAARIFA

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kunipa nafasi nimpe Taarifa Mchangaiji anayeendelea, Mbunge wa Jimbo la Kyerwa anaitwa Innocent Sebba Bilakwate na Mbunge huyu alimzidi huyo mchangaiji kura 15,943. Kwa hiyo, nampa Taarifa Mbunge anayetambulika ni Innocent Sebba Bilakwate, yeye ni wa kupewa tu. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aanatropia Theonest unaipokea Taarifa kutoka kwa Mbunge wa Kyerwa?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee. Ukiona mtu anajaribu kuji-*justify* anajua hajiamini na ha-*deserve*. (*Makofii*)

**WABUNGE FULANI:** Hoyo hoyo hoyo!

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, naongelea changamoto ya *NIDA* nikihusianisha na vikwazo wanavyopata sekta sekta binafsi. Na nitaongelea *specific* Kyerwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na nieleze nitakuja hapa nitatumia kanuni kuomba nitoe maeleo binafsi ya Mbunge juu ya changamoto ya watu wa Kyerwa ya ukosefu wa vitambulisho vya *NIDA*. Hawawezi kupata mikopo kwasaababu, ukienda kujaza formu ni lazima uweke namba ya kitambulisho cha *NIDA*. Hawawezi kupata bima za afya,

wale watu wanafanyaje? Na ile ni mikoa ambayo inapatikana mpakani kila siku unaambiwa wewe ni raia, wewe sio raia; hapo unafanyaje biashara katika mazingira hayo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwa, ni msimamizi wa jumla aiangalie Kyerwa kwa jicho la upekee hasa suala la vitambulisho vyta *NIDA*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tukitoka hapa nitaeleza kitu kingine. Leo kila mmoja mwenye simu tulioko humu ndani kama kuna *server* inaweza ikawekwa hapa unaweza ukafanya tathmini ni watu wangapi wanafanya miamala. Leo miamala ya fedha haifanyiki kama *luxury*, sio starehe, ni biashara. Watu wanafanya biashara, tuko ndani hapa biashara inaendelea, lakini tukirudi kwenye swali *bank charges* za hiyo miamala ya fedha ni kiasi gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, amekuwa analisemea mara nyingi sana. Kwamba, nikitumia simu yangu nimefanya muamala hapa, *sija-consume*, sijatumia huduma yoyote ya benki wala mtumishi ni kwa nini nakatwa fedha nyingi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo pia ipo kwenye miamala ya simu. Nimesoma kwenye ripoti ya *BOT* wamesema hivi, kwenye sera yao wamesema, kuna miamala takribani wamesema milioni 145 ambayo imefanyika katika *interval* tofauti ikihusisha *amount* zaidi ya *five billion*, lakini pia imehusisha watu zaidi ya milioni 22, unaona kwamba, ni idadi kubwa ya watu wanafanya biashara ya mitandao ya simu. Kwa hiyo, niombe Serikali, nimuombe Waziri Mkuu kuangalia namna gani wanaweza kushusha zile *charges* za simu ili watu wengi waweze kufanya biashara ili iweze kupunguza gharama ya ufanyaji wa biashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa mara nyingi nikiongelea hapa ninasema hivi kama Taifa tumekuwa tukitumia *new industrialized nation* kama *modal*. Zile *tiger*

*nations* kama *modal* ambazo zimejikwamua kutoka kwenye nchi za ulimwengu wa tatu kuwa ulimwengu wa pili na leo ni nchi zilizoendelea, sisi kama Tanzania tumekuwa tukifanya nini? Miradi mingi ambayo tumekuwa tukiifanya ni kiradi isiyogusa watu wengi, ameeleza Mbunge mmoja hapa, lakini pia *modal* tunazozitumia ni sahihi?

Mheshimiwa Naibu Spika, humu ndani kulikuwepo na sera wakati fulani wanasema sasa ni kilimo kwanza, wana magari yako *branded* kila kitu kilimo kwanza, lakini leo tunasema viwanda. Hivi kuna viwanda bila kilimo? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nataraji nione nguvu kubwa ikiwekezwa kwenye kilimo, lakini kwenye taarifa ambayo amewasilisha kwenye mpango aliowasilisha Waziri wa Fedha ameeleza kwamba, kilimo kimeshuka. Tena nimesoma kitu ambacho kimenisikitisha amesema hivi, ameeleza kwamba, kilimo kimeshuka kwasababu sitaweza kuiona kwa haraka, kimeshuka kwasababu watu wamewaza *alternative*; yaani watu wameamua kuwekeza kwenye vitu vingine, lakini hii nchi leo zaidi ya watu asilimia 80 wana-*rely* kwenye kilimo. Ina maana kama tunashindwa kuwezesha kilimo na viwanda itakuwa ni mijadala tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nisipoongelea kahawa kwa watu wa Kyerwa hawatanielewa. Hii ni zaidi ya mara 15 na katika mijadala yangu nitaongelea kahawa. Ninaongelea kahawa kwasababu, kuna shida, kungekuwa hakuna tatizo nisingeongelea kahawa; bado kuna changamoto ya soko bado kuna changamoto ya vyama vyaya ushirika. Na hapa nitamgusa ambaye anahuksika na uwekezaji na hiyo niseme ni changamoto nimesoma kwenye bajeti Fungu Namba 11 lililoanzishwa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji limetengewa bilioni 7 ambayo wamesema ni asilimia 0.02 kwenye bajeti kuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka leo twende kwenye uchumi wa kati sasa, sio kati chini, lakini Wizara au fungu la uwekezaji bado lina bajeti ndogo. Nadhani hata kamati wameeleza, wameeleza vizuri kabisa kwamba, hili

fungu liwekewe hata fedha ya maendeleo, hilo fungu liwezeshwe ili liweze kufanya kazi nzuri. Kama tunataka kwenda kwenye uchumi wa kati tunavyofika 2025 basi hayo maneno yawe *reflected* kwenye vitendo. Kwenye vitendo sio kuongea hap ani fedha iende na ionekane ikiwa inaenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho kabisa japo sio kwa umuhimu ni kuwashukuru ndugu zangu. Mungu awabariki, karibu Kyerwa baba. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naona akinamama wamewahi kweli kuyatafuta majimbo safari hii. Hii ni 2021 uchaguzi mwingine ni 2025...

**MBUNGE FULANI:** Hawapati.

**NAIBU SPIKA:** Twende taratibu. Tutaendelea na Mheshimiwa Vincent Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan na Mheshimiwa Amour Hamis ajiandae.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza napenda niipongeze sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu, imesheheni sehemu zote imegusa nyanja zote. Mimi nikiwa kama Mbunge wa Jimbo la Nkansi Kusini pia ni Mbunge wa Nkasi, Wilaya ya Nkasi, napenda kujikita katika upande wa kilimo kwa sababu sisi tunaotokea Rukwa, Nyanda za Juu Kusini, tusipoongelea kilimo ni shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi wameongelea suala la kilimo humu, napenda kuwaambia hivi wameongea wengi kuhusu utafiti, wako sahihi, lakini wanaenda kutafiti nini? Kilimo ambacho wanasesma wakulima wanalima wanazalisha mazao ya aina ipi? Ni *quantity* au *quality*? Wengi wamesema *South Africa* imeteka zao la Kongo, Zambia, sawa; tunaweza kuwa tunalima lakini tunalima mazao je, yana ushindani kwenye soko? Mbegu hizi ambazo tunawaambia watafiti waende wakatafiti, je,

watakuwa wanaotafiti wana nia njema na kutuletea mbegu zilizo bora ambazo zitaleta ushindani kwenye soko? Au ndio hao wanaokuja kusema kama bwawa la umeme halifai? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutafute watu sahihi. Mbegu zinazofaa ni aina gani ya mahindi ambayo inauzwa kwenye soko, sio bora tu kuzalisha. Kwa hiyo, unakuta Tanzania inazalisha mazao mengi, lakini mahindi yanayolimwa ni bora? Ndio yanayohitajika kwenye soko huko kwenye soko la kimataifa? Nchi Jirani zinahitaji aina ya mahindi hiyo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaweza tukawa tunalima mahindi, lakini sio bora kwenye soko hayapo na watafiti wakatuletea tu bora kuzalisha mahindi. Lakini ningependa hizi Wizara tatu hizi ni Wizara pacha. Wizara ya mambo ya Nje, Wizara ya Kilimo, Viwanda na Biashara hizi zinatakiwa ziende pamoja, lakini sijui kama wanakaa pamoja ili waone namna ya kuinua kilimo kwa ajili ya kuinua Taifa letu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Nje ya Nchi inatakiwa ikae itafute masoko kule ituletee jamani *Sudanwanahitaji* mahindi aina fulani, kwa hiyo kwenye utafiti tuleteeni mbegu wakulima wa Wilaya ya Nkasi kusini, Rukwa, Kigoma na Njombe walime aina fulani ya mbegu ndio tutakidhi kwenye soko la kitaifa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo, tunakuja kwenye suala la pembejeo, pembejeo imekuwa ni shida ni aibu mwaka huu watu wamepata hasara wakulima ambao wamejitahidi wamekuja watu feki katikati hapa wanaleta mbolea ambazo sizo hazina tija, sasa sijui kama Wizara inayorudi itatuletea majibu wale walioleta mbegu feki zingine zinatoka nje zingine zinaenda wapi, wakulima wamepata hasara kubwa mno wanatakiwa hao watu wachukuliwe hatua, wewe - *imagine* mkulima anatoa fedha zake anatembea kilometra 60 - 70 kumbe anakwenda kubeba mbolea feki, mbegu feki na Wizara ipo sio sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hii *speed ambayo* ni *legacy* ya mheshimiwa Rais Hayati John Pombe Joseph Magufuli, Rais hakuweza kuyafanya haya peke yake Rais ni taasisi ambayo ipo ndani Mheshimiwa Mama Samia yupo Mheshimiwa Hayati Magufuli yupo Mheshimiwa Naibu Spika upo Wabunge wote ni *legacy* ya Chama Cha Mapinduzi, mendeleo yote haya yanaletwa na Chama Cha Mapinduzi pamoja na *legacy* ya Waheshimiwa hawa wote kwasababu ni tasisi walikuwa wanaungana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli asingeweza vyote hivi bila kuungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mama Samia kwahiyu mtu anayekuja kutaka kubeza nawaomba Waheshimiwa Wabunge kwa umoja wetu tunaamini hawa ni asilimia ndogo sana hawawezi kutushinda sisi kama tulivyo kuweza kufuta *legacy* ya Mheshimiwa Rais ili waweze kufuta *legacy* ya Mheshimiwa Mama Samia Suluhu njembe ni mtekelezaji yeye ndiye alikuwa ni mtendaji yeye ndiye alikuwa *front line* pamoja na Waziri Mkuu. Hivyo hasi kama wanajaribu kubeza... (*Makofii*)

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa Sophia nitakupa fursa subiri.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kanuni zetu zinataka mtu akiwa anazungumza ndio anapewa taarifa lakini mzungumzaji haachi kuzungumza mpaka niwe nimemwita wa taarifa unatakiwa uendelee kuchangia mpaka nimpe fursa huyo anayesema taarifa.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, hongera sana.

**NAIBU SPIKA:** Sasa nikupe nafasi Mheshimiwa Mwakagenda japo kuwa mwanzoni ulisema mwongozo, mwongozo pia hauruhusiwi kuombwa wakati kuna mtu anazungumza, mtu akiwa anazungumza unaweza kuomba vitu viwili moja ni taarifa cha pili utaratibu kama kuna kanuni inavunjwa, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

## T A A R I F A

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante tunaendelea kujifunza bado nashukuru kwa kunielewesha, naomba nimpe taarifa mzungumzaji anayeongea kwamba sasa hivi tunazungumzia Wizara ya Waziri Mkuu tunaichangia hiyo na kutoa maoni yetu, na hakuna mtu yejote hapa ndani ya Bunge ambaye hataki maendeleo ya Taifa hili.

Kwa hiyo, nataka ajielekeze zaidi kwenye hotuba na kuweza kuijadili hiyo sote tunataka Tanzania iliyo bora, ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vincent Mbogo unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei yeye jana ameisifia *Standard gauge* amemsifia Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa hiyo *legacy* bado inaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana napenda nijikite tena kwenye upande wa Kilimo, kilimo upande wetu kimekuwa kwenye hali ngumu kutokana na hizi Wizara tatu...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** ...hizi Wizara tatu zingeweza kujikita kwa pamoja, moja isiteleze.... ....(*Makofii*)

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbogo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ngassa.

## T A A R I F A

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante napenda kumpa taarifa mzungumzaji Mheshimiwa Mbogo hiyo *Stigler's Gorge* anayoiongelea ndio ile Waziri wa Nishati amesema itawekewa maji tarehe 15 Mwezi 11 ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vincent Mbogo unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea kwa mikono miwili ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Sekunde tano malizia mchango wako.

**MHE. VINCENT P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana napenda kwenda kujikita kwenye upande wa uvuvi ziwa Tanganyika, ziwa lile bado halijatumika ipasavyo ukanda ule mapato yanapotea wavuvi wanakwenda kuvua nchi za jirani hawaji kuvua huku kwasababu ya mazingira sio rafiki na tozo, tozo ni nyingi mno mazingira sio rafiki na wavuvi, mabwawa yote, maziwa yote hata nchi za jirani kwa Tanzania nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bahari ya Hindi wanaziwa wanavulia Mombasa, ziwa Tanganyika wanakwenda Kongo, Burundi kwahiyoo tunapoteza mapato, naomba Wizara ikija hapa ijkite namna ya kutengeneza mazingira rafiki itakavyoweza kuwarudisha wavuvi tuweze kupata mapato Tanzania. Pamoja Wizara ya uvuvi itenge maeneo ya uwekezaji ijenge uvuvi, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga ahsante sana, Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan, atafuatiwa na Mheshimiwa Amour Khamis Mheshimiwa Josephat Kandege ajiandae. (*Makofi*)

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kuchangia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote niungane na watanzania wengine wenzangu waliota shukrani na pongezi zao kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi wa Chakechake, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ninatoa ahadi ya kwamba tupo nyuma yake tuna muunga mkono na tutampa kila ushirikiano atakaouhitaji kutoka kwetu Mungu amtie nguvu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni shukrani kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuleta hotuba iliyoshiba, iliyosheheni ambayo inaanishi maono ya Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hotuba ambayo imechukua mtazamo na mwelekeo wa Mheshimiwa Rais mpya aliyekuwa madarakani Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, (*Makofii*) (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchangia kwenye mambo mawili kwenye hii hotuba, jambo la kwanza ni *structure* ya utoaji wa mikopo iliyopo sasa. Moja katika maeneo ambayo tunajisifia sana *I feel very proud ni legacy* ilioachwa na Rais Hayati Dkt. Magufuli kwenye ujenzi wa zahanati zaidi ya 1,198 nchi nzima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tuna idadi ya zahanati zisizopungua 5,900 Tanzania, hili ni jambo zuri na la kuwa mfano kila mahali, tuna vituo vya afya visivyopungua 666 Tanzania nzima, kwenye uhai wa Mheshimiwa Magufuli kulijengwa vituo vya afya visivyopungua 487 Tanzania nzima. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunachokikosea kama Taifa ni kwenye *recruiting* ya wafanyakazi au watendaji au wahudumu wa kwenye hivyo vituo vya Afya. Wahudumu walivyo sasa hivi *ki-structure* tunahitaji *ma-clinical officer*

wengi zaidi na ma-*clinical officer* ni hawa vijana wenzangu ambao wanasoma diploma za *clinical officer* kwenye vyuo mbalimbali vyta elimu Tanzania ambao ndio hawapati mikopo. Mikopo sera yake ya elimu ya juu, mikopo wanapewa ma-MD ma-medical officers ambao wanaanza *degree* na kuendelea ambao hao baadae hawataki kwenda kukaa kwenye zahanati na vituo vyta afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hawawezi kwenda kuishi huko vijiji ni mtu akishakuwa na *degree* yake yaani hataki kwenda kuanzisha Maisha kwenye zahanati anajiona kama ni kudogo sana kwake. Kwa hiyo, watu ambao tunawahitaji wakae kwenye zahanati zetu hizi zaidi ya 5900 na vituo vyta afya zaidi ya 666 ni ma-*clinical officer* ambao wengi wao wanaanza na hatua ya elimu ya diploma kwenye vyuo vyta afya mbalimbali, ambao ndio hawapati mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu hapa ni kwamba lazima tutengeneze sera sasa. Aidha tubadilishe au tubadilishe sheria ili hawa watu wakopesheke wapewe mikopo ya elimu ya juu ili wasome wawe wengi wakatusaidie kwenye hizo zahanati zetu. Maana yake tukiwa tunajenga zahanati nyingi lakini mwisho zikiwa zinakosa watendaji hiyo itakuja kuwa kazi bure. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni upande mmoja upande wa pili au jambo langu la pili ambalo nilidhamiria kulichangia ni kwenye sekta ya utalii, wakati nachangia hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyekuja kuitoa hapa madarakani Hayati nilitoa mchango wangu kwenye jambo hilli, leo nataka niongeze zaidi. Kwenye llani ya Chama Cha Mapinduzi yenye *page* 303 kwenye *page* 207 Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi llani inampa *task* kazi ya kuhakikisha anakuza pato la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuitia utalii kwa kuongeza idadi ya watalii kutoka 500,000 hadi 800,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilivyo sasa hivi wastani wa watalii wanaoingia Zanzibarkwa mwezi ni katika ya 40,000 hadi 50,000 *statistic* niliyonayo hapa kwa Tanzania Bara kwa

mwaka 2020 hadi 2021 kumetembelewa na watalii wasiopungua 620,000, maana yake hiyo ni idadi ya watalii wanaoingia Tanzania kwa mwaka mmoja tu kwa Tanzania Bara, amba ni *task* aliyopewa Rais wa Zanzibarkwenye llani kwa muda wa miaka mitano kuifikia. Sasa ninachotaka kushauri hapa kuna umuhimu tena umuhimu mkubwa wa kufanya kazi kwa ushirikiano baina ya Wizara ya Utalii ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya Utalii ya Zanzibar. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naona huwa haiingii akilini na haiko vizuri ikiwa mgeni anafika Zanzibar anakaa siku saba anaondoka kurudi Ulaya hajafika bara, au anafika bara Ngorongoro anatua *K/A ana-spend* anaondoka baada ya siku saba hajafika *Zanzibar*. Wakati anakuja Tanzania ilivyo ni kwamba mifumo na ushirikiano baina ya Taasisi hizi ni kama haupo vizuri kidogo labda kuna zile *sentiment* za kwamba hizi taasisi sio za Muungano lakini sisi tunafanya kazi kama Taifa tunatakiwa tushirikiane ili kusaidia Taifa hili likipata pato lipate kwa jumla yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kuunga mkono hoja na huo ndio ulikuwa mchango wangu kwenye sehemu mbili ahsante sana naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, shukrani sana Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Kandege Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani ajiandae.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, *Bismillah Rahman Rahimu*, nakushukuru sana kwa fursa hii na kwasababu leo ni siku ya kwanza kabisa kusimama katika Bunge lako hili na Mwenyezi Mungu amejaalia kwamba ni siku ya mwanzo katika siku za Mwezi Mtukufu wa Ramadhan. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, basi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu *Sub-hanallah wa taala* kwa kutuwezesha sisi wote huku kuwa Wabunge na

kuhudhuria kwenye nyumba hii. Pili Chama changu Chama Cha Mapinduzi CCM lakini hasa hasa viongozi wake Mahsus Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli kwakuwa yeye alikiongoza Chama Cha Mapinduzi hadi leo nipo hapa kwenye Bunge hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Mama Samia kama msaidizi wake naamini walishauriana sana katika kupidisha majina yetu, kwa hiyo, nachukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Mama Samia Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu yenye manufaa ya duniani na akhera.

### **WABUNGE FULANI:** Amin!

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nisiwasahau Katibu Mkuu na Katibu wa Itikadi na Uenezi hawa ndio walitumwa kabisa kabla ya kampeni za uchaguzi walitumwa na Hayati Dkt. Magufuli kuja kupeleka ujumbe na *ku-test* mitambo pale Pemba kwa hiyo, tuwashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niwashukuru Spika na Naibu Spika kwa namna mnavyotuongoza kiasi ambacho leo najisikia kusimama hapa na kusema chochote yote hii ni kwasababu ya uongozi wenu. Katika hotuba hii ya Waziri Mkuu ambayo ni ya bajeti ya Wizara yake, naomba nichangie mambo machache sana..

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie jambo la kwanza ni Kilimo, kwa fikra yangu ili kilimo kiendelee ndani ya Tanzania, lazima tuwekeze fedha nyingi sana, na ili fedha hizi zipatikane lazima benki waondoshe riba kwa wakulima. Kwa sababu mkulima anapolima kule shambani alafu ukaja ukamkata riba, na shambani mazao yake akiyaoondo au akiyapeleka sokoni lazima pia kodi atoe kwa hiyo, tunakuwa tunamkata juu na chini kiasi ambacho tunamfanya mkulima akate tamaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana hii riba kutoka kwenye Benki iondolewe, na hili pia Mheshimiwa Hayati Dkt. Magufuli alilisema katika hotuba yake hii ni kuonesha kwamba riba kidogo inarudisha nyuma maendeleo. Katika kilimo hiki hiki kuna tafiti, watu wengi wamezungumzia kuhusu tafiti. Nilikuwa naomba kama kuna tafiti zozote basi zipelekwe kule vyuo vikuu wanafunzi waliopo pale watusaidie. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Halafu fedha ambazo zimepangwa kwenye Mawizara kwa ajili ya tafiti wapewe wanafunzi wetu wa vyuo vikuu kule ziwasaidie, sasa itakuwa sisi vyuo vikuu vinamanufaa gani kwetu ikiwa hadi sasa hatujaweza kusimamia tafiti zetu wenyewe kwa kupunguza gharama. Naomba sana hizi tafiti zipelekwe vyuo vikuu tunavyo vingi na fani tofauti kozi tofauti zinasomwa, naamini vijana wanawenza kufanya kazi hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili katika hotuba ya Waziri Mkuu nilikuwa naombi sana na ombi hili ni kuhusiana na sina hakika nitakachosema nipo kwenye sheria au vinginevyo. Lakini sisi tuna mifuko ile ya Jimbo na ile mifuko kwa upande wetu kule Pemba au *Zanzibar* inapatikana kidogo sana, na hapa kuna ahadi ya Mheshimiwa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli ya kumsaidia Rais wa *Zanzibar*.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonaje Serikali kwamba itaongeza katika kusaidia hili kumsaidia Rais wa Zanzibar kama hii mifuko itaongezwa kiwango pengine kutoka Milioni 20 zilizopo sasa hivi au pengine Milioni 50 kwa majimbo mengine bila kujali *formula* kwamba Jimbo lina watu wengi wapewe kiwango kikubwa basi sisi tuongezewe zile fedha angalau ifike Milioni 100 kwa Jimbo pale *Zanzibar* na iwe specially kwa *Zanzibar*. (*Makofî*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hizo hupati mzee.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine katika hili angalau bajeti

tunazozizungumza hapa katika kumsaidia Rais wa Zanzibar pale angalausilimia 10 kila Wizara ingekuwa inafikiriwa kupelekwa pale Zanzibar, Zanzibar leo ingekuwa Ulaya na watu wengi wangeipenda sana.

**MBUNGE FULANI:** Hamjashauriana kwa kweli!

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia mambo haya naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nadhani kwasababu umesema haufahamu kama lipo kisheria ama vipi lakini lipo kisheria na fedha pia zinatengwa kisheria kwa kadri ambavyo Bunge hili limetunga hiyo sheria. Tunaendelea na Mheshimiwa Josephat Kandege atafuatiwa na Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani Mheshimiwa Justin Nyamoga ajilande.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo niweze kutoa mchango katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kipekee naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na wasaidizi wake wote kwa hotuba nzuri ambayo hakika inaonyesha matumaini makubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipongeze Serikali kwa *ku-respond timely* kuhusiana na suala zima la Bima ya Afya kwa Watanzania wote. Walikuwa wamekusudia kwamba wangeweza kuleta Muswada mwezi Septemba lakini wamekiri kwamba kutokana na unyeti wa suala hili, basi ndani ya Bunge hili la bajeti wataweza kuleta Muswada huo ambao hakika sisi kama Wabunge tutakuwa na nafasi ya kufanya maboresho ili kile ambacho tunakusudia kwa ajili ya Watanzania kiweze kufikiwa. Naomba Serikali isiishie hapo, tumeanza vizuri hivyo ni vema mlango huu tukautumia ipasavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa siku ya leo nitachangia maeneo mawili nikipata nafasi na eneo la tatu. Eneo la kwanza ambalo naomba nishauri ni kuhusiana na hifadhi ya

jamii kwa ujumla wake. Kama tumeanza kutambua umuhimu wa afya za watu wetu ni vizuri sasa *in a holistic manner* tukatizana ustawi wa Watanzania kwa ujumla wake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo mfuko unasoma ni hifadhi ya jamii lakini ukienda kufuatilia ndani unakuta kwamba hiyo hifadhi ya jamii zaidi inawalenga watu ambao wameajiriwa Serikalini na zile sekta za kuajiriwa ambazo zinajulikana. Hata hivyo, sekta ya Watanzania walio wengi, zaidi ya 65% ambayo inaa jiri wakulima, wavuvi na wafugaji huoni dirisha ambalo limewekwa ili baada ya kuwa wamefanyakazi nzuri ya kujenga uchumi katika taifa hili waweze kuhudumiwa. Kila mtu ni mzee mtarajiwa watu hawa tunawasaidiaje ili baada ya kwamba wamefanyakazi nzuri waweze kuishi maisha ambayo ni *decent*, ambayo kila mtu anatamani? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine tunakuwa tuna-refer Biblia ambavyo siyo sahihi kwamba kwa mwanadamu ambaye amezaliwa na mwanamke miaka yake ya kuishi si mingi akiwa na nguvu 70 au 80 lakini mbona tukitizama wenzetu wanafika miaka 99 wao Biblia yao ikoje? Uki ja kutizama kwa ujumla unakuta ni namna ambavyo maandalizi yanafanya ili mtu huyu baada ya kwamba amefanyakazi kubwa ya kujenga uchumi aishi maisha ambayo ni *decent*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine tunasingizia kwamba unajua kwa *culture* yetu sisi Waafrika isingependeza mtu akishakuwa mzee atunzwe sehemu ambayo siyo pale alipozaliwa. Hii dhana nadhani imepitwa na wakati. Sisi ni mashuhuda pale ambapo tunakuwa na wazazi wetu na sisi tuko kwenye shughuli zingine jinsi wanavyopata taabu. Ni vizuri ifike wakati muafaka hawa watu ambao wamefanya kazi nzuri na kwa bahati nzuri kuna makundi ambayo vipato vyao viko tofauti tofauti, kuna wakulima ambapo kuna misimu ambayo wanapata fedha wanaweza wakachangia kwa utaratibu ambao utakuwa umewekwa, wavuvi wanaweza wakachangia katika utaratibu ambao utakuwa umewekwa na wafugaji

halikadhalika ili pale ambapo umri ukishafika pale anapohitaji kutunzwa awe na *option* yake kwamba katika kile ambacho amekuwa akichangia apate pesa au a-opt kwamba naomba niende katika maeneo ambayo yametunzwa maalum kwa ajili ya kutunza wazee. Maeneo hayo kutakuwa na madaktari na huduma zote ambazo ni muhimu ili wengine waonekane kwamba kazi waliyoifanya hawakupoteza juhudii zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali watutafutie fomula itakuwa ni sahihi ili kuwasaidia Watanzania hawa wengine ambao hawako kwenye kada ya utumishi Serikalini ili nao wafaidike ili tupate Watanzania ambao wanaishi miaka 99. Kama huko kwingine inawezekana kwa nini sisi isiwezekane? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo naomba kuchangia kwa siku ya leo ni kuhusiana na maendeleo kutofautiana kati ya mkoa na mkoa na halmashauri na halmashauri. Yapo mengine ni kwa sababu ya kihistoria hatuna wa kumlaumu imetokea hivyo na maeneo mengine yana uchumi mzuri kutokana na rasilimali zinazopatikana katika maeneo hayo. Sasa wengine wamefanyaje? Ili Taifa kwa ujumla wake kila eneo katika nchi hii liwe ni sehemu salama na ya kuvutia kuishi ni vizuri tukaja na *Development Equalization Fund* ambayo wale ambao wanazalisha *in excess* na wale ambao watakuwa *willing* na mtu yoyote yule aweze kuchangia ili sasa kama Taifa tutizame maeneo ambayo yanahitaji kusaidiwa kutokana na mfuko huo wasaidiwe ili kila sehemu ya Tanzania iwe sehemu salama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu ulivyo sasa hivi ukamchukua Mkurugenzi ambaye yuko kwenye Jiji ambalo lina vyanzo vingi vya mapato ataonekana anafanya vizuri sana lakini ukampeleka katika halmashauri ambavyo vyanzo vyake ni kidogo huyo huyo ambaye alikuwa anaonekana anafanya vizuri sana mtaishi kumfukuza kwa sababu inaonekana kwamba ha-perform. Lazima tuje na fomula ya kusaidia wale ambao wanahitaji kusaidiwa ili

tunyanyuke kwa ujumla kama Taifa. Mwananchi ambaye anaishi Newala atamani kuendelea kuishi Newala kulikoni kutamani kwenda Dar es Salaam kwa sababu inaonekana iko vizuri. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imegonga.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Katani Ahmed Katani atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Nyamoga, Mheshimiwa Zuena Bushiri ajilandeae.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue fursa hii kuungana na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini asiyeshukuru kwa kidogo hawezi kushukuru kwa kingi.

Nishukuru sana kwa huduma aliyotupa Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa Taifa hili la Tanzania. Bado alama aliyoiacha itakuwa kumbukumbu kwa vizazi na vizazi. Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba hii ya bajeti ya Waziri Mkuu nitajikita sana ukurasa wa 30 ambao umezungumzia sana suala la kilimo. Moja, nipongeze watu wa Wizara ya Kilimo ambao wanaleta pembejeo kwa wakulima, lakini ombi langu kwao walete pembejeo hii kwa wakati. Maeneo ya Masasi korosho zinaanza kupuliziwa dawa kuanzia mwezi wa sita mwanzoni kabisa. Hata baadhi ya maeneo ya Lindi ukienda kule Nachunyu Lindi korosho zinapuliziwa dawa mapema sana. Sasa ni matarajio yangu mkakati huu wa kuleta pembejeo ni vyema ziletwe kwa wakati sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nishauri sana Wizara hii ya Kilimo wakati wanaleta pembejeo wawaambie wakulima mapema sana ni kiasi gani cha fedha watakatwa ili wawe na *awareness* kwamba hizi pembejeo wanazopewa leo bure siyo kwamba wanapewa bure ni ili baadaye waweze kulipa. Sasa ni vizuri mkatoa mchanganuo wanachotakiwa kulipa kwa wakati huu kabla ya kufika wakati wamelima, wamevuna *then* ukaléta tu mchanganuo ambao unaweza ukawachanganya wakulima. Hili nishauri sana lifanyike sasa mapema ili liweze kutusaidia. (*Makofí*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye ukurasa ule wa 30 umezungumziwa mfumo wa *TMX*, niipongeze Serikali imesema mfumo ule kwa sasa hautatumika. Kwenye hili nataka nitoe takwimu ili Wizara ione kwamba *TMX* kwa sasa haifai. Msimu wa korosho 2016/2017 tumeuza korosho mpaka Sh.4,000, msimu wa korosho 2015/2016 tumeuza korosho mpaka Sh.3,700. Hata hivyo, *TMX* ambayo imeanza kufanyiwa majaribio kwenye korosho na ufuta msimu wa mwaka jana kwenye korosho za Tandahimba zile za *TANECU* kwenye tani 51,000 *TMX* imeuza tani 4,600. Ukioanisha na bei *TANECU* wameuza bei kubwa zaidi ya Sh.2,700 ukilinganisha na *TMX* ambayo imeuza kwa Sh.2,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wanunuzi wake wa *TMX* ni wale wale wanaokwenda kwenye mnada wa kawaida. Sasa kwa namna hiyo tumeshaona wazi kwamba *TMX* imefeli. Kama kuna majaribio ya kwenda kufanyabiashara *TMX* isiwe kwenye korosho na ufuta huku kwenye korosho na ufuta uachwe utaratibu ule ambao umezoleka ambao ni mfumo wetu wa Stakabadhi Ghalani ambao wenyewe umeleta tija kwa wakulima, kwa misimu mitatu wakulima wamepata neema imekuja *TMX* hamna kitu. (*Makofí*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nipongeze hotuba maana Waziri Mkuu amesema *TMX* isitumike nisitisize haimfaí mkulima siyo wa korosho tu hata wa pamba, watu wa pamba msiingie kwenye huu mtego. *TMX* ni mtego mkubwa sana, sisi wa kwenye korosho tumefanya majaribio

tumeona kati ya mnada wa kawaida na mnada wa *TMX*, wa kawaida umekuwa bei juu kuliko *TMX*. Kwa hiyo hii, *TMX* ni ugonjwa ambapo naomba Wizara ya Kilimo msiujaribu kabisa, uondoeni kwenye mfumo, hauwafai wakulima hata kidogo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nasisitiza sana hili kwa sababu hii tumeiona. Niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge kwenye korosho kuna kitu kinaitwa *moisture* ni unyaufu ambapo korosho ikiwa mbichi ukienda kuipima unapokwenda kwenye mfumo wa *TMX* kwa ajili ya kusema unapeleka *sales catalogue* kule mnunuzi anaporudi huku akakuta korosho iko tofauti *TMX* hana msaada wowote kwa mkulima. Mfumo wetu wa kawaida mnunuzi anakwenda anaiona korosho, tunaposema korosho hii auta ni 51 anaiona *site pale*, huyu *TMX* kwanza wanunuzi wake ni hawa hawa madalali siyo wenyewe wa Ulaya, hawa wanaofanya *TMX* ni akina Alibaba wako Ulaya na mambo yao yanaenda hivi. Kama mnaweza kuleta viwanda vya kubangua korosho mka-process korosho, mnaweza mkafanya *TMX*, lakini kwa hii *raw cashewnut* tuachenî kwenye mfumo huu tuliokuwa nao na tuliouzoea tutamsaidia mkulima kwa namna kubwa sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, hili mtatusaidia ninyi watu wa *TRA*, kuna mashine hizi za *EFD*, sisi wengine kule tunafanya biashara kidogo. Tuliambiwa tukinunua mashine zile tutarejeshewa fedha baadaye. Tumelipia Sh.590,000 mpaka Sh.600,000 lakini ukikaa baada ya muda fulani unakwenda ku-*upgrade* ile mashine unalipia shilingi 80,000. Sasa mbona tunapokwenda kwa wenzetu hawa wa *TANESCO* wakishatupa *meter* tumeshamaliza, sisi tunalipia tu kila wakati kwa nini? Sasa hawa wa *TRA* na *EFD*, moja, waturudishie fedha kama walivyosema maana ni mali yao ile siyo mali ya mfanyabiashara, *EFD machine* ni mali ya *TRA*, ni mali ya Serikali.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Justin Nyamoga atafuatiwa na Mheshimiwa Zueno Bushiri, Mheshimiwa Shamsia Aziz Mtamba ajiandae.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kushukuru kwa nafasi hii niliyoipata. Nichukue fursa hii pia kukishukuru Chama cha Mapinduzi kwa kuendelea kusimamia llani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwanza kwa kuleta shukrani kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Kilolo. Wengi wameshukuru uongozi wa Rais wetu Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa mambo makubwa aliyooyafanya. Wananchi wa Kilolo wanamshukuru na watamkumbuka kupidia mambo mbalimbali ambayo waliyapata katika kipindi cha awamu iliyopita na wamenitura nishukuru kwa mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanashukuru kwamba Mji wa Ilula ambao haukuwa na maji kwa miaka mingi sasa una maji ya kutosha na ni kupidia utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi. Wanashukuru sana Wizara ya Maji kwa kuwapatia maji watu wa Mji wa Ilula. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Kilolo wanashukuru kwa mara ya kwanza kwenye vijiji wamepata barabara ya lami kilomita 18 kutoka Kidabaga - Boma la Ng'ombe. Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI ametembelea ameona barabara ile inaendelea kujengwa. Wanashukuru sana na watamkumbuka Hayati Dkt. John Joseph Magufuli kwa jambo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wanashukuru kwa sababu wamejengewa hospitali ya wilaya. Wanaishukuru sana Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwamba kwa mara ya kwanza Wilaya ya Kilolo ina hospitali nzuri ya mfano ambayo itatibu watu wengi na watu wale wataondokana na kero waliyokuwa nayo ya maradhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mengi yaliyofanyika ambayo wananchi wa Kilolo hawatamsahau Dkt. John Joseph Pombe Magufuli katika uongozi wake niliona nitaje hayo machache. Kwa niaba ya wananchi ambao wamenituma, hayo yamefanyika na yanaonekana na ndiyo ambayo ni kielelezo cha utendaji mzuri wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hao pia wamenituma nikumbushe mambo machache kwa Serikali hii sikivu. Jambo la kwanza wameniomba nikumbushe kwamba ile barabara ambayo ni ahadi ya kutoka Iringa Mjini kwenda Kilolo hadi Idete bado barabara ile inaendelea kujengwa lakini haijakamilika. Wanaamini Serikali hii sikivu itatekeleza hilo kwa sababu imo kwenye ahadi na kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wananchi hawa wa Kilolo wanakumbusha kwamba mara kwa mara viongozi waliotembelea pale Kilolo akiwepo Waziri wa TAMISEMI, Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda kwa kuona ukubwa wa Halmashauri ya Kilolo waliahidi kuigawa Halmashauri ile na kuwa Halmashauri mbili na pia kuelekea kugawa lile eneo kuwa Majimbo. Jambo hili lipo TAMISEMI hasa la halmashauri na wananchi wale wa Kilolo wanaombwa kupata majibu ni lini sasa halmashauri ile itagawanywa ili kupata halmashauri mbili ili kurahisisha utekelezaji wa mambo mbalimbali hasa kuleta karibu huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wanakumbusha kwamba kuna ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu alipofanya ziara ambayo ni ya kituo cha afya pale katika Mji wa Ilula. Nayo pia wanaikumbusha kwamba Serikali iangalie na kwa

kuwa hii ni bajeti ya Waziri Mkuu basi wanaomba kukumbusha hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwa ujumla wake niendelee kukumbusha ajira kwa vijana hasa walioko katika shule za sekondari ambao wanajitolea; walimu wa kujitolea kwenye shule mbalimbali wa masomo ya sayansi. Wako wengi hata katika Jimbo la Kilolo lakini na katika maeneo mbalimbali, hilo pia tunakumbusha kwamba liendelee kuangaliwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze kwenye....

**NAIBU SPIKA:** Kengele imegonga Mheshimiwa.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukruu sana, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zueno Bushiri atafuatiwa na Mheshimiwa Shamsia Aziz Mtamba, Mheshimiwa Hamis Hussein Tabasam Mwagao ajiandae.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ili nami nichangie kuhusu hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu 2021/2022. Mimi nitajikita zaidi katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na kazi ambazo amezifanya katika Taifa hili la Tanzania. Pia niipongeze Serikali kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya afya katika nchi nzima ya Tanzania. Pia niipongeze Serikali kwa kutoa dawa na vifaa tiba katika maeneo mengi ya zahanati zetu pamoja na hospitali zetu nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mipango mizuri ya Serikali tumeweza kujenga miundombinu mingi katika nchi yetu. Kwa mfano, tumepeata vituo vya afya vya kutosha, zahanati za kutosha na hospitali za rufaa nyingi nchini Tanzania. Hata hivyo, kila lenye mafanikio lazima tukubali kuwa litakuwa na changamoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika zahanati hizi ambazo zimejengwa zimekuwa na uhaba wa madaktari pamoja na wauguzi. Utakuta maeneo mengine hasa maeneo ya vijiji zahanati moja inahudumiwa na daktari mmoja wakati wanaoitumia ni zaidi ya vijiji viwili au vitatu. Niiombe Serikali sasa ione umuhimu wa kuongeza bajeti katika sekta hii ili zahanati na hospitali zetu ziweze kupata watumishi stahiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna upungufu wa dawa. Nadhani Wabunge wenzangu wote wanakiri kwamba hospitali zetu zimebakia madaktari kwa *professional* zao ambazo wakishakuandikia dawa unaenda kutafuta hela ili ukununue wewe mwenyewe, maeneo mengi dawa hazipatikani. Niiombe sasa au niishauri Serikali iweze kuongeza bajeti katika sehemu hii ambapo dawa zinahitajika sana ili wananchi wetu waweze kupata haki stahiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba ugonjwa wa *COVID-19* umetingisha sana nchi yetu, kumekuwa na upungufu wa mitungi ya gesi. Wananchi wengi wanaoishi vijiji wanaopata magonjwa yale wanakosa *oxygen* na hivyo kuhatarisha maisha yao kwa sababu unapotaka kupata mitungi ya oxygen ni lazima uende katika hospitali kubwa za mikoa, halmashauri au rufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali sasa, ili kuwasaidia wale wananchi ambao wapo vijiji, Serikali itenye fedha za kutosha ili iweze kupeleka mitungi hii hata katika ngazi ya zahanati ili kuokoa wananchi wetu walioko vijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijatendea haki wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro kama nitakuwa sijachangia hospitali ya Rufaa ya Mawenzi katika Jengo la Mama na Mtoto. Hospitali ya Mawenzi ina jengo la Mama na Mtoto ambalo limejengwa tangu 2008. Ni takribani miaka 13 sasa jengo hilo halimaliziki. Hospitali ya Mawenzi inatibu wilaya saba za Mkoa wa Kilimanjaro. Kwa hiyo, ukienda katika wodi ya zamani ambayo pia ni chakavu kwa majengo, unakuta wanawake wanalala wawili wawili; mmoja anageuzia kichwa huku na mwingine kule na vitoto vyao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika hili Serikali iweze kutenga fedha ili iweze kumalizia jengo lile na wanawake waweze kujifungua salama na katika maeneo ambayo ni mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba. Atafuatiwa na Mheshimiwa Hessein Amar na Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, ajiandae.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya nzuri na leo hii nimeweza kusimama katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mionganoni mwa matatizo makubwa yanayowakabili wananchi wa Jimbo langu la Mtwara Vijijini ni maji. Ifike wakati Serikali itoe fedha kwa ajili ya kusambaza maji kutoka Mto Ruvuma hadi kwa wananchi wangu. Sijui kwa nini suala hili limekuwa gumu wakati Serikali ilitenga fedha na wananchi walifanyiwa uthamini mwaka 2015 ili mradi huu uanze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Mtwara Vijijini lina kata 21, lakini ndani ya kata hizi 21, zote zimekuwa

na changamoto kubwa sana ya maji ikiwemo Kata ya Mango pacha nne. Kata hii tokea tumepeata uhuru haijawai kabisa kufurahia huduma hii ya majisafi na salama. Nikija Kata ya Libwidi, nayo imekuwa na changamoto kubwa sana ya maji; halikadhalika na Kata za Naguruwe, Kata ya Mkutimango, Kata ya Mbalawa na Makome, Kata ya Naumbu na Pemba Pwani nazo zimekuwa na changamoto kubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mkoa wa Mtwara kiujuimla tuna changamoto kubwa sana ya maji, ndio maana tunataka mradi huu wa Mto Ruvuma ufanye kazi. Mradi huu wa Mto Ruvuma utaleta manufaa kwa maeneo mengi. Sitafaidika mimi katika jimbo langu tu, wanaweza kunufaika kwa kaka yangu Mheshimiwa Chikota; kwa kaka yangu Mheshimiwa Katani; utakwenda Nanyumbu; watakwenda Songea na Namtumbo. Kwa hiyo, mradi huu wa Mto Ruvuma una faida sana na utanufalsha maeneo mengi wataweza kupungukiwa na kero hii ya maji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mtwara uchumi wetu mkubwa ni Korosho. Naomba katika Bajeti hii, zao hili la Korosho lisiyumbishwe yumbishwe, mwachie bodi ifanye kazi yake. Naiomba Serikali irudishe Mfuko wa Pembejeo. Mfuko huu ulikuwa ni mkombozi kwa mkulima wa Korosho. Kwa hiyo, wananchi na wakulima wa Korosho wa Mtwara wamenituma, ni lini Mfuko huu wa pembejeo utarudishwa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyindi nikisimama ndani ya Bunge nimekuwa nikizungumzia sana masuala ya matibabu kwa wananchi hasa kwa wananchi wangu wa Mtwara Vijijini. Kusema kweli wamekuwa wakipata taabu sana wanapokwenda katika hospitali zetu hasa wale wenye magonjwa makubwa kama moyo pamoja na figo. Wapokwenda katika hospitali zetu wanakuta Madaktari Bingwa hakuna, wanaambiwa waende Muhimbili. Kutokana na uchumi wa watu wetu wanashindwa kwenda Muhimbili. Hivyo, naishauri Serikali iweke utaratibu angalau kwa miezi miwili au mmoja wawe wanatuletea Madaktari Bingwa katika mikoa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uvuvi iboreshwe hasa katika Jimbo langu la Mtwara Vijijini. Sekta hii napenda iboreshwe katika maeneo yafuatayo: wavuvi wapewe elimu ya kisasa, wapatiwe mikopo na vyombo vya kisasa vya uvuvi kama mashine za boti, nyavi, ndoana, pamoja na vifaa vingine. Pia wavuvi wapewe semina mbalimbali za kuwajengea uwezo ili kuhifadhi hifadhi ya bahari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na doria mbalimbali katika bahari zetu. Jeshi la Polisi wamekuwa wakifanya doria mbalimbali, lakini wavuvi wamekuwa wakilalamika kupigwa pamoja na kuchomewa nyavyo zao. Kwa hiyo, naomba wasitumie nguvu kubwa, watoe elimu ya kutosha kwa wavuvi. Wakikamilisha haya, Serikali na Halmashauri wataweza kupata mapato ya kutosha kutookana na uvuvi. Pia zitengwe bandari maalum kwa ajili ya uvuvi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Amar. Atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Chaurembo na Mheshimiwa Grace Tendega, ajiandae.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kusimama hapa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuunga mkono hoja iliyopo mbele yetu ambayo ni hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa kweli imesheheni na imegusa maeneo yote, hususan kwenye maendeleo ya nchi yetu. Vile vile niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa kipindi chake cha miaka mitano kuweza kutuingizia fedha nydingi za maendeleo katika Wilaya ya Nyang'wale zaidi ya shilingi bilioni 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuendelea kutekeleza yale yote ambayo yaliyoanzishwa na Hayati Mheshimiwa Dkt. John

Pombe Magufuli, tunamuunga mkono kwa nguvu zote Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, tuko naye bega kwa bega na ninawaomba Watanzania waungane na wananchi wa Nyangh'wale kuwalaani wale ambao wanayaponda na kuyapuuza mazuri yalioanzishwa na Hayati Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia maeneo machache sana. Namwomba Waziri wa Fedha na Waziri wa Viwanda mnisikilize vizuri. Kuna changamoto nyngi kwenye upande wa kodi na huwa nalizungumza kila mara, lakini hamlichukuli maanani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha anisikilize vizuri. Nimeshauri mara nyngi sana tupanue wigo wa kukusanya kodi. Kuna maeneo mengi sana tunapoteza kodi na mnasema wale ni wafanyabiashara wadogo lakini wanapoteza mapato ya Serikali. Mfano, ukienda Chako ni Chako pale, ukiangalia yule mtu anauza kuku zaidi ya 300 kwa siku moja, lakini mtu huyo hatoi risiti. Hilo ni eneo moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, nilishasema kwamba *TRA* na wafanyabiashara kuna usiri mkubwa. Kwa nini nasema hivyo? Leo hii wafanyabishara wenye maduka, ushahidi ninao, nimeamua kujilipua Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba unilinde; baadhi ya maduka, katika maduka 10, matatu tu ndiyo yanayotoa risiti. Maduka saba hayatoi risiti na ushahidi ninao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nimekwenda kwenye duka fulani Dar es Salaam muda wa saa saba mchana, nikanunua bidhaa zaidi ya shilingi 200,000/=, wamenifungia mzigo. Wakati nataka kuondoka nikawaambia nipeni risiti, wanadai kwamba hapa tangu asubuhi anayetoa risiti hayupo. Mauzo kiasi gani Serikali imepoteza fedha pale? Naomba lifanyieni kazi. Kama utataka ushahidi zaidi, niko tayari kuvala kofia na kanzu iliyoisha, niende na kuonesha maeneo ambapo upotevu wa fedha za Serikali upo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa ushauri kwa upande huo. Hakikisha kwamba unawasajili wafanyabiashara wa kat i ama wafanyabiashara wadogo, wagawie zile mashine ya *EFD* ili waweze kutoa risiti. Nakuomba Mheshimiwa Waziri achukue ushauri mwingine, punguzeni *VAT* kutoka kwenye asilimia 18 na iende mpaka 13 ili watu waweze kulipa *VAT*. Huo ni ushauri wangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme jambo lingine. Walipa kodi wa nchi hii juzi nilisikia ni takribani milioni 3.9, lakini kuna walipa kodi zaidi ya milioni 3.9 amba hamjawasajili na wapo, fanyeni utafiti wa kina. Hizi fedha mnazosema mnakusanya shilingi trillioni mbili kwa mwezi ni kidogo sana. Mimi ni mfanyabiashara, ni mchimbaji, ninaelewa. Tuliweza kulisaidia Taifa kwenye upande wa madini, tulitoa ushauri na leo hii Waziri wa Madini yuko pale, anazungumza kwa kutamba, yuko vizuri, Wizara yake inakusanya pesa vizuri. Nakuomba Mheshimiwa tuiteni wafanyabiashara tuweze kusema yaliyoko kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania hao wafanyabiashara hawana nia ya kukwepa kodi ila kuna matatizo upande wa *TRA*. Tunaomba mtuite tuje tutoe ushauri. Pia hatuwezi kusema yote hapa; siwezi kumwaga mchele kwenye ndege wengi, kwa sababu kuna mapapa wapo amba wanapoteza mapato makubwa ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa *TBS*. Leo hii ukienda Dubai ukaléta mzigo unaozidi dola 5,000, *TBS* watakupiga faini ya asilimia 15, lakini kuna watu wale mapapa wanaingiza makontena na hawatozwi hiyo *TBS*. Leo hii mnaenda kuwakamua hao watu wadogo, watu wachache lakini kuna mapapa wapo. Mheshimiwa nitafute kwa wakati wako na unilinde nitakupa siri za wafanyabiashara amba wanapoteza mapato ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Fedha japokuwa siyo jambo la kawaida, ila nafikiri safari hii ungewafuata wewe wafanyabiashara. Kwa sababu biashara ziko tofauti kutoka mkoja mmoja na mwininge. Ni vizuri uwafuate ili kila mahali uelewe changamoto zao ni zipi kutegemeana na mazingira yao, kuliko wao kukufuata wewe halafu wanaongea watu wacheche wengine hawapati fursa. Kwa hiyo, michango kama hiyo inakuwa kidogo mtihani. Wafuate wewe huko huko kwenye mikoa yao wakueleze biashara zilizoko huko ili upande hizo fedha zinazotafutwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Tendega na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, ajiandae.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuwepo leo nikiwa hai. Pili, namshukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuweza kuongea katika kikao hiki cha leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwa ufinyu wa muda nianze kwa kuzingatia kanuni ya 175 katika Kanuni zetu za Kudumu. Pili, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri aliyeitoa. Kwa kweli ukiisoma ile hotuba, imelezea mambo mengi yaliyofanyika katika nchi hii na kwa kweli mambo yale yamefanywa na viongozi wetu wakubwa kwa Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba natoe ushauri mdogo sana kwa Serikali, lakini tukiufanya kazi tutaweza kudhibiti uvujaji wa mapato katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kufuatilia miaka yote sioni *forum* ya kisheria inayompa nguvu Mkuu wa Wilaya aweze kusimamia mapato yanayopelekwa katika Halmashauri zetu kutoka Serikali Kuu. Serikali Kuu inapeleka kwenye Halmashauri zetu, zaidi ya asilimia 80 ya mapato zinaiendesha Halmashauri zetu. Mapato yale yanapofika

kwenye Halmashauri zile basi Mkurugenzi anafanya yale anayoyataka bila kupata *concern* ya Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri iundwe *forum* maalum ya kumfanya Mkuu wa Wilaya awe Mwenyekiti; Mkurugenzi awe Katibu; Wabunge wa Majimbo na Viti Maalum wawe Wajumbe wa *forum* hiyo. *Forum* hiyo nashauri iitwe Kamati ya Maendeleo, Nidhamu na Utawala. Kamati hiyo itatusaidia sana kudhibiti mapato katika Halmashauri zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niseme ya watu wa Jimbo la Mbagala. Sekta ya Afya katika Jimbo letu la Mbagala tunayo ile Hospitali ya Wilaya ya Zakiem. Nadhani ni hospitali pekee katika nchi yetu yenye *level* ya wilaya isiyokuwa na wodi za kulaza wagonjwa. Naiomba sana, Serikali tuipe hadhi hospitali illi tuweze kupata wodi za kulaza wagonjwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, katika Sekta ya Elimu, sote tunafahamu katika Jimbo la Mbagala, ndiyo jimbo lenye shule zenye wanafunzi wengi nchi nzima. Shule ya Maji Matitu ina wanafunzi zaidi ya 9,000. Naiomba sana Serikali ilisaidie Jimbo la Mbagala kulipatia shule za kutosha. Katika hili namwomba dada yangu Mheshimiwa Jenista, ndugu zetu wa *NSSF* wana maeneo mengi wasiyoyaendeleza. Tunaomba sana mtupe maeneo yale yaliyokuwa Tuangoma twende tukajenge shule.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie katika kuzungumza suala la *TARURA*. Barabara nydingi katika Jiji letu la Dar es Salaam zimekuwa na matatizo makubwa. Mheshimiwa Rais amesema, Halmashauri zetu huko nyuma zilikuwa zinatenga fedha zaidi ya shilingi bilioni nne kila Halmashauri katika *ku-service* barabara zile. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri utaratibu ule uendelee kurudiwa ili fedha zile zikiunganishwa na fedha zinazotoka

kwenye *Road Fund* ziweze zikafanye kazi kubwa. Kuna Kata ya kama ya Kiburugwa na Kata ya Mianzini iko hoi katika suala nzima la barabara.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Grace Tendega, atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda na Mheshimiwa Tecla Ungele, ajiandae.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nitajikita hasa katika sehemu mbili na kama kuna muda nitaongeza, lakini najikita katika ajira pamoja na elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumzia ajira, ni kwa ajira kwa watu ambao wana ujuzi wa kutosha kufanya majukumu katika ajira hizo. Namaanisha *Skilled Labor*. Tunapozungumzia uchumi wa kati ambao tumeshaingia; katika hotuba hii nimeangalia sijaona vizuri namna ambavyo tumedadavua vizuri kupata ajira vizuri kwa vijana na wengine, lakini pia ajira yenye ujuzi. Nina maanisha nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapozungumzia ajira, nazungumzia ajira na watu ambao wana ujuzi wa kutosha kufanya majukumu katika ajira hizo, namaanisha *skilled labour*. Sasa tunapozungumzia uchumi wa kati ambao tumeshaingia uchumi wa kati, katika hotuba hii nimeangalia sijaona vizuri namna ambavyo tumedadavua vizuri kupata ajira vizuri kwa vijana na wengine, lakini pia ajira yenye ujuzi inamaanisha nini? Tumejikita kutoa elimu mpaka kufikia Vyuo Vikuu, kupata *degree* na na tunavyoandaa hawa watu wakiondoka pale, hawa wanakuwa katika *level ya managerial*, yaani wanakuwa ni *supervisors*, lakini katika *level/ile ambayo ni watendaji kazi ambao wapo hasa katika VETA*, hatujikita sana. Hapa ndipo tutaandaa wale

watenda kazi, ambao watasaidia kuinua uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia vyuo vya VETA vilivyopo, siyo mikoa yote ina VETA, lakini kama mikoa yote haina VETA, bado Walimu wanaokwenda kufundisha wanafunzi wetu ni wachache na vyuo vinavyotoa ni vichache. Kwa hiyo hapa sasa ndio Serikali ijikite katika *ui-invest* huko, kuhakikisha tunapata Walimu wazuri ambao watakwenda kufundisha, yaani hao *technicians* watakwenda kufundisha VETA ili tuweze kupata watu ambao ni *skilled*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya nusu ya Wabunge tuko hapa kila mmoja utakuta mtu anakuuliza kuna ajira wapi, vijana wanatuuliza, wanasema nataka ajira, lakini tumeweka ajira kama kitu ambacho watu wamefika *university*, lakini kumbe mtu akifunzwa vizuri kuhusu nyanja yake kwa mfano tukisema wafanyakazi wa majumbani *qualified*, wafanyakazi wa saloon *qualified*, *gardeners qualified*, tuwapate wapi watu ambao ni *qualified* katika nyanja tofauti hawa ndio watapata kipato na pia wataweza kuajiriwa kwa sababu wana ujuzi na wanaweza kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji kutengeneza *middle class* wengi ili tuweze kupata kodi na Serikali iweze kuijendesha. Sasa Serikali, hajajikita hapo. Tukiangalia katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kitengo *Vote 65* ambapo walitengewa bilioni moja mpaka nazungumza hapa hajatoka. Hii inaonesha kwamba bado Serikali haiko *serious* kuangalia ajira kwa vijana. Kwa hiyo naomba Serikali iweze kuangalia hivyo na Serikali ihamasish, kuna *short courses* za mambo hayo. Serikalini hawazungumzi kwamba kuna *short courses* ya hiki, hiki, hiki. Watu wakifikiri ajira anajua aende akasome, amalize *form six*, aende mpaka chuo kikuu, lakini hao wanaomaliza darasa la saba kwenda mpaka kidato cha nne tunawapeleke wapi? Tuandae katika bajeti yetu, waende wakafanye kazi waweze kuleta uchumi wa nchi hii, wafanye kazi inayotakiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wezetu China mwaka 2017 walikuwa na *technicians* milioni hamsini. Sasa na sisi tukijewekea malengo angalau wanafunzi hao wanaomaliza darasa la saba mpaka *form fourtuwa-train* katika hizo kada, wote wanaofanya *decoration* na *whatever hivyo tutafika mbali*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, napenda nikazie pia hawa Walimu ambao wanapata *diploma* kwenye *DTE* hao Walimu ni muhimu, wako wachache, unakuta nyumba wamekutengenezea mlango, mlango haupendezi, lakini *finishing* kama hii wanafundisha pale na ndizo ajira, tunahitaji tupate vitu hivyo vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kimoja nataka tuzungumzie kwa watu wenyе ulemavu, watu hawa wamekuwa wakitozwa kodi, niombe Serikali itoe kodi kwenye vifaa ambavyo ni vya watu wenyе ulemavu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Shukrani sana. Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, atafuatiwa na Mheshimiwa Tecla Ungele na tutamalizia na Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutuwezesha kufanya kuendelea kufanya kazi ya Taifa letu ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wote ambao wanamsaidia, Makatibu Wakuu na watumishi wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambao

kazi hizi nzuri ambazo tunaziona zimefanywa kwa juhudzi zao. Ukimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu bila kumshukuru Mheshimiwa hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli unakuwa hujakamilisha shukrani, maana huyo Waziri Mkuu ni matunda ya Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Mwenyezi Mungu amuweke mahali pema. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata bahati sana ya kufanya kazi muda mrefu kwenye chama chetu. Nimeanza kazi ya uongozi mwaka 1988 na sasa nina miaka 33 nikiwa mjumbe wa NEC. NEC yenye nimekaa miaka 15 lakini nimeshika vyeo mbalimbali kwa muda wote wa miaka 33. Hata hawa baadhi ya makada na Wabunge wenzangu wanaosema hapa wengine walio wengi wamenikuta humo, wengi wote akina Kibajaji, akina Msukuma, akina January Makamba na wengine walio wengi. Niliowakuta ni akina Mheshimiwa Lukuvi hapa, kwa hiyo kwenye chama chetu nimekaa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niseme jambo moja. Nakijua sana chama chetu, naujua uwezo wa chama chetu katika kusimamia mambo yote ya msingi ya uongozi wa Taifa na hata ndani ya chama chenyewe. Kunapofika kuna jambo lolote ambalo wewe ni kama Mbunge, au ni mwana CCM au ni mwananchi una mashaka lipeleke kwa CCM litapata majibu. (*Makofij/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipopata msiba wa kiongozi wetu, wengi tulihuzunika sana, kwa sababu kwanza hatukuamini na pili, tulihuzunika kwa sababu bado tulikuwa tunamhitaji, lakini la tatu, tulihuzunika kwa sababu tulijiuliza nini hatima ya Taifa letu baada ya kuondoka kwake. Sisi makada tuliobobe vinenoneno vingine tunavyoviona vinapita tulivitarajia. Ninachokionba, sisi wenyе mapenzi mema wenyе kujua kazi ya Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, tutumie busara sana katika kusema jambo lolote tunaloliona linatokea. Inawezekana akatukana mtu halafu wewe ukasimama kusema, ukawa wewe unatangaza tusi badala ya kusaidia. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui kama naeleweka vizuri? Umesikia neno huko, ulipime, hili ni la kwenda kusema au ni la kuliacha, maana chama chetu kinao uongozi imara kinaweza kupata majibu ya matatizo yote tuliyonayo. Naomba niseme kama mjambe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, lakini nimo ndani ya Bunge; tabia ya mtu kujipa ukaka wa Taifa, kujipa udada wa Taifa, kujipa ushangazi wa Taifa, unakemea, unaweza ukakosea unaweza uka-overdo, tuache. Kama unaona jambo fulani lina shida, lipeleke kwenye chama chetu, litapata majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wabunge ningependa sana tuishi kwa kuheshimiana, kustahiana, hiki ni chombo kikubwa Watanzania wanatuangalia, wanarushiana vineno visivyokuwa na maana na wakati mwingine kama mwenzako hujaelewa vizuri alichokisema, pata muda wa kujifunza, hakuna kitu kibaya kama kumtafsiri vibaya mtu aliyesema vizuri, halafu umeshamchafua unajuliza utarudije kumsafisha. Kwa hiyo nimesimama hapa kwa kweli kusema jambo hilo, chama chetu kina majibu yote ya nchi yetu juu ya matatizo ya wananchi na chama. Mtu asijipe jukumu lolote kubwa, ajue chama kipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ningependa niseme hivi, nimepongeza kazi nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nimesikiliza hapa mchango wa ndugu yangu Mheshimiwa Shabiby juu ya *TARURA*, niseme nami nataka kuongezea jambo moja kwenye *TARURA*. *TARURA* haina tatizo tu kwenye bajeti au kwenye mahusiano na *Councils* bali ina tatizo hata la kimuundo ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *TARURA* kuna mtu anaitwa *regional coordinator* yupo mkoani, huyo ndie anayetangaza tenda, ndiye anayetoea kazi, ndiye anayelipa, ndiye anayeweza kuvunja mkataba, hawa *District Manager* wa *TARURA* wamekaa kama sijui nitasemaje, yaani nitafute neno gani, lakini wanafanya *supervision* ambayo hawana nguvu nayo. Kwa hiyo, tunapokwenda kuipa nguvu *TARURA* kwa kuongezea fedha, lazima tuangalie muundo wake,

tugatue madaraka kutoka juu tuyarudishe chini, kwa Mameneja wa Wilaya wa TARURA. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa nilizungumze, sisi wa Kigoma tulivyosikia *Standard Gauge* inaanza Mwanza, tukanung'unika nung'unika, unajua sisi hapa ndio ingekuwa na *impact* ya kiuchumi na nini, lakini kupanga ni kuchagua, tulikwisha chagua Mwanza, hakuna tena kurudi kuangalia huku na kule.

Hata hivyo, inakuwaje huku mnapelekea *standard gauge*, halafu hii *narrow gauge* ambayo ilikuwepo huku ya mkoloni inaachwa hivyo. Hali ya reli yetu ni mbovu sana hasa kutoka Dodoma kwenda Kigoma. Maeneo mengi ni mabovu. Nimemwona Waziri Mkuu amekuja na mpango wa kununua mabehewa na vichwa vya treni, tunashukuru sana hilo ni moja ya tatizo, lakini na ile reli ikarabatiwe katika kiwango cha kufanya wanaosafiri wawe na uhakika na maisha yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali si nzuri na niwaambie katika hali ya kawaida, unajua watu wakiwa wanalamika mbona *standard gauge* imeanza huku, basi hii ya kwao mbovumbovu mnawatengenezea na wenyewe ili kuwafuta machozi kulikoni waendelee kubaki.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, muda umeisha! Naunga mkono hoja na nashukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tecla Ungele tutamalizia na Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutupatia uhai na hata sasa tunaendelea kuhudumu katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ya bajeti iliyosheheni matumaini makubwa katika mwaka 2021/2022. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia kwenye maeneo mawili; la kwanza kuhusu watumishi wa Idara ya Afya; kwa uzoefu na *observations* nyingi za Mkoa wa Lindi, vituo vingi vya afya vinahudumiwa na wahudumu wa afya yaani *Medical Attendants*. Sasa hii inaathiri utoaji wa huduma ya dharura ya uzazi yaani *CEmONC* na hiyo itaashiri kufikia malengo ya kupunguza vifo vya akinamama wakati wa ujauzito na kujifungua. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitolea mifano michache tu, najua wilaya zote zina shida hizo, lakini mfano Kituo cha Afya cha Nanjilinji, kimepata huduma nzuri za majengo na tunashukuru Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, lakini watoa huduma ambao wana ujuzi hawapo. Kunapotokea dharura ya uzazi, mzazi huyo anakimbizwa kwenye Hospitali ya Wilaya jirani ambayo ni Ruangwa ambapo kuna kilomita 44 kutoka Nanjilinji, tofauti na kutoka Nanjilinji kwenda Hospitali ya Wilaya Kinyoga kule Kilwa ambayo kuna kilomita 174.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara inayotoka Nanjilinji kwenda Ruangwa nayo sio nzuri, ni barabara ya vumbi lakini pia inapita kwenye Mto Nakiu ambao hauna daraja, sasa masika kama haya ukijaa, hebu ona sasa hapo, mgonjwa yule ni mama anayehitaji kujifungua, anayehitaji *operation* ya kujifungua, lakini anashindwa kuvuka pale na *ambulance* unayo lakini kuna shida. Mkoa wa Lindi una shida sana una changamoto za huduma za afya, majengo tumepata tunashukuru na vifaa sehemu nyingine vipo, lakini watoa huduma ni wachache. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchangia kwenye miundombinu, Mkoa wa Lindi kuna sehemu chache sana ile barabara kutoka Kibiti – Lindi – Masasi – Tunduru – Songea; ni hiyo tu ndiyo ya lami, lakini tunaomba ile barabara ya kutoka Masasi – Nachingwea; Nanganga – Ruangwa;

Ruangwa - Nachingwea, Nachingwea – Liwale; na Nangrukuru -Liwale, tunaomba ijengwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna changamoto ya barabara za vijjini; natolea mfano kwa sasa ni masika, barabara zingine hazipitiki, mfano barabara ya kutoka Mipingo kwenda Mnyangara mpaka kule Namapwia ambako anatoka yule mjisusi unayemsikia, sasa hivi hakupitiki kabisa. Pia kuna barabara ya kutoka Hoteli Tatu kwenda Pande na Lihimalyao kwenyewe ni changamoto kubwa. Pia kuna barabara inayotoka Somanga kwenda mpaka Kibata, nako ni changamoto; kwa ujumla barabara za vijjini Mkoa wa Lindi kuna changamoto kubwa. Jamani, tafadhalii tunaomba mkoa ule uangaliwe kwa jicho la pekee ili kuwanusuru wananchi wale, ili nao angalau na wenyewe wachangie kwenye maendeleo ya nchi hii na wajisikie kwamba kwenye nchi yao ya kufaaldi matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi kwanza nitoe pole kwa Mheshimiwa Rais mama Samia, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Spika na wewe Naibu Spika kwa kuondokewa na kipenzi chetu Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Watanzania kwa ujumla tunajipa pole sana kwa msiba huu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasikitika sana, kuna baadhi ya watu muda si mrefu, hayati Dkt. Magufuli tangu tumemzika wameanza kuzungumza mambo ya ajabu, nashangaa! Msiba huu uliotukuta mama Samia, Waziri Mkuu wamezunguka nchi hii kututafutia kura sisi, kila mahali Waziri Mkuu amekwenda huku, Makamu wa Rais na ndio ambaye ni Rais amekwenda huko na ndiyo tumerudi hapa Waheshimiwa Wabunge. Leo mtu anasimama na watu

wengine kwenye mitandao ya kijamii kumtukana na wengine ni kwa sababu wamekosa vyeo na kadhalika na ndiyo wanaosema maneno ambayo hayaeleweki, vyeo atatoa kwa watu wangapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wamelia, Naibu Spika umelia machozi, Spika wetu amelia machozi, mama Samia mliona analia machozi, Marais wastaa fu amelia machozi, Mwinyi amelia machozi, walikuwa wanalilia nini? Wanalia kwa huzuni kwa sababu tumeondokewa na kipenzi cha Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mtu mwingine anasema nilipougua nimepigwa risasi kule Nairobi hakuja kunitazama, alikuja mama Samia. jamani Wabunge tuwe wakweli, hivi ndani ya familia ukimtuma ndugu yako baba au mama si ndio wewe umekwenda kumtazama, sasa alitaka afanyiwe nini, amekwenda Makamu wa Rais ambaye sasa ni Rais kwa kutumwa na Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Kwa hiyo, lazima tushukuru kwa kila jambo ndugu zangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Wanamakambako au wananchi wa Jimbo la Makambako wamenitura, wanahuzunika sana na wanamtakia kila la kheri mama Samia, pamoja na Waziri Mkuu watekeleze wajibu wa Watanzania.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga kuna taarifa Mheshimiwa Msukuma.

## TAARIFA

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Napenda kumpa taarifa mzungumzaji kuhusiana na machungu yaliyopo kwa Watanzania kwamba, ndiyo maana kuna mzungumzaji amezungumza mchana humu anasema kwamba, baadhi ya Wabunge wakikosoa isionekane nongwa. Sisi tunaona nongwa kwa sababu wakosooji wote waliokosoa ni watu waliokula viapo, sasa viapo huwa vinaendelea hata kama umetolewa kwenye

madaraka. Tutaendelea kuwapiga mpaka watambue umuhimu wa kiapo walichokiapa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga, malizia mchango wako.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nimeipokea taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika bajeti hii ndio Mtendaji Mkuu wa Serikali, sasa naomba nizungumzie changamoto, kazi kubwa zimefanyika katika Jimbo la Makambako na Tanzania kwa ujumla, lakini kwa leo naomba nichangie changamoto. Changamoto ya kwanza, tuna tatizo la fidia katika Mji wa Makambako, kuna wananchi wanaokaa katika eneo lile la Polisi, wananchi hawa wameanza kuishi pale kabla ya Polisi kupewa eneo lile mpaka sasa wanaishi maisha magumu, hawawezi kuendeleza kufanya kitu chochote.

Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake, Mheshimiwa Jenista dada yangu wahakikishe tunalipa fidia kwa wananchi hawa na *IGPSirro* namwamini sana, anafanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya pili, katika fidia pale Idofi, Idofi inajengwa *one stop center*, Serikali imepeleka fedha zaidi ya milioni 800 na kitu, zilizobaki tunaomba zimaliziwe ili wananchi wale waishi kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya tatu katika fidia, kuna soko la kimataifa, walilipwa watu zaidi ya bilioni tatu, milioni mia moja na kitu, wamebaki watu kumi na nane, wanapata tabu, tunaomba Serikali imalizie katika kulipa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya nne katika fidia, kuna umeme wa upepo Mheshimiwa Dkt. Kalemani nimekwenda kwake zaidi ya mara mbili. Naomba wakae walitatue tatizo hili la kuwalipa wale wananchi fidia kwa ajili ya umeme wa upepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa afya, tumepewa zahanati nyingi, tumejenga katika Mji wa Makambako, wananchi wamefanya kazi hiyo pamoja na Madiwani, pamoja na mimi Mbunge. Tuna hospitali, tuna kituo cha afya, tunaomba vifaa tiba ili zahanati hizi pamoja na kituo cha afya kipo Lyamkena pale, kiweze kuanza. Tuna hospitali ya Halmashauri na kadhalika, tuna kituo cha afya ambacho kimeanza kujengwa kule Kitandililo ambacho Mheshimiwa Diwani na wananchi wake na mimi Mbunge wao tumeanza kukijenga, tunaiomba Serikali iunge mkono jitihada za wananchi ambazo zimeanzwa kule Kitandililo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho si kwa umuhimu, kwenye Halmashauri yangu ya Makambako, Madiwani posho wanayoipata kwenye kikao ni tofauti na halmashauri nyingine. Naomba Waziri Mheshimiwa Ummy yuko hapa, tafadhalli niombe sana kupitia Waziri Mkuu, Madiwani hawa wapewe posho sawa na halmashauri zingine, kwa sababu nikiwatatajia hapa wanapata kiduchu na ninajua tatizo lililopo Makambako lipo katika halmashauri nyingi. Niwaombe sana safari hii Madiwani hawa wapewe posho kama wanavyopewa wengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge kama tulivyokubaliana kwa hoja ile iliyokuwa imetolewa ya kubadili muda tutakuwa tunamaliza muda kama huu kipindi chote hiki cha Ramadhani. Baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.07 Jioni Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 15 Aprili, 2021, Saa Tatu Asubuhi)*